# HOTUBA ILIYOFUNULIWA

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Hotuba Iliyofunuliwa

Khutbah Ilhaamiyyah (Arabic)
(Swahili Translation)

Tafsisi ya Kiswahili ya Khutbah Ilhaamiyyah (Kiarabu)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza (Kiarabu): 1902
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +25522110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover designed by Usman Nasir Choudhary

**ISBN:**
978-1-84880-520-0
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

ٹائیٹل بار اول

هذا هو الكتاب الذي ألهمت حصة منه من رب العباد ـ في يوم عيد من الأعياد ـ فقرأته على الحاضرين ـ بإنطاق الروح الأمين ـ من غير مدد الترقيم والتدوين ـ فلا شك أنه آية من الآيات ـ وما كان لبشر أن ينطق كمثلي مرتجلاً متخطراً في شرع هذه العبارات ـ وكان الناس يرقبون طبعه رقبة يوم العيد ـ ويستطلعون بعيون المشتاق المريد ـ فالحمد لله الذي أدام مقصودهم بعد الانتظار ـ ووجد وأمطرهم كبستان مذللة أغصانه من الثمار ـ وأنه صنيعة إحسان الحضرة ـ ومطية تبليغ الناس إلى السعادة وأنه غيث من الله بعد ما أمحلت البلاد و عم الفساد ـ ولن تجد هذه المعارف في الآثار المتلقاة المدونة من الثقات ـ بل هي حقائق أوحيت إليّ من رب الكائنات ـ وأنه إظهار تام وهل بعد المسيح كتم ـ وهل بعد خاتم الخلفاء على السر ختم ـ وليس من العجب أن تسمع من خاتم الأئمة ككلمات ما سمعت من قبل من علماء الملة بل العجب كل العجب أن يأتي المسيح الموعود والإمام المنتظر وحَكَمُ الناس وخاتم الخلفاء ثم لا يأتي بمعرفة جديدة من حضرة الكبرياء ويتكلم كتكلم العامة من العلماء ولا يفرق فرقاناً بين الظلمة والضياء ـ وإني سميت هذه الرسالة

# خُطبَةً إلهَامِيَّةً

## وإنّي علّمتُها إلهاماً مِنْ ربّي وكانتْ آيةً

تعداد الاشاعة ۲۱۰۰

ثمن نسخة واحدة عمر ۸/

وإنها طبع في مطبع ضياء الإسلام قاديان باهتمام الحكيم فضل الدين البهيروي في سنة ١٣١٩ من الهجرة المقدسة

## Jalada la chapa ya kwanza

Hiki ni kitabu ambacho sehemu yake nimefunuliwa siku ya Idi moja, toka kwa Mola wa watu, nami nikawasomea waliohudhuria kwa kutamkishwa na Roho Mwaminifu pasipo kuiiandika na kuihariri. Bila shaka hii ni ishara mojawapo miongoni mwa ishara nyingi. Binadamu hawezi kutongoa mfano wangu bila kujiandaa papo hapo mithili ya ibara hizi. Na watu walikuwa wanaingojea hotuba hii ichapwe, jinsi wanavyoingojea siku ya Idi, na kutaka kuiona kwa macho ya mwenye shauku na utashi. Basi sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyewaonyesha makusudio yao baada ya kusubiri sana na wakapata matulubu yao kama bustani ambayo mitunda yake imegooka. Na hili ni tendo la hisani ya Mungu na ni rikabu kuwafikisha watu kwenye bahati njema. Na hii ndiyo mvua toka kwa Mungu iliyonyesha baada ya nchi kuwa kama na ufisadi kutapakaa. Na hutapata katu maarifa haya ndani ya maandishi yaliyochaguliwa na kupangwa na wenye kutegemewa, bali haya ni mambo ya kweli niliyofunuliwa na Mola wa ulimwengu. Na huu ndio ushindi kamili. Na je baada ya Masihi kuna taficho, na je baada ya Khatamul Khulafaa kuna muhuri juu ya siri? Na hamna ajabu kwamba utasikia toka kwa Khatam wa Maimamu elimu za ndani msizosikia hapo kabla toka kwa maulamaa wa dini, bali ingekuwa ajabu sana kwamba aje Masihi Mau‘udi na Imamu anayetazamiwa kufika na Mwamuzi wa watu na Khatamul Khulafaa,

lakini asilete maarifa mapya toka kwa Mungu Mtukufu na alonge kama walongavyo maulamaa wa kawaida wala asitenganishe kwa uwazi kiza na mwanga. Nami nimekiita kitabu hiki:

**HOTUBA ILIYOFUNULIWA**

Nami nimefundishwa kwa njia ya ufunuo, na hii ndiyo Ishara.

Na imechapishwa katika Matbaa Dhiyaul Islam Qadian chini ya usimamizi wa Al-Hakiim Fadhlud Din wa Bhera mnamo mwaka 1319 Hijra

Bei: Rupia 1 Anna 8 Idadi: 2100

# NENO LA MWENEZI

Hii ndiyo tafsiri ya 'Khutbah Ilhaamiyyah' aliyotoa Hadhrat Masihi Mau'udi[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, tarehe 11 Aprili 1900, siku ya Idi al-Adha, kwa lugha ya Kiarabu.

Hotuba yenyewe inaanzia na maneno 'Enyi waja wa Mungu, zingatieni…' (uk. 49) hadi maneno 'na Mwenye habari zao Atawatanabahisha' (uk. 64). Ndani ya hotuba hii akaeleza kwa ufasaha hekima na falsafa ya kuchinja dhabihu. Milango minne ya baada ya hotuba na baadhi ya matangazo na maelezo ya pembeni aliviandika baadaye, na kitabu kizima kilichapwa mnamo mwezi Oktoba 1902.

Khuhusiana na sehemu ile ambayo ndio 'Hotuba Iliyofunuliwa', Seyidna Ahmad[as] ameandika ndani ya kitabu chake Hakikatul Wahyi kama ifuatavyo:

> 'Tarehe 11 Aprili 1900, siku ya Idi al-Adha nilifunuliwa saa za asubuhi, 'Leo utoe hotuba kwa Kiarabu, nawe umejaaliwa uwezo; na pia nilifunuliwa: 'Kalaamun Ufsihat min ladun Rabbin Kariim.' Yaani, ndani ya maneno haya, ufasaha umetiliwa na Mola Mkarimu… Ndipo nikainuka baada ya sala ya Idi kutoa hotuba ya Idi. Na Mwenyezi Mungu Anajua kwamba nilijaaliwa uwezo maalum kutoka ghaibu. Na kinywani mwangu mlikuwa mkitoka papohapo hotuba kwa lugha yenye ufasaha ya Kiarabu iliyokuwa zaidi ya

uwezo wangu. Sifikiri kuwa hotuba iliyokuwa na kurasa kadha mtu yeyote duniani anaweza kutoa kwa ufasaha na balagha hivyo bila kuandika kwanza juu ya karatasi, pasipo ufunuo hasa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wakati hotuba hii iliyoitwa 'Hotuba Ilhamiyya' iliposomwa, idadi ya wahudhuriao pengine ilikuwa karibu mia mbili. Subhanallah. Wakati huo chemchem toka ghaibu ilikuwa inafunguliwa. Sielewi kuwa ni mimi niliyekuwa nikisema ama malaika fulani alikuwa anasema kwa ulimi wangu, kwani nilikuwa natambua kuwa simo ndani ya usemaji huo. Sentensi zilizotungwa tayari zilikuwa zinatoka zenyewe mdomoni mwangu, na kila sentensi ilikuwa ishara kwangu. Huu ndio muujiza wa kielimu Alioonyesha Mungu, na hakuna yeyote awezaye kuleta mfano wake!

Sipendi kuwakawilisha zaidi wasomaji wenye hamu ya kujua aliyosema Masihi Mau'udi[as] katika hotuba yake ya kimuujiza.

Hatimaye shukurani nyingi kwa Sheikh Ansar Hussain aliyepanga kwa shauku herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha fometi.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 15 Julai 2020

## TANGAZO

Enyi ndugu toka Arabuni, Uajemi, Siria na nchi nyinginezo za Kiislamu! Jueni, Mwenyezi Mungu Awahurumieni, kuwa nimeandika kitabu hiki kwa kufunuliwa na Mola Wangu, nami nimeamrishwa niwaiteni kwenye njia niliyoongozwa kwake na kuwafundisheni adabu zangu. Na hii ndiyo baada ya kukatika tamaa toka kwa maulamaa wa nchi hii na imethibitika kuwa hawaijali Nyumba ya Akhera na mwendo wao kwenye ukweli ukazuilika kwa faliji ya kuzuliwa si kwa faliji ya kweli. Athari ya dawa yoyote haikuwafaa wala juhudi ya tabibu, wala hayakubaki katika nch yao malisho kwa ajili ya farasi bora wa maarifa wala haitarajiwi toka kwa wenyeji wa nchi. Hapo nikatiliwa moyoni mwangu na Mungu Mtukufu kwamba nielekee kwenu kutafuta msaada ili muwe wasaidizi wangu kama wenyeji wa Madina. Na yule aliyenisaidia na kunisadikisha, huyo amemridhisha Mola wake na Mbora[saw] wa mahuluku. Na wanyama wabovu zaidi ndio wale watu walio viziwi, mabubu wasioelekea kwenye haki na hekima wala hawasikilizi hoja hata kama ni miongoni mwa hoja imara fika. Na wanapoambiwa aminini yaliyowajieni toka kwa Mola wenu, yaani haki na dalili bayana, baada ya siku za kukithiri madhehebu na kuhitilafiana kwao na kuchafuka kwa bahari ya upotevu, husema hatuelewi haki ni kitu gani, nasi tumewakuta baba zetu juu ya itikadi fulani nasi tutakuwa nayo hadi siku ya kufa. Nami sikuwaambia

isipokuwa iliyonena Kurani. Na jawabu lao halikuwa ila matusi na maneno maovu. Mwenyezi Mungu Alinijulisha kuwa Isa bin Mariamu[as] ameishafariki na ameungana na wafu, na yule aliyekuwa ateremke toka mbinguni ndiye aliyesimama baina yenu kama nilivyofunuliwa toka kwa Mungu Mtukufu. Na uhakika wa kushuka[1] ulikuwa ni kudhihiri Masihi Mau'udi wakati wa njia zote kukatika

---

[1] Jueni kuwa neno *nuzuul* — kushuka — limechaguliwa kwa ajili ya Masihi Mau'udi kwa sababu mbili: (1) Mojawapo ni kwa kudhihirisha kukatika kwa njia ya kiardhi kama vile serikali, utawala na nyenzo za vita ndani ya nchi alimotumwa toka kwa Mungu Mmoja. Tuseme, hii iliashiria kwenye jambo hili kwamba Masihi Mau'udi atatokea ndani ya ile nchi ambamo haitabaki kwa Islam nguvu wala kwa Waislamu uwezo wowote, hata hivyo watamkataa na watataka kuzima nuru ya Mungu badala ya kuwa miongoni mwa wasaidizi. Hivyo, atasaidiwa na Mola wa mbingu na hatakuwa na hisani ya mfalme kati ya Wafalme wa ardhi wala wenye madola wala matajiri, wala hatatumia upanga wala mkuki, kana kwamba ameteremka toka mbinguni, na Mwenyezi Mungu Amemsaidia na kumwauni. (2) Ya pili ni kudhihiri umashuhuri wa Masihi Mau'udi haraka sana katika wakati na zama kidogo ndani ya nchi zote. Kwani kinachoshuka toka mbinguni huwa anakiona kila mmoja aliye karibu au mbali na katika pande na jiha mbalimbali, na halibakia pazia juu ya macho ya waadilifu, na kinashuhudiwa kama umeme unaomulika toka upande mmoja hadi upande mwingine na unazingira pande zote kama duara. Mwandishi.

na unyonge wa dola la Kiislamu na ushindi wa makundi ya maadui. Na hii iliashiria kwenye hili kwamba hii yote itashuka toka mbinguni pasipo kukata shingo na kuwaua maaudi, na kwa mwanga wake itaonekana kama jua. Lakini wenye kuchukua maana ya dhahiri wakaichukulia istiara hii kidhahiri, na huu ulikuwa ni msiba wa kwanza ulioushukia umati huu. Mwenyezi Mungu hakutaka kutokana na 'kumteremsha' Masihi ila kuonyesha mkabala wa dini mbili wazi wazi. Kwani Nabii wetu Mteule[saw] alikuwa mithili ya Musa[as], na silsila ya Ukhalifa wa Kiislamu uikuwa mithii ya silsila ya Ukhalifa wa Musa[as] toka kwa Mungu aliye Mjuzi. Basi hakuna budi kwa ajili ya kushabihiana huku na kwa mkabala huu kuwa mwishoni mwa silsila hii adhihiri Masihi kama Masihi wa silsila ya Musa[as], na Wayahudi kama Wayahudi waliomkufurisha Isa[as] na kumkadhi-bisha na wakataka kumwua na kumfikisha kwa wenye madaraka. Na ni ajabu kwamba maulamaa wa Kiislamu wamekiri kuwa Wayahudi walioahidiwa katika zama za mwisho sio Wayahudi kwa hakika, bali ndio Waislamu walio mfano wao kimatendo na kitabia. Hata hivyo wanasema kwamba Masihi atashuka toka mbinguni naye ndiye kwa hakika mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu, si mithili yake miongoni mwa mawalii. Ndiyo kusema kwamba wameufikiria umati huu kuwa mbovu na mbaya sana miongoni mwa nyimati, kwani wamedhani kwamba Waislamu ndio watu ambao ndani yao hamna hata mmoja awezaye kuitwa kuwa yu mithili

ya baadhi ya watu bora waliopita, lakini mithili ya wenye shari wamekithiri kati yao. Hivyo, fikirini, Enyi kundi la wenye akili!

Kisha suala la kushuka kwa Isa, Nabii wa Mungu, lilikuwa miongoni mwa bidaa za Manasara. Ama Kurani, basi hii inamfisha na kumwingiza ndani ya wafu. Na Manasara walishurutishika kuzua itikadi hii mbovu katika siku za kukata tamaa na kufa moyo kupata msaada ulioahidiwa. Kwani, Wayahudi walikuwa wakiwadhihaki na kuwaudhi kwa maneno ya namna namna walipoona kutelekezwa kwao na kunaswa kwao katika maafa, na walikuwa wakisema yuko wapi Masihi wenu aliyekuwa akidhani kuwa atakirithi kiti cha kifalme cha Daudi na atapata utawala na kuwaokoa Wayahudi? Hapo wakaudhika Manasara kusikia shutuma hizi. Wangesubiri mpaka lini juu ya shutuma hizi, basi wakazua majibu mawili wakati wa shutuma na lawama hizi mbili. Wakasema, ingawje Yesu bin Mariamu hakupata Usultani katika kipindi hiki, lakini yeye atashuka kwa sura ya wafalme wakali, wenye ghadhabu katika zama za mwisho na kukata mikono ya Wayahudi na miguu yao na pua zao na kuwahilikisha kwa adhabu kali na dhila. Na baada ya kuwaadhibu huku, atawaketisha wapendwa wao juu ya viti vya enzi vilivyoahidiwa ndani ya Kitabu. Ama kauli ya Masihi kwamba watakaomwamini, atawaokoa katika taabu zilizowashukia wana wa Israeli, basi maana yake ni kwamba atawaokoa kwa damu yake katika dhambi, si

katika dhuluma ya serikali ya Kirumi kama inavyodhaniwa na kusemwa.

Hivyo, kimuhtasari ni kwamba kukaa kwa Manasara muda mrefu katika misiba kulipowaudhi na Wayahudi wakatumia midomo michafu kuhusiana na habari zao na wakawahesabu kuwa wenye kuhasirika na kushindwa, dhihaka hii ikawaumiza, basi wakazusha itikadi mbili zilizotajwa ili kuwanyamazisha maadui. Ni tabia ya binadamu kuyashikilia matamanio wakati wa kuvuma pepo kali za kukatisha tamaa. Na aonapo kuwa hayakubakia matarajio, ajifurahisha nafsi yake kwa matamanio, na anataka kitu kisichoweza kuingia katika mawazo wala kisichosikika masikioni isipokuwa kwa nadra. Pengine anataka alkemia anapoishiwa mali, pengine anaelekea kutiisha nyota, na kushughulikia kupiga falaki na kadhalika. Hivyo Manasara walipopata pigo la kauli za maaudi, na hawakuwa na mahali pa kukimbilia ili kuepukana na balaa hili, basi wakazua waliyozua na kuyategemea matamanio kama ilivyo sera ya asira na mfungwa. Basi wakaeneza mafundisho haya mawili kama ujuavyo na uonavyo, na wakatimiza haki ya upofu. Na wakati ambapo itikadi ya Masihi kushuka ikawa sehemu ya tabia yao na ikazingira ufahamu na mazoea yao, basi bila shaka shauku yao yote ilihusikana na ushukaji wa Isa[as] ili aje kuwaangamiza maadui zao, na kuwakalisha juu ya viti vya heshima na enzi. Basi hii ndiyo sababu ya kusambaa kwa itikadi hii ndani ya madhehebu ya Kikristo. Mfano wao ndani ya Islam

unapatikana katika Shia. Kwani, zama za kunyimika ziliporefuka kwao na hakuibuka mfalme kati yao kwa karne nyingi, wakazusha wenyewe kuwa Mahdi wao amejificha ndani ya pango, naye atatoka katika zama za mwisho na kuwahuisha masahaba wa Mtume[saw] wa Mungu ili awaue kwa kuwatesa. Na ingawaje Husain[ra] bin Ali[ra] hakuweza kuwaokoa katika dhuluma ya Yazid, lakini yeye atawaokoa kwa damu yake katika adhabu kali siku ya mwisho. Kadhalika kila aliyehasirika na kushindwa akajua jawabu hili. Na nimepata kusikia kwamba wafuasi wa dhehebu la Mawahabii wa Kihindi, mithii ya madhehebu hayo wanamngojea Sheikh wao Seyid Ahmad Barelawii, nao wakapitisha umri wao majangwani wakimngojea. Basi, hao wote wanastahili kuhurumiwa, kwani hadi sasa hata mmojawapo kati ya wakubwa wao hakurejea, bali waliowangojea wakawarejea na majuto mengi yalioje nyoyoni mwa walioenda kuzikwa makaburini!

Hivyo, kiini cha kauli ni kwamba itikadi ya Masihi kurejea na kuwa hai ilikuwa ni ubunifu wa Manasara na uzushi wao ili wapate utulivu na kukomesha masingizio ya Wayahudi. Na Waislamu wakajiingiza humo pasipo sababu yoyote na wakanaswa bila wavu, na wakala sumu bila kupata utamu. Na walipokubali nguzo moja miongoni mwa nguzo mbili za dini ya Kikristo, basi kuna maana gani kuikataa nguzo ya pili, yaani kafara? Tumeeleza kwa utondoti mambo haya yote ndani ya kitabu hiki, na kama u mtafutaji wa haki, hayo

yakutosha. Kwa hakika wale waliodhani miongoni mwa Waislamu kwamba Isa[as] atashuka toka mbinguni hawakuifuata haki, bali wanahangaika katika bonde la upotevu, hawanayo elimu yake ila wanakisia tu. Je wamepewa dalili yoyote au wamefundishwa haya ndani ya Kurani, ndiyo maana wanashikamana nayo? La, sivyo, bali wameyafuata matamanio ya waliopotea hapo kabla na wakaiacha kauli ya Mola wao wala hawaijali. Kurani imeeleza kuwa Isa[as] amekwishafariki. Basi jambo lipi wataliamini baada yake. Je hawaitafakari siri ya ujaji wa Masihi? Au nyoyo zao zimetiwa kufuli? Au hawa ni watu wasio na busara? Mwenyezi Mungu Alikuwa amewafanyia hisani wana wa Israeli kwa kumtuma Musa[as] na manabii waliokuja baada yake toka miongoni mwao. Na wakawaasi manabii wao, wakalikadhibisha kundi moja la manabii na kundi jingine wakajaribu kuwaua. Hapo Mungu Akataka kuwaondolea neema yake na kuwapa watu wengine, ili Aone hao wanatendaje. Hivyo, Akamwinua mithili ya Musa[as] kutoka miongoni mwa wana wa Ismaeli, na Akawafanya Maulamaa wa umati wake kama manabii wa silsila ya Musa[as] na kuvunjilia mbali majisifu ya Wayahudi kwa njia hii kwa sababu walikuwa wanatakabari. Na Akampa Nabii[saw] wetu yote aliyopewa Musa[as] bali na zaidi, na Akampa Kitabu na Makhalifa mfano wake na kuunguza nyoyo za waliodhulumu na kutakabari ili warejee. Na kama Yeye Alivyoumba jozi za kila namna, ndivyo Alivyofanya silsila ya Ki-Ismaeli kuwa jozi ya silsila ya

Ki-Israeli, na hii imenena Kurani, na hawaikani ila vipofu. Je huoni kauli ya Mwenyezi Mungu ndani ya Sura Al-Jaathiya:

> ‘Na kwa yakini Tuliwapa wana wa Israeli Kitabu na hukumu na unabii na Tukawapa vitu vizuri na Tukawafahili kuliko walimwengu. Na Tukawapa maelezo ya amri, basi hawakuhitilafiana ila baada ya kuwafikia elimu, kwa uasi baina yao; hakika Mola wako Atahukumu kati yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana. Kisha Tumekuweka juu ya sheria hasa katika amri, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wale wasiojua’ (45:17-19).

Basi, angalia jinsi Mwenyezi Mungu Alivyotaja silsila mbili zinazokabiliana: Silsila ya Musa[as] hadi Isa[as], na silsila ya Nabii[saw] wetu hadi Masihi Mau‘udi aliyewasili katika zama zenu hizi. Yeye hakutokana na Wakureishi kama ambavyo Isa[as] hakutokana na wana wa Israeli, naye ndiye utambuzi wa Saa (ya mpinduzi) kwa watu wote kama Isa[as] alivyokuwa utambuzi wa Saa (ya mpinduzi) ya Wayahudi. Na hii imeashiriwa ndani ya Sura Al-Faatiha. Na haya siyo maneno yaliyozushwa, bali mbingu imeshuhudia kwa ishara zake na ardhi imelonga kwamba wakati wenyewe ndio wakati huu huu. Hivyo, Mche Mwenyezi Mungu na usikate tamaa katika rehema ya Mwenyezi Mungu. Na amani iwe juu ya afuataye mwongozo.

Basi, kwa ufupi ni kwamba Kurani imejaa maelezo haya kwamba Mwenyezi Mungu Alimchagua Musa[as] baada ya kuviangamiza vizazi vya kwanza, na kumpa Torati na kuwatuma manabii mfululizo kumsaidia, kisha Akamtuma Isa[as] juu ya nyayo zao.[2] Na Akamchagua

[2] **Maelezo ya pembeni:** Jahili mmoja amenipinga atokanaye na mji uitwao jina Jahl, Enyi wenye akili, na linaishia kwenye herufi miim (m) ili iwe dalili juu ya upotefu wa moyo na mauti. Akafurahia sana kipingamizi chake na akanitukana na kunitaja kwa maneno mabaya mno. Akasema kwamba mtu huyu anadhani kuwa Isa[as] alikuwa miongoni mwa wafuasi wa Musa[as], ilhali dhana yake hii ni batili na uongo wake ni dhahiri fika. Bali Isa[as] alipewa sheria hasa ya kujitegemea, na akawaondoshea wafuasi wake sheria ya Musa[as] na akaimarisha Injili badala ya Torati. Basi tambueni kuwa kauli hii haiwezi kutoka isipokuwa kinywani mwa aliyenajisika kwa najisi ya ukosefu wa ujuzi na ujahili, na pua ya busara yake imeoza kwa ukoma wa chuki. Jahili huyu anadhani kuwa analeta dalili juu ya madai yake kutoka ndani ya Kurani ambayo ndiyo mwamuzi wakati wa ugomvi. Na akasoma kauli ya Mwenyezi Mungu: 'Na Tukampa Injili iliyomo ndani yake mwongozo na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati na mwongozo na mauidha kwa wamchao. Na watu wa Injili wahukumu kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio waasi.' [Al-Maaida, 5:47-48] yaani habari njema za ujaji wa Mbora[saw] wa viumbe. Huyo hakuelewa siri ya aya hii na akanishambulia kwa sauti iliyo mbaya kuliko sauti zote

Muhammad[saw] baada ya kuwahilikisha Wayahudi na kuwaangamiza. Na hamna shaka wala wasiwasi kwamba silsila ya Musa[as] na ya Muhammad[saw] zakabiliana, na ndivyo Alivyotaka Mwenyezi Mungu na kuamua. Ama Isa[as], basi yu miongoni mwa mahadimu

---

na akadhani kwamba amejikinga kwenye nguzo yenye nguvu. Akanitusi kama wanawake wenye mazungumzo machafu. Na akasema kuwa hii ndiyo dalili wazi ya Injili kuwa sheria ya kudumu. Namsikitikia yeye na ghaidhi yake aliyoitoa kama vijidudu vya ardhini. Na mwenye bahati mbaya zaidi miongoni mwa watu ni yule asiye na akili lakini anajihesabu kuwa kati ya wenye busara. Na hali yenyewe ni kwamba kila mtoto wa kiume na wa kike — licha ya wa Waislamu wanaume na wanawake, waliobalehe — anajua kwamba Kurani haiwaamuru Wayahudi na Manasara kuvifuata Vitabu vyao na kuimarika juu ya sheria zao, bali inawaita kwenye Islam na maamrisho yake. Mwenyezi Mungu Amesema ndani ya Kitabu chake kiheshimiwacho: "Bila shaka dini hasa mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu [Sura Aaali 'Imraan 3:20]. 'Na anayataka dini isiyokuwa ya Kiislamu, basi haitakubaliwa kwake, naye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye hasara' [Sura Aali 'Imraan 3:86]. Hivyo, yawezekanaje kudhaniwa kumhusu Mungu Kudusi kwamba katika aya hii Anawaita Wayahudi na Manasara kwenye Islam na Anasema kuwa hamtafaulu abadan wala hamtaingia Peponi isipokuwa baada ya nyinyi kuwa Waislamu, wala Torati yenu haitawafaeni wala Injili yenu isipokuwa Kurani, kisha Asahau

wa sheria ya Kiisraeli na katika manabii wa silsila ya Musa[as], na hakupewa sheria kamili ya kudumu, wala hayapatikani ndani ya Kitabu chake maelezo ya vilivyo haramu na vilivyo halali wala urithi na ndoa wala masuala mengine. Na Manasara wanakubali jambo hili,

---

kauli yake ya kwanza na kuliamuru kila kundi la Wayahudi na Manasara kuimarika juu ya sheria zao na kushikamana na Vitabu vyao, na hii itawatosha kwa wokovu wao. Hii siyo ila ni kujumuisha mambo mawili yanayopingana na ni hitilafu ndani ya Kurani, ilhali Mwenyezi Mungu Akakitakasa Kitabu chake na hitilafu kwa kauli yake: 'Na kama ingalitoka kwa aisyekuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka wangalikuta ndani yake hitilafu nyingi' [Sura An-Nisaa 4:83]. Bali, aya alizobadilisha mpinzani maana zao kama mfano wa Wayahudi zaashiria kwenye bishara kumhusu Nabii wetu[saw] kwamba zilikwepo ndani ya Torati na Injili, hivyo Mungu Anasema wamekuwaje hawatekelezi wasia wa Torati na Injili wala hawasilimu! Naam, kama ibara ya Kurani ingalikuwa ya wakati uliopita na isingalisema وَلْيَحْكُمْ — na wahukumu — bali ingalisema 'na Manasara walikuwa wakihukumu kwa Injili tu, hapo ingekuwa dalili juu ya msimamo wake. Ama maneno yaliyobakia ya aya hizo, yaani maneno yaliyomo humo ya 'nuru' na 'mwongozo', basi hayo siyo dalili juu ya Injili kuwa sheria ya kudumu. Je Zaburi na Vitabu vinginavyo vya manabii wa wana wa Israeli si mwongozo kwa watu? Je humo mna giza tu na haimo nuru. Basi zingatia, na usiwe miongoni mwa majahili. Na Manasara wameafikiana juu

ndiyo sababu twaona mikononi mwao Torati pia kama tunavyoona Injili. Na baadhi ya madhehebu yao husema kwamba kwa damu ya Yesu tumeokolewa katika mizigo ya sheria ya Torati. Na baadhi yao huyaharamisha yaliyoharamishwa na Torai na hawali nyama ya nguruwe kama vile Manasara wa Armenia, na hawa ndio wa zamani zaidi kuliko madhehebu mengine. Manasara wote wanaafikiana juu ya jambo hili kwamba Isa[as] akaleta fadhili ya Mungu na Musa[as] akaleta sheria, na wakaziita zama zao kama zama za sheria na zama za fadhili, na wakaziita zile za awali kuwa Agano la Kale na za pili Agano Jipya. Waulize, basi, ukishuku ndani yake.

Hivyo kiini cha maneno yetu ni kwamba Mwenyezi Mungu Alielekea kwa wana wa Israeli na kuanzisha silsila ya Musa[as] na kuitimiliza kwa Isa[as], naye ndiye tofali lake la mwisho. Kisha Akaelekea kwa wana wa Ismaeli na Akaanzisha silsila ya Nabii wetu Mteule[saw] na Akamfanya kuwa mithili ya Musa[as] ili Aonyeshe mkabala katika yote aliyojaaliwa na Akaihitimisha silsila hii kwa mithili ya Isa[as] ili kuitimizia silsila hii neema

---

ya hili kwamba Isa[as] bin Mariamu hakuwaletea sheria. Hapa twaandika ushahidi wa G.A. Lefroy ambaye ndiye Askofu wa Lahore, yaani kiongozi wa Makasisi wa sehemu hiyo, na hii yakutosha, kama ukihofia kuchafuliwa jina lako na kudhalilika. Na tumeona afadhali tuuandike ushahidi huu peke yake ndani ya maelezo ya pembeni. Mwandishi.

kama Alivyoitimiza juu ya silsila ya awali. Na kama silsila ya Muhammad[saw] haingekuwa na Masihi huyu wa Muhammad[saw], mgawanyo huu ungekuwa mbaya sana. Basi, tafakarini sana, na akili ndiyo kwa ajili ya kazi hii hii, Enyi wenye akili! Hakuna kilichomwokoa isipokuwa ukweli, basi na utafuteni kwa kugonga mlango wa Mungu Mtukufu na elekeeni kwenye Mungu kikamilifu kwa makusidio haya na Mwombeni usiku, na angukeni mkilia mbele ya Mungu Mwenye Enzi na nguvu, na msipite mkidhihaki na kusingizia na jikingeni kwa Mwenyezi Mungu Awalindeni na shetani.

Enyi watumishi wa Mungu, shikeni nasaha na zindukeni, kwani Masihi Mwamuzi ameishafika, hivyo tafuteni elimu ya kimbingu na msiithamini milki yenu mbele ya Mola Mtukufu. Wallahi nimefika toka kwa Mwenyezi Mungu na sikutunga uongo; ameshindwa yule aliyezusha uongo. Hakika siku za Mungu zimewadia, na ni masikitiko juu ya yule aliyekataa, na hafaulu akengeukaye hata akija toka upande wowote. Na haki — nami nasema haki — ndiyo kwamba ujaji wa Masihi toka katika umati huu ulikuwa ni jambo lililokuwa hamna budi kutekelezwa toka kwa Mungu Mtukufu kwa sababu ya ghera yake, na Alikadaria tangu azali kudhihiri kwake. Na siri ndani yake ni hii kwamba Mwenyezi Mungu Alitaka kuufanya mwisho wa dunia uwe kama mwanzo wake katika kukanusha wengine na kujisahau ndani ya utii wa Mungu Mmoja, na baada ya kuwaita watu kwenye Umoja wa kulazimishwa,

watungwe ndani ya ushanga wa Umoja wa asili. Watu walikuwa wamegawanyika katika makundi mbalimbali na rai za namna namna na matamanio tofauti na walikuwa watii wa utawala wa shetani, dajali na dhuluma. Wasingezuilika kama usingewafikia utulivu tele. Na shetani aliye chatu wa kale na dajali mkubwa asingewaachia huru katika kifungo chake. Huyu alitaka kuwameza wote na kuwafanya kuwa kuni za moto. Kwani akaangalia kwenye siku zake, na akaona siku za muhula wake zimebakia kidogo, hivyo akahofia kuwa miongoni mwa walioshindwa, kwa sababu alikuwa amepewa muhula hadi wakati huu. Hivyo akaona kuwa atahilikika kwa yakini, basi ashambulie kwa shambulio lililo mwisho wa mashambulio yake na mwisho wa harakati zake. Basi, akajumuisha yote aliyokuwa nayo, yaani njama zake na hila zake na silaha zake na zana zote za vita, na akasonga mbele kama milima iendayo na bahari zilizofurika, pamoja na majeshi yake yote ili aingie ndani ya sehemu makhsus ya Ukhalifa. Hapo ndipo Mwenyezi Mungu Alipomteremsha Masihi wake toka mbinguni pamoja na silaha ya kimbingu ili hukumu ya mwisho itolewe baina ya kufuru na imani, na Akateremsha pamoja naye ishara zake na Malaika wa mbinguni. Hivyo, leo ni siku ya vita baina ya mwitaji kwenye Mungu na mwitaji kwenye asiyekuwa Mungu, isiyosikika mithili yake katika zama za awali wala haitasikika baadaye. Leo dajali mzushi hatakiacha chochote katika hila zake ila atazitumia hizo, wala

Masihi mwenye kumwomba Mwenyezi Mungu hataacha kujibidiisha kumkaribia Mungu na kuelekea kwenye Muumbaji ila ataikamilisha. Na wote wawili watapigana vita kali sana mpaka nguvu zao na ukali wao utawastaajabisha wote waliomo mbinguni. Na milima itaikuta miguu ya Masihi kuimarika zaidi kuliko milima, na bahari zitauona moyo wa Masihi mwepesi zaidi na kutiririka zaidi kuliko maji ya bahari. Vita vikali vitaendelea mpaka miaka arobaini tangu Masihi adhihiri, ndipo dua ya Masihi itakubaliwa kwa sababu ya uchamungu wake na ukweli wake, na Malaika wa kusaidia watateremka na Mwenyezi Mungu Atamfanya chatu huyu pamoja na majeshi yake washindwe vibaya sana kwa kumfanyia mja wake hisani. Basi, nyoyo za watu zitarejea kwenye Tauhidi toka ushirikina, na kwenye huba ya Mungu pekee toka huba ya shetani, na kwenye kuzama ndani ya Mungu toka hali ya kutenganishwa Naye, na kwenye kujinyima toka tamaa za nafsi. Kwani shetani anakaribisha kwenye tamaa za nafsi na kutengana na Mungu, lakini Masihi anaita kwenye Umoja na kujipoteza ndani ya huba ya Mungu, na baina ya hawa wawili kuna uadui wa dhati tangu azali. Na Masihi atakapopata ushindi, hapo yatamalizika mapigano yote yaliyokuwa yanaendelea baina ya majeshi ya Rahmani na majeshi ya shetani, ndipo kipindi hiki cha dunia kitakwisha na zama zitakamilisha duara lake na tabia ya binadamu itarejea kwenye hali ya awali, isipokuwa wale ambao bahati yao mbaya ya tangu azali

imewazingira, hawa ndio watakaonyimika. Na kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu na hisani yake, Akaukadiria ushindi huu kwa mkono wa Masihi wa Muhammad[saw] ili Awaonyeshe watu kuwa yu mkamilifu zaidi kuliko Masihi wa Kiisraeli katika baadhi ya mambo yake. Na hii ndiyo kwa sababu ya ghera ya Mwenyezi Mungu waliyoichochea Manasara kwa kumsifu Masihi wao kupita mipaka. Na kama shani ya Masihi wa Muhammad[saw] ndiyo hii, basi kubwa ilioje shani ya yule Nabii[saw] ambaye Masihi ni katika umati wake. Ee Mungu, Umteremshie baraka na amani ambayo isiache baraka yoyote katika baraka zako na kuwadhalilisha maadui zake kwa misaada yako na ishara zako. Amin.

Mwandishi: Mirza Ghulam Ahmad
Toka Qadian, Panjab.
25 Agosti 1901

Bishops Bourno
Lahore
Aug. 15.01.

Dear Sir,

The Lord Jesus Christ was certainly not a lawgiver, in the sense in which Moses was, giving a complete descriptive law about such things as clean and unclean food etc. That he did not do this must be evident to any one who reads the New testament with any care or thought whatever. The Mosaic law of meats etc was given in order to develop in the minds of men who were in a very elementary stage of education and religion, the sense of law, and gradually of Holiness and the reverse. It is therefore called in the New testament a "Schoolmaster to bring us to Christ" (gal iii. 24) for it developed a conscience in men which, when awakened, could not find rest in any external or purely ceremonial acts but needed an inner righteousness of heart and life. And it was to bring this that Christ came, By His life and death he both deepened in men's minds the sense of what sin really is and how terrible it is and also showed men how they could be reconciled to God, obtaining forgiveness of sins and also power by the gift of the Holy Spirit to live a new life in real holiness, and in love to God and man. What the characteristics of that new life are, you can see by reading the sermon of the mount St. Mathew Chapters V-VII.

**Tafsiri**

Bishop Bourno
Lahore
15 Agosti 1901

Bwana Mheshimiwa,

Bwana, Yesu Kristo hakuwa fika mwenye kuleta sheria katika maana ambamo Hadhrat Musa alikuwa mwenye kuleta sheria, ambaye alitoa sheria kamili kwa kirefu kuhusiana na mambo kama vile nyama gani ni halali na gani ndio haramu n.k.w.k. Hata mtu akiitupia Injili macho kijuujuu tu atabainikiwa kwamba Yesu Masihi hakuwa mwenye sheria.

Sheria ya Musa kuhusu vyakula ilishuka ili moyo wa mtu ukilelewa upate ufahamu wa sheria, na hatua kwa hatua aanze kufahamu yaliyo matakatifu na yasiyo matakatifu. Kwani, wakati huo binadamu alikuwa kwenye hatua ya kwanza ya mafundiho na dini. Ndiyo maana ikasemwa ndani ya Injili kwamba sheria ya Musa ilikuwa ni mwalimu, iliyotufikisha mpaka kwa Masihi, kwani sheria hii ilizalisha moyoni mwa mtu ile tabia ambayo kwa kupata maendeleo haikutosheka na vitendo vya dhahiri na rasmi bali ikawa yenye kutafuta ukweli wa ndani mwa moyo na roho. Masihi alikuja kuleta ukweli huu. Kwa njia ya maisha yake na mauti yake akatilia nyoyoni mwa watu kwamba dhambi ni nini na ni ya kutisha namna gani, na kwa kupata msamaha wa dhambi na kwa kupata maisha ya utukufu kwa kujaaliwa na Roho Mtakatifu, na kwa kuimarisha huba baina ya Mungu na

mtu, twaweza kumridhisha Mungu. Kwa kusoma ndani ya Mathayo, mlango wa 5-7, *mawaidha ya mlimani* yaweza kujulikana sifa bainifu za maisha hayo mapya.

Saini: J. A. Lefroy, Askofu wa Lahore

## Nyongeza ya Hotuba iliyofunuliwa

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [3]

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [4]



Mfano wa Mnara wa Masihi

## TANGAZO LA MCHANGO KWA MNARA WA MASIHI

”بخرام کہ وقت تو نزدیک رسید و پائے محمدیاں بر منار بلند تر محکم افتاد“[5]

(Huu ni ufunuo ulioandikwa ndani ya Baraahine Ahmadiyya, ambayo imepita miaka ishirini tangu ichapishwa)

Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, msikiti wa Qadian aliujenga marehemu baba yangu baina ya mitaa miwili yenye maduka, penye mahali palipoinuka, ukiwa mdogo. Sasa kwa ajili ya shani ya Islam umepanuliwa sana, na sehemu nyingine pia imejengwa. Hivyo, msikiti huu sasa umekuwa na sura nyingine, yaani mwanzoni wasaa wa msikiti huu ulikuwa hivi kwamba kwa shida watu mia mbili waliweza kusali ndani yake, lakini sasa watu wapatao elfu mbili wanaweza kusali humo, na pengine baadaye pia msikiti huu utapanuliwa. Siku za mwanzo

---

[3] Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[4] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

[5] “Ufurahi, kwani wakati wako umekaribia na mguu wa wafuasi wa Muhammad[saw] umeimarika juu ya Mnara Mrefu sana.”

wa madai yangu, kwa wingi watu kumi na watano au ishirini walikuwa wanajumuika kwa sala ya Ijumaa, lakini sasa wasalio mia tatu au mia nne ni makisio ya kawaida, na wakati mwingine idadi inafikia mia saba au mia nane. Watu wanakuja toka mbali sana. Hii ni kudura ya ajabu ya Mwenyezi Mungu kwamba masheikh wa Panjab na India walitia bidii sana ili Jumuiya yetu ivunjike na kusambaratika, lakini kadri walivyoendelea kujaribu kuing'olea mbali, ndivyo maendeleo yalivyoendelea kuzidi na Jumuiya hii ikasambaa kinyume cha kawaida ndani ya nchi hii. Hili ni jambo lililo ishara moja kwa wenye macho. Kama hii ingekuwa kazi ya binadamu, ingeishafutika tangu muda mrefu kwa sababu ya juhudi za masheikh, lakini kwa kuwa kazi hii ilikuwa ya Mungu na ilikuwa Mkononi Mwake, hivyo ukinzani haukuweza kuizuia.

Sasa ili kukamilisha imeonelewa kwamba upande wa mashariki wa msikiti, kama ulivyo utashi wa Hadithi za Mtume[saw] wa Mungu, ujengwe mnara mrefu sana, na mnara huu uwe mahususi kwa kazi tatu:

Ya kwanza ndiyo hii kwamba ili mwadhini akipanda juu yake awe anatoa adhana mara tano ili Jina Tukufu la Mungu lifikishwe kwa sauti ya juu usiku na mchana mara tano, na ili kwamba kimuhtasari watu watangaziwe toka kwetu kwamba Yule Mungu wa tangu azali na wa milele Anayepaswa kuabudiwa ndiye tu Yule Mungu Ambaye kwake Mtume Mtukufu Muhammad Mteule[saw]

anaongoza; minghairi yake hakuna Mungu mwingine katika ardhi wala huko mbinguni.

Shabaha ya pili ya mnara huu itakuwa kwamba kwenye sehemu ya juu sana ya ukuta wa mnara huu iwekwe kandili kubwa sana ambayo bei yake itakuwa Rupia 100 au zaidi kidogo. Mwanga huu utafika mbali sana kwa kung'arisha macho ya watu.

Kusudio la tatu litakuwa ni kwamba kwenye sehemu moja ya juu kabisa ya mnara itatiliwa saa kubwa itakayogharimu Rupia 400 au 500, ili watu wajue wakati na binadamu waelekee kutambua thamani ya wakati.

Mambo hayo yote matatu yatakayojiri kwa njia ya mnara huu, ndani mwake mna hakika tatu zilizofichika. Mosi, adhama itakayotolewa kwa kupaza sauti, chini yake hakika hii imefichika kwamba sasa kwa kweli wakati umewadia kufikishia sauti ya ‘Hakuna apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu’ kwenye kila sikio. Yaani, sasa wakati unasema wenyewe kuwa minghari ya Yule Mungu wa toka azali hadi milele Ambaye Mtume Mtukufu[saw] ameongoza kwake miungu yote ni batili iliyozushwa. Kwa nini ni batili? Kwa sababu waiaminio hawawezi kupata baraka yoyote kwayo, wala hawawezi kuonyesha ishara yoyote.

Pili, kandili itakayowekwa ukutani mwa mnara huu, chini yake ipo hakika hii kwamba watu watambue kuwa zama za mwanga wa mbinguni zimekuja, na jinsi ardhi ilivyosonga mbele katika uvumbuzi wake ndivyo

mbingu ilivyotaka kudhihirisha nuru zake kwa uwazi zaidi sana, ili watafutao ukweli wafikiwe na siku za kuburudika, na kila jicho liwezalo kuona liuone mwanga wa kimbingu na kwa sababu ya mwanga huu kusalimika na makosa.

Tatu, ile saa kubwa itakayotiwa katika sehemu fulani ya ukuta wa mnara huu, chini yake hakika hii imefichika kwamba watu wapate kutambua wakati wao, yaani wafahamu kwamba wakati wa kufunguka milango ya mbingu umewadia. Tangu sasa jihadi za kiardhi zimefungwa na vita vimekoma kama ilivyokuwa imeandikwa ndani ya Hadithi kwamba Masihi atakapowasili itaharamishwa kupigana vita kwa ajili ya dini. Hivyo, tangu leo kupigana kwa ajili ya dini imeharamishwa. Sasa anayeinua upanga na akiitwa *Ghazi* — mshindi — anawaua makafiri, yeye mtu huyo anamwasi Mungu na Mtume wake[saw]. Funueni Sahih Bukhari mkasome ndani yake Hadithi ile imhusuyo Masihi, yaani *yadha'ul Harb,* inayomaanisha kwamba atakapokuja Masihi, vita za kijihadi zitamalizika. Basi Masihi ameishafika, naye ndiye anayeongea nanyi.

Kwa ufupi, ile iliyosimuliwa ndani ya Hadithi ya Mtume[saw] kuhusiana na Masihi Mau'udi kwamba atateremka karibu na mnara mweupe, ilimaanisha kwamba alama ya wakati wa ujaji wa Masihi Mau'udi ni hii kwamba wakati huo kwa sababu ya kuchanganyikana kwa watu wa sehemu mbali mbali za dunia na

kufunguliwa njia nyingi na kuwasiliana kwa urahisi, kazi ya kufikisha maamrisho na mwanga wa dini na kutangaza itakuwa rahisi sana kana kwamba mtu huyo amesimama juu ya mnara. Hii iliashiria kwenye garimoshi, vyombo viendeshwavyo kwa mvuke na nidhamu ya posta, ambavyo viliifanya dunia nzima kama mji mmoja. Ilmuradi, kwa ajili ya zama za Masihi kuna ishara ndani ya neno mnara kwamba mwanga wake na satui yake itaenea duniani haraka sana. Mambo haya hayakupatikana kwa Nabii yeyote. Na imeandikwa katika Injili kuwa ujaji wa Masihi utakuwa jinsi umeme ukimemeta upande mmoja mbinguni unavyong'arisha mara moja pande zote, hii iliashiria kwenye jambo hili hili. Ndiyo sababu kwamba kwa kuwa Masihi amekuja kuifikishia mwanga dunia nzima, hivyo akaandaliwa mapema mambo haya yote. Hakuja kumwaga damu, bali ameleta ujumbe wa suluhu kwa dunia nzima. Kwa nini, basi, zimwagwe sasa damu za wanadamu? Kama yupo atafutaye ukweli, basi na aone ishara za Mungu ambazo kwa mamia zilidhihirika na zaendelea kudhihiri. Kama kuna mtu asiyemtafuta Mungu, mwacheni tu, msimfikirie kumwua, kwani nawaambia kweli kabisa kwamba ile siku ya mwisho ipo karibu ambayo Manabii wote waliendelea kutisha kwayo dunia.

Ilmuradi, saa ile itakayowekwa kujua wakati, ndiyo kwa kukumbusha wakati wa Masihi kuwadia. Na ndani mwa mnara huu wenyewe mna hakika moja iliyofichika, nayo ndiyo hii kwamba ndani ya Hadithi za Mtume[saw]

imeelezwa mara kwa mara kwamba Masihi anayetazamiwa kuja atakuwa mwenye mnara, yaani katika zama zake ukweli wa Islam utafikia upeo wake ulio kama mnara mrefu sana, na dini ya Kiislamu itazishinda dini zote jinsi ambavyo mtu anapotoa adhana juu ya mnara mrefu, basi sauti yake inazishinda sauti zote nyingine. Basi, ilikadiriwa kwamba itakuwa hivyo katika siku za Masihi, kama Asemavyo Mwenyezi Mungu: "Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote."[6] Aya hii inahusikana na Masihi Mau'udi. Na sauti ile ya juu kabisa ya hoja ya Kiislamu ambayo mbele yake sauti nyingine zote zitafifia, ilikuwa imewekwa mahususi tangu azali kwa ajili ya Masihi, na tangu kale ilikatwa shauri kuhusu mguu wa Masihi Mau'udi kuwa juu ya mnara mrefu ambao hakuna jengo lililo refu kuliko huo. Kwenye hii hii imeashiriwa ndani ya ufunuo huu ulioandikwa katika ukurasa 522 wa Baraahine Ahmadiyya, nao ndio huu: 'Ufurahi, kwani wakati wako umekaribia, na mguu wa wafuasi wa Muhammad[saw] umeimarika juu ya mnara mrefu sana.' Kadhalika, msikiti wa Masihi Mau'udi pia ni Masjid Aksa — Msikiti wa Mbali — kwani upo mbali sana toka zama za mwanzo wa Islam, na ndani ya riwaya moja Nabii Mtukufu[saw] wa Mungu alitabiri kwamba Masihi atashuka

[6] Sura As-Saff, 61:10

karibu na mnara wa mashariki wa Masjid Aksa.[7] Sasa, Enyi marafiki, mnara huu unatayarishwa ili sawa na Hadithi uwe ni kumbukumbu ya zama za Masihi Mau'udi na pia utimie ule utabiri uliotajwa ndani ya aya hii ya Kurani Tukufu: 'Utukufu ni wa Yeye Ambaye Alimpeleka

---

[7] Ipo katika baadhi ya Hadithi kwamba kuna mnara fulani upande wa mashariki wa Dimashki — Damascus — ambao karibu yake Masihi atashuka. Hadithi hii haiko kinyume cha muradi wetu, kwani tumeishaeleza mara nyingi kuwa kijiji chetu hiki kinachoitwa Qadian, na msikiti wetu huu ambao karibu yake mnara utajengwa ni upande wa mashariki toka Dimashki. Hadithi haielezi kwamba mnara huo utaungana na Dimashki na utakuwa sehemu yake, bali utakuwa upande wake wa mashariki. Kisha ndani ya Hadithi nyingine kuna maelezo kwamba karibu na Masjid Aksa atashuka Masihi. Hii yathibitisha kuwa mnara ule ndio mnara wa Masjid Aksa hii hii, na Dimashki imetajwa kwa sababu ile tuliyoishaeleza sasa hivi. Hapo Masjid Aksa haimaanisha msikiti wa Jerusalem, bali ni msikiti wa Masihi Mau'udi ambao kwa sababu ya umbali wa zama ni Masjid Aksa mbele ya Mwenyezi Mungu. Nani anaweza kukataa ya kuwa ule msikiti anaofanya Masihi Mau'udi kuwa msingi unastahili kuitwa Masjid Aksa yaani msikiti wa Mbali. Kwani, ikiwa dhati ya Masihi Mau'udi kwa ajili ya Islam ni ukuta wa mwisho naye atashuka katika zama za mwisho na ndani ya sehemu ya mbali sana ya dunia pamoja na baraka za kimbingu, kwa hiyo kila Mwislamu hana budi kuamini kwamba msikiti wa Masihi Mau'udi

Mtumishi Wake usiku kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ambao mnara wake umetajwa ndani ya Hadithi pia kwamba Masihi atashuka karibu na mnara. Dimashki — Damascus — imetajwa katika

---

ndio Masjid Aksa. Kwani kwenye nukta ya mwisho ya mstari mrefu wa zama za Kiislamu kuna dhati ya Masihi Mau'udi, hivyo msikiti wa Masihi Mau'udi u mbali sana mno toka zama za kwanza zilizo mwanzo wa Islam, basi kwa sababu hii hustahili kuitwa Masjid Aksa — Msikiti wa Mbali — na mnara wa msikiti huu, unastahili kuwa mrefu zaidi kuliko minara yote, kwani mnara huu ni taswira ya kidhahiri ya Masihi Mau'udi kuhakikisha haki na kujibidiisha kwake na kuishindisha dini. Basi, kama ambavyo ukweli wa Kiislamu umeishafika kwenye daraja ya juu kabisa mkononi mwa Masihi Mau'udi, na juhudi ya Masihi inaendelea kurudisha toka thurea imani iliyokuwa imepotea, ndivyo kulandana na hali hii mnara huu unavyodhihirisha adhama ya mambo ya Kiroho. Ile sauti itakayofikishwa kwenye kona nne za dunia inahitaji mnara ulio mrefu mno. Karibu miaka ishirini imepita niliandika ndani ya kitabu change Baraahine Ahmadiyya maneno haya ya Mwenyezi Mungu niliyotamkishwa ulimini mwangu, yaani maneno haya:

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ قَرِيبًا مِنَ الْقَادِيَانِ۔ وَبِالْحَقِّ أَنْزَلْنَاهُ وَبِالْحَقِّ نَزَلَ۔ صَدَقَ اللّٰهُ وَرَسُولُه۔
وَكَانَ أَمْرُ اللّٰهِ مَفْعُولًا

Tazameni Baraahine Ahmadiyya, uk 498. Yaani, Tumemteremsha

Hadithi ya Muslim kwa sababu chanzo cha itikadi ya Utatu — miungu watatu — ni Dimashki, na ushukaji wa Masihi Mau'udi ni kwa lengo la kufutilia mbali fikara za 'watatu' na kuimarisha duniani jalali ya Mungu Mmoja. Hivyo ili kuashiria kwenye habari hii ikasemwa

---

Masihi Mau'udi huyu katika Qadian; ameteremshwa kwa haja ya kweli. Aliyonena Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani na Mtume[saw] ndani ya Hadithi yametimia kwa ujaji wake. Wakati wa ufunuo huu, kama nilivyoandika mara nyingi, nikajua kwa njia ya kashfi kwamba ufunuo huu umeandikwa ndani ya Kurani Tukufu. Na wakati huo katika hali ya kashfi moyoni mwangu mlikuwa na yakini kwamba katika Kurani Tukufu miji mitatu imetajwa, yaani Makka, Madina na Qadian. Sasa miaka karibu ishirini imepita tangu nilipoandika ndani ya Baraahine Ahmadiyya. Sasa wakati wa kuandika kitabu hiki ikafunuliwa kwangu kwamba niliyoandika ndani ya Baraahine Ahmadiyya kuhusiana na Qadian kwa njia ya kashfi, yaani hii imetajwa ndani ya Kurani Tukufu, kwa hakika jambo hili ni sahihi, kwani ni hakika kabisa kwamba aya hii ya Kurani Tukufu: "Utukufu ni wa Yeye Ambaye Alimpeleka Mtumishi Wake usiku kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali ambao Tumevibariki vilivyoko Pembezoni mwake' inajumuisha Miraji zote mbili, za kimakani na kizamani, na bila hii Miraji haikamiliki. Hivyo, kama Mwenyezi Mungu Alivyompeleka Mtume[saw] kutoka msikiti mtukufu mpaka Baitil Mukaddas katika safari ya kimakani ndivyo katika safari ya kizamani Alivyompeleka Mtume[saw] kutoka zama za adhama ya

kuwa mnara wa Masihi ambao karibu yake yeye atashuka, upo upande wa mashariki toka Dimashki. Na hii ndiyo sahihi pia, kwani Qadian iliyo katika Wilaya ya Gurdaspur, Panjab, ambayo ipo upande wa kusini-magharibi toka Lahore, ndiyo kabisa upande wa

---

Kiislamu, zilizokuwa zama za Mtume[saw], mpaka zama za baraka za Kiislamu zilizo zama za Masihi Mau'udi.★ Basi, kwa jiha hii safari, katika kashfi, ya Mtume[saw] iendayo mpaka zama za mwisho za Islam, Masjid Aksa humaanisha Msikiti wa Masihi Mau'udi uliopo ndani ya Qadian, ambao kuhusiana nao yamo katika Baraahine Ahmadiyya maneno haya ya Mungu: مُبَارِكٌ وَ مُبَارَكٌ وَ كُلُّ اَمْرٍ مُبَارَكٌ يُجْعَلُ فِيْهِ . Na neno hili مبارك lililo kauli ya kutendwa na kauli tendi laafikiana na aya ya Kurani Tukufu — بَارَكْنَا حَوْلَهٗ — Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake. Basi, hamna shaka kuwa habari ya Qadian imo ndani ya Kurani Tukufu kama Asemavyo Mwenyezi Mungu: سُبْحٰنَ الَّذِيْٓ اَسْرٰى بِعَبْدِهٖ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اِلَى الْمَسْجِدِ الْاَقْصَا الَّذِيْ بٰرَكْنَا حَوْلَهٗ. Maana moja ya aya hii ndiyo ile ile ijulikanayo baina ya maulamma, yaani haya ni maelezo ya Miraji ya kimakani ya

---

★ Zama za adhama za Islam zilikuwa zama za uwepo wa Mtume[saw]. Athari yake kubwa ilikuwa hii kwamba waaminio waliokolewa kama Musa katika mashambulio ya makafiri, kwa hiyo Baitullah ikapewa jina Baiti Aamin. Lakini zama za baraka zilizo zama za Masihi Mau'udi, athari yake ndiyo hii kwamba raha za aina zote zipatikane duniani, na si tu amani iwepo, bali na maisha maridhawa pia. Mwandishi.

mashariki toka Dimashki. Hivyo, imethibitika kwamba huu Mnaratul Masihi pia upo upande wa mashariki wa Dimashki. Kila mtafutaji wa haki anapaswa kufikiria sana juu ya neno Dimashki kwamba kuna hekima gani ndani yake kuandika kuwa Masihi Mau'udi atashuka

---

Mtume[saw], lakini hakuna shaka kwamba mbali na hii kulikuwa na Miraji moja ya kizamani pia ya Mtume[saw], ambayo shabaha yake ilikuwa ili ukamilifu wa mtazamo wake wa kashfi udhihiri na pia ithibitike kwamba baraka za zama za Masihi pia kwa hakika ni baraka zake[saw]zilizozalika kwa nadhari na hima yake[saw]. Kwa sababu hii hii Masihi kwa namna fulani ni sura ya huyo huyo[saw]. Na Miraji ile ilikuwa kufikia hadi mwisho wa dunia kwa jicho la kashfi, inayohusikana na zama za Masihi. Na katika Miraji hii Mtume[saw] aliposafiri kutoka Msikiti Mtakatifu mpaka Msikiti Aksa, huu Msikiti Aksa ndio ule ule uliopo Qadian upande wa mashariki, ambao Mungu katika kauli yake Ameupa jina Mubarak. Msikiti huu umejengwa kidhahiri kwa amri ya Masihi Mau'udi na ni taswira kwa njia ya kiroho ya baraka na sifa kamilifu za Masihi Mau'udi ambazo ni hiba kutoka kwa Mtume[saw] na jinsi ruhania ya Msikiti Mtakatifu ni sifa kamilifu za Hadhrat Adamu[as] na Hadhrat Ibrahimu[as], na ruhania ya Baitul-Mukaddas ni sifa kamilifu za Manabii wa Wana wa Israeli, ndivyo ulivyo msikiti huu Aksa wa Masihi Mau'udi — uliotajwa ndani ya Kurani Tukufu — taswira ya sifa kamilifu za ruhania za Masihi Mau'udi.

Hivyo, imebainika kutokana na utafiti huu kwamba ndani ya Miraji ya Mtume[saw] kuna kupaa kwenye zama zilizopita

upande wa Mashariki toka Dimashki, kwani mambo yasemwayo na Mwenyezi Mungu hayawi ya bahati, bali chini yake huwa siri na ishara, kwa sababu mambo yote ya Mwenyezi Mungu hujaa ishara na siri.

---

na kuteremka kwenye zama zijazo. Kiini cha Miraji ni kwamba Mtume[saw] ni Mbora miongoni mwa wa awali na wa mwisho. Miraji kuanzia toka Msikiti Mtukufu inaashiri kwamba sifa kamilifu zote za Safiyyullah Adam[as] na za Khalilullah Ibrahimu[as] zlikuwemo ndani ya Mtume[saw]. Tena toka hapo mguu wake kwa safari ya kimakani ukaenda upande wa Baitul Mukaddas, na ndani yake iliashiriwa kuwa Mtume[saw] alikuwa na sifa zote kamilifu za Manabii wa Kiisraeli ndani mwake. Kisha toka hapo mguu wa Mtume[saw] kwa safari ya kizamni ukaenda hadi Msikiti Aksa, ulio msikiti wa Masihi Mau'udi, yaani mtazamo wake wa kashfi ulifika mpaka zama za mwisho ziitwazo zama za Masihi Mau'udi. Hii yaashiira kwamba aliyojaaliwa Masihi Mau'udi yote haya yamo ndani mwa dhati ya Mtume[saw]. Kisha mguu wa Mtume[saw], akiendelea kusafiri, ukapaa juu na kupata daraja ya قَابَ قَوْسَيْنِ — akawa umbali wa pinde mbili. Hii iliashiria kwenye jambo hili kwamba Mtume[saw] alikuwa dhihirisho la sifa za Mungu kitimilifu kikamilifu. Ilmuradi aina hii ya Miraji ya Mtume[saw], yaani kutoka msikti Mtukufu mpaka Msikiti Aksa, ambayo ilikuwa ni safari ya namna zote mbili, ya kizamani na ya kimakani. Na safari moja ilikuwa kwenye Mwenyezi Mungu iliyoepukana na makani na zama. Kusudio la Miraji hii ya aina mpya lilikuwa ni kwamba Mtume[saw] ni Mbora wa watu wa awali na wa mwisho na kwamba

Sasa, wapinzani wetu ingawaje wanasoma Hadithi ya Dimashki mara kwa mara lakini hawawezi kujibu kwamba kuna siri gani ndani ya habari hizi za Hadithi kwamba Masihi Mau'udi atashuka upande wa mashariki toka Dimashki karibu na mnara, bali wameichukulia

---

safari yake kwenye Mwenyezi Mungu ni mpaka nukta ya juu kabisa na kwenda zaidi yake binadamu hana nafasi. Lakini kuandika maelezo haya ya pembeni kuna shabaha hii kwamba kama ilivyoandikwa miaka ishirini mapema ndani ya Baraahine Ahmadiyya kwamba habari za Qadian zimo katika Kurani Tukufu, kashfi hii likuwa sahihi na sawa fika. Kwani, Miraji ya kizamani ya Mtume[saw] na safari yake kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti Aksa haiwezi kuwa sawa mpaka ikubaliwe safari yake hadi msikiti fulani ambao kwa sababu ya umbali wa zama uwe Msikiti Aksa — Msikiti wa Mbali. Na ni dhahiri kwamba zama za Masihi Mau'udi ni zama ambazo kulinganishwa na zama za Mtume[saw] ni ng'ambo ya pili ya bahari ya Kiislamu. Mwanzo wa safari ulielezwa kutoka Msikiti Mtukufu, na mwisho wa safari uliwekwa mpaka Msikiti wa Mbali ambao vimebarikiwa vilivyoko pembezoni mwake. Kubarikiwa huku kunaashiria kwamba katika zama za Mtume[saw] shani ya Islam ilidhihirishwa na ikaharamishwa kwamba dhuluma ya makafiri iifutilie mbali Islam, kama ilivyo dhahiri katika aya مَنۡ دَخَلَهٗ كَانَ اٰمِنًا — atakayeiingia atakuwa salama. Lakini katika zama za Masihi Mau'udi, ambaye jina lake la pili ni Mahdi pia, baraka za Islam zitathibitishwa na itaonyeshwa kuwa Islam pekee ndiyo dini yenye baraka. Kama ilivyokwisha elezwa,

Hadithi hii kama kisa tu. Lakini kumbukeni kwamba sio kisa hiki. Mambo ya Mwenyezi Mungu yameepukana na upuuzi, bali ndani ya maneo ya Hadithi hii kwanza Dimashki imetajwa kisha ikasemwa kuna mnara mmoja upande wake wa mashariki, ndani mwake mna siri, nayo

---

zama zile zitakuwa zenye baraka, suluhu itaenea duniani, mbingu itaonyesha baraka zake kwa ishara nyingi, na ndani ya ardhi, kwa sababu ya kupatikana matunda ya namna namna na raha za aina aina, baraka zitatapakaa sana ambazo kiasi hiki hazitakuwa zimeenea hapo kabla. Ndiyo sababu zama za Masihi Mau'udi na Mahdi aliyeahidiwa zimeitwa ndani ya Hadithi zama za baraka. Kama mnavyoona, uvumbuzi wa maelfu ya vitu vipya umeeneza duniani baraka na raha za namna gani, kwani kupitia garimoshi matunda ya mashariki na magharibi yanaweza kujumuika mahali pamoja, na kwa njia ya telegramu habari za maelfu ya maili zinawasili, taabu za safari zimekoma mara moja zilizokuwa katika zama zilizopita.

Almuradi, jina la zama hizi tulizomo humu ni zama za baraka, lakini zama za Nabii[saw] wetu zilikuwa zama za misaada na kuondoa maafa, na katika zama hizo makusudio makubwa ya Mwenyezi Mungu yalikuwa kufutilia mbali shari. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akaikinga Islam na maadui katika zama hizo kwa Mkono Wake wenye nguvu na kuwafukuzilia mbali maadui kama mwanamume mwenye nguvu anawafuza mbwa kwa fimbo.

Hivyo, kwa kuwa zama za Masihi na Mahdi Mau'udi zilikuwa ni zama za baraka, basi Mwenyezi Mungu Akasema kuhusiana naye

ndiyo ile ile tuliyoisha eleza sasa hivi, yaani msingi wa Utatu na miungu watatu uliwekwa humo Dimashki. Yenye nuhusi sana ilioje siku alipoingia Myahudi Paulo ndani ya Dimashki akizusha ndoto moja na kuwaambia Wakristo majuha kwamba Bwana Yesu alinidhihirikia na

---

'Tumebariki vilivyoko pembezoni mwake,' yaani pembezoni mwa makazi ya Masihi Mau'udi kokote mtakapotupa jicho, baraka zitaonekana kila mahali. Hivyo, twaona kwamba ardhi imekaliwa sana na watu, bustani zimekithiri, mifereji imekuwa mingi, vitu vya raha kwa raia vimekuwa vingi namna gani, ndivyo hivyo ulivyokuwa ukitiririka mto wa misaada ya Mungu ndani ya zama za Mtume[saw].

Basi, kiini cha maneno hayo ni kwamba zama ni za aina mbili: zama za misaada na kuondoa maafa na zama za baraka na vitu vizuri, na kwenye hii hii ameashiria Mwenyezi Mungu katika kauli yake: 'Utukufu ni wa Yeye Ambaye Alimpeleka Mtumishi Wake usiku kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake.' [Sura Banii Israaiil, 17:2] Ujue kwamba neno 'Msikiti Mtukufu' katika kauli ya Mwenyezi Mungu huashiria kwenye zama ilimodhihiri heshima ya vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu kwa msaada wa Mungu na ikadhihiri heshima ya mipaka yake na maamrisho yake na faradhi zake na ikaonekana shani ya dini yake na haiba ya dini yake. Na hizo ndizo zama za Nabii[saw] wetu. Na Msikiti Mtukufu ndio nyumba aliyoijenga Ibrahim[as] ndani ya Makka nayo ipo mpaka wakati huu, Mwenyezi Mungu akaihifadhi na kila afa. Ama kauli ya Mwenyezi Mungu iliyo baada ya kauli hii, yaani 'Msikiti wa

kuniambia nieneze mafundisho haya, kana kwamba yeye pia ni Mungu. Hivyo, ndoto hii hii ilipanda mbegu ya Utatu. Kwa kifupi, shamba hili la ushirikina mkubwa kwanza lilikua na kustawi ndani ya Dimashki, kisha sumu hii ikaendelea kuenea sehemu

---

Mbali ambao Tumebariki vilivyoko pembezoni mwake,' hii yaashiria kwenye zama ambamo zitadhihirika baraka duniani kwa kila jiha kama tulivyoeleza hapo kabla, nazo ndizo zama za Masihi Mau'udi na Mahdi aliyekuwa ameahidiwa. Na Msikiti wa Mbali ndio alioujenga Masihi Mau'udi ndani ya Qadian uliopewa jina Aksa kwa sababu ya umbali wake kutoka zama za Unabii na kwa sababu upo upande wa mbali toka mwanzo wa Islam. Basi zingatia sehemu hii, kwani hii imewekewa siri nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Ajuaye sana.

Kwa kifupi ni kwamba Miraji ya Mtume[saw] ni ya aina tatu: safari ya kimakani, safari ya kizamani na safari isiyo ya kimakani wala ya kizamani. Ndani ya safari ya kimakani mna ishara kwenye utawala na ushindi, yaani kuna ishara kuwa utawala wa Kiislamu utaenea kutoka Makka mpaka Baitul Mukaddas. Na ndani ya safari ya kizamnai mna ishara kwenye mafundisho na athari, yaani zama za Masihi Mau'udi pia zitakuwa zimepata ulezi kutoka kwa athari za Mtume[saw], kama Asemavyo ndani ya Kurani Tukufu: 'Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao.' [Sura Al-Jumu'a, 62:4] Na safari isiyokuwa ya kimakani wala kizamani huashiria kwenye daraja ya juu kabisa ya kukaribiana na Mwenyezi Mungu na kumsogelea Yeye, ambapo duara laishia la ukaribu uwezekanao. Basi, fahamu. Mwandishi

nyingine mbalimbali. Hivyo, kwa kuwa Mwenyezi Mungu alijua kwamba jiwe la msingi la kumfanya mtu kuwa Mungu liliwekwa awali ndani ya Dimashki, kwa hiyo Mwenyezi Mungu wakati wa kuzitaja zama ambapo ghera ya Mungu itafutilia mbali mafundisho haya batili, Akaitaja tena Dimashki na Akasema kwamba Mnara wa Masihi, yaani chanzo cha kudhihiri nuru, upo upande wa mashariki wa Dimashki. Ibara hii haikumaanisha kwamba mnara huo ni sehemu ya Dimashki na kwamba upo ndani ya Dimashki kama ilivyofikiriwa kwa bahati mbaya. Bali muradi wake ulikuwa kwamba nuru, ya Masihi Mau‘udi ikitokeza kama nuru ya juu kutoka upande wa mashariki wa Dimashki itatowesha kiza cha magharibi. Hii ilikuwa ni ishara nyepesi, kwani mnara wa Masihi ambao karibu yake yeye atashuka, umesemwa kuwa upande wa mashariki wa Dimashki, na Utatu wa ki-Dimashki umewekwa upande wake wa magharibi, na kwa nia hii imebashiriwa kwamba atakapowasili Masihi atadhihiri kama jua linalotokeza toka mashariki na kinyume chake taa ya Utatu iliyodhoofika iliyopo upande wa magharibi itaendelea kufifia siku hadi siku. Kwani, ndani ya vitabu vya Mungu kutokeza upande wa mashariki ni alama ya kupokelewa na kwenda upande wa magharibu ni alama ya kuharibika. Kwa kuashiria kwenye alama hii hii Mwenyezi Mungu akaifanya Qadian iliyo mahali pa kushukia kwa Masihi Mau‘udi, iwe upande wa mashariki toka Dimashki, na kuiweka Dimashki upande wake wa magharibi. Wapinzani wetu

wamepotoka hivi kwamba wakiona ndani ya maneno ya Hadithi kwamba Masihi Mau'udi atashuka karibu na mnara ule uliopo upande wa mashariki wa Dimashki wakafahamu kwamba mnara huo umo ndani ya Dimashki, ilhali hamna mnara kama huo huko Dimashki. Hawakufikiria kwamba kama isemwe kuwa sehemu fulani ni upande wa mashariki wa mji fulani, je huwa inamanisha siku zote kwamba mahali hapo pameungana na mji huo? Na hata kama kungekuwa na maneno ya aina hii ndani ya Hadithi ambayo kwa hayo ingefahamika kwamba mnara huo umeungana na Dimashki na kungekuwa hamna uwezekano wa kuchukua maana nyingine, hata hivyo kwa kulingana na ushahidi mwingine haingeweza kukubalika. Lakini sasa kwa sababu ya kuzingatia Hadithi yafahamika wazi sana kwamba muradi wa Hadithi hii ni huu tu kwamba mnara huo ni upande wa mashariki wa Dimashki, sio kwa hakika sehemu ya mji huo, hapo sio uaminifu na busara kwamba kwa kutojali hekima na siri za Mwenyezi Mungu tulizoeleza ndani ya tangazo hili, tukazanie bila sababu kwamba mnara ule ambao Masihi atashuka karibu yake umo ndani ya Dimashki. Bali, Mtume[saw] wa Mungu ameuchukua mnara huo kuwa mnara wa Msikiti Aksa uliopo upande wa mashariki toka Dimashki, yaani msikiti wa Masihi Mau'udi uliopanuliwa wakati huu na jengo limezidishwa, na msikiti huu kwa hakika upo upande wa mashariki wa Dimashki. Na Msikiti huu umepanuliwa na umejengwa

ili uurekebishe uharibifu wa Ki-dimashki. Na mnara huu ndio ule mnara ambao haja yake imekubaliwa ndani ya Hadithi za Mtume[saw] na Mnaratul Masihi huu utagharimu si chini ya Rupia elfu kumi. Sasa wale marafiki watakaosaidia katika ujenzi wa mnara huu, nafahamu kwa yakini kwamba watatoa huduma kubwa. Najua kwa yakini kuwa kutoa wakati huu haitasababisha hasara kwao. Wakamkatia Mwenyezi Mungu sehemu ya mali yao na watarudishiwa pamoja na uzidishio. Laiti nyonyo zao zingefahamu kwamba kazi hii ina adhama kubwa namna gani mbele ya Mungu. Yule Mungu aliyeamrisha kujenga mnara ameisha ashiria kwamba Islam iliyo katika hali ya kufa itapuliziwa roho ya uhai katika sehemu hii hii, na hii itakuwa ni medani ya ushindi dhahiri; lakini ushindi huu hautakuwa kwa silaha ziundwazo na binadamu, bali kwa silaha ya kimbingu, silaha wanayotumia Malaika.

**Kuanzia leo, jihadi ya kibinadamu ifanywayo kwa upanga imefungwa kwa amri ya Mungu. Tangu sasa yule mtu anayeinua upanga na kujiita Ghazi — mpiganaji mshindi — anamwasi yule Mtume[saw] aliyekwisha sema tangu miaka 1300 kwamba kwa ujaji wa Masihi Mau'udi jihadi zote za upanga zitakwisha. Basi, sasa baada ya mimi kudhihiri hakuna jihadi yoyote ya upanga. Toka kwetu bendera nyeupe ya suluhu imeinuliwa juu. Siyo njia moja tu ya kuwaita kwenye Mwenyezi Mungu.** Hivyo, njia iliyoishapingwa na majahili, hekima ya

Mwenyezi Mungu na masilahi hayataki kuishikilia ile ile njia mara nyingine. Mfano wake ni kama huu kwamba ishara zilizokwisha kadhibishwa zamani hakupewa Seyidi Rasulullah[saw] hizo. Hivyo, Masihi Mau'udi analiamrisha jeshi lake kurudi nyuma toka mahali palipokataliwa. Yule anayeshindana na ubaya kwa ubaya hayuko pamoja nasi. Jikingeni na mashambulio ya mwenye shari, lakini msishindane kishari. Yule anayempa mtu mwingine dawa chungu ili apone, huyo anamtendea wema, kuhusiana naye hatusemi kwamba ameshindana na ubaya kwa ubaya. Kila wema na ubaya huzalika kwa kulingana na nia. Hivyo, yapasa nia yenu isiwe mbaya katu ili muwe kama Malaika.

Tangazo hili limeandikwa kwa kutengeneza mnara, lakini ikumbukwe kwamba baadhi ya sehemu za jengo la msikiti haziko katika hali nzuri, hivyo imeamuliwa kwamba fedha zitakazosalia baada matumizi ya Manaratul Masih, hizo zitatumika kwa jengo la pili la msikiti. Kazi hii ni ya haraka sana. Zikunjueni nyoyo zenu na kumridhisha Mungu. Rupia hizi zitawarudieni pamoja na baraka nyingi. Sitaki kusema zaidi ya haya na ninamaliza na kumwachia Mungu haya yote.

Mwishowe nawaelekeza marafiki zangu kwenye jambo moja la muhimu sana kwamba shabaha yetu ni kuwa ndani ya mnara huu, au popote ipasavyo, kijengwa chumba kimoja cha duara au cha sura nyingine ambamo kwa akali watu mia waweza kukaa. Chumba hiki

kitatumika kwa ajili ya kutoa mawaidha na hotuba za kidini, kwani nia yetu ni kwamba ndani ya kila mwaka mara moja au mara mbili mkutano uwe unafanywa katika Qadian ili kutoka hotuba za kidini. Katika mkutano huu kila mtu kutokana na Waislamu, Mabaniani, Waaria, Wakristo na Masingasinga ataeleza mambo mazuri ya dini yake sharti asiishambulie dini nyingine kwa njia yoyote, bali asema apendavyo kwa kuisaidia dini yake kwa adabu njema. Hivyo, inaandikwa kwamba marafiki zetu wamwonyesha tangazo hili kila fundi mwashi, na kama yeyote aweze kutayarisha ramani ya mnara huu, ambayo iweze kutimiza shabaha zote mbili, basi na atuarifu.

Wassalam

Mimi Mirza Ghulam Ahmad Kutoka Qadian
28 Mei 1900
Imepigwa chapa ndani
ya Matbaa ya Dhiyaul Islam Qadian.

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [8]

نَحْمُدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ [9]

Enyi waja wa Mungu, zingatieni siku yenu hii iliyo siku ya dhabihu, kwani ndani yake mmefichika siri nyingi kwa wenye busara. Nanyi mwatambua kwamba katika siku hii wanyama wengi wanachinjwa, makundi kwa makundi ya ngamia, ng'ombe na mbuzi hudhabihiwa kupata radhi ya Mola wa ulimwengu, na ndivyo ifanyavyo tangu mwanzo wa zama za Islam hadi siku hizi. Nami nadhani kwamba dhabihu hizi katika sheria yetu ng'avu hazihesabiki, na zinazishinda zile dhabihu za nyimati za hapo kabla. Wingi wa dhabihu umefikia hadi kwamba uso wa ardhi umefunikwa na damu, hata kwamba kama damu zao zote zingekusanywa pamoja na kutaka kuzitiririsha, kwa yakini mifereji ingeanza kupita kwa hizo, na mito kutiririka, na maeneo yaliyo katika nyanda za chini na mabonde makubwa yangefurika na damu. Na kitendo hiki chahesabiwa katika dini yetu katika yale mambo yanayomsogeza mtu karibu na Mwenyezi Mungu. Na kitendo hiki kimechukuliwa

[8] Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[9] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

kama ni rikabu afananaye na umeme katika mwendo na mng'ao. Kwa hiyo, dhabihu zimeitwa *kurbani*, kwani imesimuliwa katika Hadithi kuwa hizi dhabihu zinasababisha mtu kumkurubia Mungu na kumlaki, ambaye ametoa dhabihu kwa ikhlasi na moyo wa ibada na uaminifu. Na hizi ni miongoni mwa ibada kubwa za sheria, kwa hiyo zinaitwa *nasika*. Na *Nusuk* kwa lugha ya Kiarabu yamaanisha utii na ibada. Kadhalika neno *Nusuk* latumika pia kwa kuchinja wale wanyama wanaochinjwa kisheria. Basi ushirikiano huu unaopatikana katika maana za *Nusuk* ndio dalili thabiti ya jambo hili kwamba mwenye ibada ya kweli ndiye yule mtu ambaye kwa kutafuta radhi ya Mola wa viumbe akachinja nafsi yake pamwe na nguvu zake zote na wapendwa wake ambao moyo wake ulikuwa umevutika kwao; na akatupilia mbali tamaa zake za nafsi hata kwamba matamanio yake yote yakaporomoka na kupondeka tikitiki na kufutika, na yeye mwenyewe akayeyuka na kupotea na kufichika. Na upepo mkali wa utilifu ukavuma juu yake, na chembe zake ikazirusha hewani dhoruba hii kali. Na yule aliyetafakari katika maana hizi mbili zinazoshirikiana ndani ya neno *Nusuk* na kuzingatia sehemu hii kwa busara na kwa kufumbua macho, basi hakutabaki kwake maficho wala ugomvi. Ndani mwake mna dokezo kwamba ile ibada inayookoa katika hasara ya Akhera ndiyo kuichinja nafsi *Ammara*, inayokuwa na jazba sana mno ya maovu na kuamrisha wakati wote kutenda mabaya,

na kuichinja kwa visu vitenganishavyo na mahuluku kwa kuelekeza kwa Mungu, kwa kuvumilia uchungu wa namna namna, ili nafsi ipate kuokoka na mauti ya usahaulifu. Na hii hii ndiyo maana ya Islam, na hakika ya utii kamili. Na Mwislamu ni yule aliyekwishaweka uso wake mbele ya Mungu wa walimwenu wote, ili kuchinjwa, na amekwisha kudhahi ngamia jike wa nafsi yake, na kujilaza kifudifudi, wala asisahau mauti hata kwa kitambo kidogo.

Basi, muhtasari wa maneno ni kwamba dhabihu zilizo katika Islam ndio kwa kusudio hili, na ni kwa kuhimiza kujipatia daraja hii, na ni msingi kwa ule uhakika unaopatikana baada ya kumsogelea Mungu kikamilifu. Hivyo, ni wajibu kwa kila mwaminio mwanamume na mwanamke atafutaye radhi ya Mungu Wadudi kwamba afahamu uhakika huu na kuufanya kuwa makusudio hasa na kuingiza nafsini mwake hata kwamba huo upate kupenya katika kila chembe yake. Na mtu asipate kumakinika wala kutulia kabla hajatoa dhabihu hii kwa Mola Mwabudiwa. Wala asikinai kwa mfano tu na kwa ganda kama majahili na vipofu, bali atekeleza uhakika wa dhabihu yake, na atimize roho ya dhabihu kwa akili yake yote na roho ya uchamungu wake. Hii ndiyo daraja inapoishia safari ya wamwendeao Mungu na upeo wa makusudio ya wamtambuao Yeye, na hapo ndipo zamalizika daraja za Wacha-Mungu, na hatua zote zakamilika hapo za Ma-Siddiki na wateule; na hapo ndipo mwisho wa mwendo wa Mawalii.

Na kama ukiishafika kwenye darja hii, basi umeishafikisha juhudi zako mpaka upeo na umeishawasilia daraja ya kujipoteza ndani ya huba ya Mungu. Basi, hapo mti wa kumkurubia Mola umefikia ukuaji mtimilifu. Na shingo ya roho yako itawasilia majani mabichi ya bustani ya utakatifu na ukuu kama yule ngamia jike mwenye shingo ndefu alipoisha fikisha shingo yake kwenye mti uliostawi. Baada ya hapo kuna mivuto, minukio na madhihirisho matukufu ya Mungu Aliye Mmoja, ili kukata vena zilizobaki za ubinadamu. Baada ya hayo kuna kuihuisha na kuibakiza na kuisogeza karibu na Mungu nafsi iliyotulia, iliyomridhia Mungu na Mungu Ameridhia iliyotilifika ndani ya Mungu, ili mtu ajiweke tayari kupokea neema baada ya kupata maisha ya pili. Na baada ya hapo mtu huvalishwa na Mungu joho la Ukhalifa, na anajaaliwa sifa za Kiungu kwa njia ya kivuli ili daraja ya Ukhalifa ithibitike. Na halafu anashuka kwenye mahuluku ili kuwavutia kwenye mambo ya roho na kuwatoa katika giza la kiardhi na kuwapeleka kwenye mwanga wa kimbingu. Na anafanywa mrithi wa kila aliyepita kabla yake, yaani Manabii na Ma-Sdiddiki na wenye elimu ya ufahamu na majua ya ukaribu na uwalii wa Mungu. Na anajaaliwa elimu ya waliopita na maarifa ya waliotangulia miongoni mwa wenye busara na wenye hekima ya dini ili kuthibitisha daraja ya urithi. Kisha mja huyo anakaa duniani hadi muda Alioupenda Mola wake, Mola mwenye heshima, ili awang'arishe mahuluku kwa

mwanga wa mwongozo. Na anapoisha waangaza watu kwa nuru ya Mola wake au akiisha fanya mahubiri kwa kiasi cha kutosha, hapo jina lake linatimia na Mola wake Anamwita na roho yake hurufaishwa kwenye nukta yake ya nafsi. Na hii hii ndiyo maana ya kurufaisha mbele ya wenye elimu na maarifa. Na arufaishwaye ndiye yule anyweshwaye kikombe cha mwungano na Mungu, kwa mikono ya Yule mpendwa aliye mto wa uzuri, na huingiza chini ya shuka la Urabi juu ya kuwa utumishi wake wa kudumu. Na hii ndiyo daraja ya mwisho anayofikia mtafutaji wa haki katika maisha ya binadamu. Basi, Enyi mahuluku, msiighafilikie daraja hii wala siri iliyopo katika dhabihu. Na mzifanye dhabihu kuwa kama vioo kwa kuona uhakika huu. Na msipitiwe na wasia huu, wala msiwe kama wale walioshahau Mola wao na mauti yao. Na imeashiriwa kwenye siri hii iliyofichika, ndani ya maneno ya Mola wetu Ajitegemeaye. Yeye Akasema: 'Sema, hakika sala yangu na ***Nusuk (Ibada)*** yangu, uhai wangu na kifo change ni kwa ajili ya Mola wa walimwengu.' Angalia jinsi Alivyofasiri '***Nusuk'*** kwa neno '*uhai' na 'kifo',* na kwalo Ameashiria kwenye hakika ya dhabihu. Basi, tafakarini, ndani yake, Enyi wenye akili.

Na yule aliyedhabihi akiwa ametambua hakika ya dhabihu yake na kwa ukweli wa dhamira na ikhlasi ya nia, basi akadhabihi nafsi yake na wanawe na wajukuu wake, na kwake kuna ujira mkubwa kama ujira wa Ibrahimu[as] mbele ya Mola wake Karimu. Na kwenye hii hii aliashiria Seyidna Mustafa Mtume[saw] wetu Mteule na

aliye Imamu wa wacha Mungu na Khatamun Nabiyyina, na kasema — naye ndiye mkweli kuliko wakweli wote baada ya Mwenyezi Mungu — kwamba kwa yakini dhabihu ndio rikabu wanaofikisha kwa Mola wa mahuluku na kufuta makosa na kuondoa mabalaa. Maneno hayo yametufikia kutoka kwa Mbora[saw] wa viumbe — juu yake amani ya Mwenyezi Mungu na baraka ng'avu. Yeye ameashiria ndani yake kwenye hekima za dhabihu kwa maneno yaliyo lulu zing'aazo.

Basi, ni masikitiko, masikitiko sana mno, kwamba watu wengi hawafahamu nukta hizi zilizofichika, wala hawaufuati wasia huu. Idi haimaanishi kwao isipokuwa kuoga na kuvaa nguo mpya na kula mno kwa kujaza kinywa pamoja na watumishi wa watumwa, kisha kutoka kwa kujipamba ili kusali sala ya Idi kama ndio matajri wakubwa. Na utaona kuwa furaha yao kubwa zaidi siku hiyo ni kula vyakula vizuri vinono, na utashi wao wa hali ya juu ndio mavazi mazuri ili kuwaonyesha watu. Hawafahamu dhabihu ni kitu gani na kwa sababu ipi mbuzi na ng'ombe wanadhabihiwa. Kwao, Idi yao tangu kucha hadi kuchwa ndio kwa ajili ya kula na kunywa na maisha anisi, na mavazi mazuri, na kuwapanda farasi wakimbiao kwa kasi sana, na nyama mbichi. Hutaona kuwa shughuli yao siku hiyo ni minghairi ya kujivalia nguo nyororo na kuchana nywele zao na kutia wanja machoni na kutia uturi mavazini, na kupamba ncha za juu ya vilemba na kuremba mashungi ya nywele kama wanawake wajipambavyo. Kisha

wanafanya harakati mara chache ndani ya sala jinsi kuku adonavyo punje, pasipo kutia moyo ndani yake, pamoja na wasiwasi mwingi na moyo usiotulia. Tena kazi yao ni kuvutika kwenye vyakula vya namna namna na maakuli ya aina aina na kujaza tumbo kwa neema mbalimbali kama wanyama na mahayawani, na kuelekea kwenye michezo na burudani na mambo ya kijahili, na kuziacha huru nafsi zao malishoni mwa anasa na kupanda juu ya farasi, magari ya farasi, ngamia, ngamia jike, nyumbu na shingo za watu, wakijipamba kwa mapambo ya namna namna; na kupoteza siku nzima katika mambo ya upuuzi na kupelekeana zawadi ya nyama na kufaharia kwa nyama za ng'ombe na wanambuzi. Na wanashughulikia furaha na starehe na mambo ya kuvutia nafsi na maasi na kucheka na kuangua kicheko mpaka magego na meno ya mbele kuonekana, na kucheza ngoma pamoja na makahaba na kuwabusu na kuwakumbatia na halafu mkanda wa kiunoni. Basi, twasema *innaa lillahi* juu ya misiba ya Islam na mageuko ya zama. Nyoyo zimejifia, dhambi zimekithiri masumbuko yamezidi, basi wakati wa usiku huu wenye giza totoro na wakati wa kiza kinene cha dhoruba kali, rehema ya Mwenyezi Mungu ilitaka kwamba ishuke nuru kutoka mbingu.[10] Hivyo, mimi ndimi ile nuru na

[10] Haya yaliyoandikwa ndani ya Hadithi kwamba Masihi atashuka, neno hili la *nuzuul* — kushuka — limechaguliwa kuashiria kwamba katika zama zile kiza kitavavagaa kote ardhini, uaminifu, amana

Mujadidi niliyetumwa, na mja niliyesaidiwa, na Mahdi niliyekuwa nimeahidiwa, na Masihi Mau'udi. Nami

---

na ukweli vitatoweka duniani na ardhi itajaa dhuluma na ujeuri. Ndipo Mungu Atateremsha nuru toka mbinguni na kuing'arisha ardhi mara nyingine. Hiyo itakuja toka juu, kwani nuru daima huja toka juu. Na wakati wa ujaji wa Masihi umeelezwa kuwa ni wakati ambapo njia zote za kuieneza Islam zitasitishika, na mikono miwili ya Waislamu itakuwa haina nguvu, kwani ghera ya Mungu itataka kuiondoa kuifutilia mbali shutuma hii kuwa Islam ilienezwa kwa upanga. Hivyo kwa zama za Masihi Mau'udi, ni amri ya kutia panga ndani ya ala zake na mtu yeyote asiinue upanga. Kama akiuinua, atashindwa vibaya sana mbele ya makafiri na atadhalilika kama vile kundi la wafuasi wa Hadhrat Musa[as] waliofukuzwa katika Misri na hawa, siku zote waliendelea kushindwa katika vita walizopigana kinyume na utashi wa Musa[as]. Basi, hata sasa itakuwa hivyo hivyo. Kwani, kushuka kwa Masihi Mau'udi toka mbinguni kumechukuliwa kutokana na maana hii hii ya ndani ya kwamba mkono wake hautazigusa njia za kidunia, bali kwa maji tu ya mbinguni atainyweshelza bustani ya Islam. Sababu yake ni kwamba Mwenyezi Mungu sasa Anataka kuonyesha mwujiza huu kwamba Islam haihitaji upanga wala njia za kibinadamu kwa kuenea. Hivyo, juu ya kukatazwa wazi wazi na kuwepo kwa Hadithi *Yadha'ul Harb*, anayeinua upanga na kutaka kuwa mpiganaji vita, huyo kana kwamba anataka kuutilia shaka mwujiza huu ambao Mwenyezi Mungu Ametaka kuudhihirisha, yaani kuishindisha Islam duniani bila njia za kibinadamu na kuifanya ipendwe na mahuluku. Mwandishi.

ninayo daraja mbele ya Mwenyezi Mungu asiyeijua yeyote katika watu, na siri yangu imefichika na iko mbali sana na Mawalii wengi achilia mbali watu wa kawaida. Na daraja yangu ni mbali sana na wanaozama mbizi (katika bahari ya maarifa), na mpao wangu ni juu mno kuliko makadirio ya wakadiriao. Mwendo wangu katika njia ya Mungu ni wa kasi zaidi kuliko ngamia waendao kwa haraka sana. Basi, msinilinganishe na yeyote awaye, wala yeyote yule na mimi, wala msijiangamize kwa kutia shaka na kupigana. Mimi ni kiini kisichokuwa na ganda, na roho isiyo na mwili, na jua lisilofichwa na moshi wa uadui. Mtafuteni mithili yangu, hamtampata katu hata mkimtafuta kwa kutumia taa. Na hii siyo fahari bali ni kutoa shukurani kwa neema za Mwenyezi Mungu Aliepanda mti huu. Nami nimeogeshwa kwa maji ya nuru na kutakaswa na uchafu na taka kwa chemchem ya Utukufu wa Mungu. Mungu Mwenye Enzi Ameniita jina Ahmad, basi nisifuni, na msinitukane, wala msifikishe jambo lenu hadi kukata tamaa. Na yule aliyenisifu na hakubakiza namna yoyote ya sifa njema, yeye hakuongopa. Na yule aliyekadhibisha maneno haya ndiye yeye aliyeongopa na kumghadhibisha Rahmani. Basi, ni masikitiko kwa yule aliyetia shaka na kuvunja ahadi na akauchafua moyo kwa wasiwasi wa shetani. Mimi nimefika kutoka kwa kizingiti cha juu sana ili Mola wangu Aonyeshe kwa njia yangu baadhi ya sifa Zake za Kijalali na za Kijamali, yaani kuondoa shari na kufikisha heri, kwani zama zilimhitaji yule aiondoaye

shari iliyopita kiasi na ainyanyuaye heri iliopotea na kufichika. Basi, ukarimu wa Mungu ulitaka kwamba zama zijaaliwe kile kitu zinachoomba kwa ulimi wa hali, na wanawake kwa wanaume wahurumiwe. Hivyo, Akanifanya kuwa dhihirisho la Masihi Isa[as] bin Mariamu kwa kuondolea mbali madhara na kuangamiza sababu za upotevu, na Akanifanya niwe dhihirisho la Nabii Mahdi Ahmad Akram[saw] ili kuwatolea watu heri na kurudia kuleta mara nyingine mvua ya ujuzi na mwongozo, na kuwatakasa watu na taka za usahaulifu na dhambi. Basi, nimefika nikijivalia mavazi mawili ya njano yaliyotiwa rangi ya kijalali na rangi ya kijamali, nami nimejaaliwa sifa za kufisha na kuhuisha kutoka kwa Mola Awezaye sana kutenda *Apendavyo.* Ama sifa ya kijalali niliyojaaliwa, basi hiyo ni athri ya mimi kuwa *Buruuz* — dhihirisho — ya Isa[as] kutoka kwa Mwenyezi Jalali[11] ili niteketeze ushirikina usiodhibitika uliopo katika itikadi za wapotevu, unaowaka kikamilifu ambao ni mbaya zaidi kuliko kila shari machoni mwa Mwenyezi Mungu Mjuzi wa hali zilizopo, na ili nibomoe kwayo nguzo ya uongo na uzushi juu ya Mwenyezi Mungu. Na sifa ya Kijamali niliyojaaliwa ndiyo athari ya mimi kuwa *Buruuz* — dhihirisho — ya Ahmad[saw] kutoka kwa Mwenyezi Mungu, Mkarimu, Mpaji, ili nirudishe kwayo

[11] Nimesema mara nyingi kwamba sikuja na panga na mikuki, bali ninazo ishara na nguvu takatifu na ufasaha wa kusema. Basi jalali yangu ni ya kimbingu, sio kwa majeshi. Mwandishi.

wema wa itikadi ya Umoja wa Mungu iliyotoweka kwenye ndimi, nyoyo, kauli na matendo, na niimarishe kwayo uchamungu na dini. Nami nimeamrishwa kuua[12] nguruwe za ufisadi, ukosefu wa imani na upotevu, ambao wanakanyaga chini ya miguu lulu za ukweli na kutilifikisha mashamba ya watu na kuharibu makonde ya imani na uchamungu na amali. Na kuua huku ndio kwa silaha ya kimbingu sio kwa panga na mishale jinsi wadhanivyo walionyimwa ukweli na kauli iliyo sawa. Kwani hao wamepotea na kuwapoteza wengi miongoni mwa majahili. Na kwa hakika nimeharamishwa kupigana vita, na amri hii imenisabikia kabla ya uwepo wangu, kwamba niache vita wala nisifanye kitali. Basi, hakuna jihadi isipokuwa jihadi ya mdomo na kuonyesha ishara na hoja. Kadhalika nimeamuriwa kujaza nyumba za waaminio na ghala zao kwa mali, lakini si kwa fedha na dhahabu bali kwa elimu na mwongozo na hidaya na yakini kikamilifu, na imani iimarishwe zaidi sana kuliko milima na kuwatolea habari njema wale waliolemewa na mizigo. Hivyo, muwe na habari njema kuwa ameishafika Masihi, na Mungu Mweza Amemtawaza kumfanya Masihi na kumjaalia maneno yenye ufasaha. Yeye anawakingeni na kundi fulani linalosafiri ardhini

---

[12] Neno hili ni neno la Hadithi kama ilivyokuja katika Bukhari. Na muradi wa kuua ni kuitimiza hoja na kubatilisha iliyo batili kwa dalili madhubuti na ishara za kimbingu, sio kuua kwa hakika. Mwandishi

kupoteza watu, na anapiga kelele na kuwaiteni muje kwa Mwenyezi Mungu. Yeye anaiondolea mbali kila shaka na kuifuta. Hivyo, muwe na habari njema kwamba amewajieni Mahdi aliyekuwa ameahidiwa. Anayo mali nyingi pamoja naye na bidhaa zilizorusika, naye anajitahidi kwamba mrudishiwe utajiri wenu uliopotea na ustawi wenu, uliozikwa kaburini ukiwa hai, utolewe nje. Hili si jambo lililozushwa, bali ni nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu iliyo na ishara kubwa pamoja nayo.

Enyi watu, mimi ndimi Masihi wa Ki-Muhammad[saw], nami ndimi Ahmad Mahdi, na Mola wangu Yu pamoja nami mpaka niingie kaburini. Na mimi nimejaaliwa moto unaoteketeza kabisa, na maji baridi. Ni nyota Yamani, na mvua ya Kiroho; udhia wangu ni mkuki mkali na dua yangu ni dawa mujarabu. Naionyesha kaumu moja sifa yangu ya kijalali, na kaumu nyingine sifa ya kijamali. Ninayo mkononi mwangu silaha iyaangamizayo mazoea ya dhuluma na dhambi; na katika mkono wangu mwingine mna sharubati ambayo nahuisha kwayo nyoyo mara nyingine, na shoka kuhilikisha na pumzi kuhuisha.

Ama sifa yangu ya kijalali, hii ndiyo kwa sababu watu wamekusudia kuning'olea mbali ja Ibni Mariam. Na sifa yangu ya kijamali ni kwa sababu rehema yangu imebubujika kama Seyidi Ahmad[saw] ili niwaongoze watu waliomsahau Mola Mtukufu.

Je mwastaajabia jambo hili, na hamzingatii hali ya zama na mahitaji yake. Je hamzingatii zama zinazomhitaji Mola Afanyaye sana Apendavyo, ili Awaonyeshe watu fulani sifa yake ya kijalali, na watu wengine sifa yake ya kijamali. Ishara zimekwisha dhihirika na alama zimebainika na migogoro imekwisha. Jua na mwezi vimepatwa katika mwezi wa Ramadhani, lakini hamfahamu. Baadhi ya watu wamekufa sawa na utabiri na wengi wakauawa, lakini hamtafakari. Ishara nyingi zimedhihiri juu ya ukweli wangu, lakini hamjali.

Ardhi, mbingu, maji na udongo vilitoa ushahidi wa ukweli wangu, lakini hamwogopi. Akili, maandiko, alama na ishara vilibainisha, na ushuhuda, ruya na kashfi vilifafanua, hata hivyo mnakataa. Kwa hakika ishara hizo zina shani kubwa kwa watu wanaozingatia. Na nyota *Dhus Siniin* imetokeza na sehemu ya tano ya karne hii imeishapita isipokuwa miaka michache, basi semeni yuko wapi Mujadidi kama mnajua. Tauni imeshuka kutoka mbinguni na hija imezuiliwa, vifo vimekithiri. Kaumu zimegombana juu ya mgodi wa dhahabu nao wanapigana. Msalaba ulinyanyuka na Islam ikaondoka mahali pake na ikapotea kana kwamba ni msafiri. Ufasiki umekithiri na mafasiki pia. Pombe, kamari na dansi vimewapendeza watu, wazinzi na watumianao ukali wamedhihiri na wacha Mungu wamepungua. Na wakati wa Mola wetu umefichuka na yametimia yale waliyoyasema Manabii. Basi jambo gani mtaliamini baada yake?

Enyi watu, simameni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, makundi kwa makundi au mmoja mmoja, na Mcheni Mungu na fikirieni kama yule mtu asiye bahili wala adui kwamba je wakati huu si wakati wa Mwenyezi Mungu kuwahurumia watu, na wakati wa kuondoa shari na kukata kiu ya nyoyo kwa kunyehsa mvua. Je mafuriko ya maovu hayajafikia kilele chake, na ujahili haujarefusha mapambizo yake? Nchi imechafuka na Iblisi amewatolea shukurani majahili. Basi, Mshukuruni Mwenyezi Mungu Aliyewakumbukeni na kudhukuru dini yenu na kuihifadhi isipotee, na Akakikinga na maafa kilimo chenu, mashamba yenu na mimea yake. Na Akanyesha mvua na kukamilisha raslimali yake. Na ili kuondoa madhara Akatuma Masihi wake, na Madhi wake kwa kutoa heri, na Amewaingiza katika zama za Imam wenu baada ya zama zilizokuwa za minghairi yake.

Enyi ndugu, zama zetu hizi zinalandana na mwezi wetu huu kikamilifu, kwani hizi ni zama za mwisho na mwezi huu ndio mwezi wa mwisho katika miezi ya kalenda ya Kiislamu, na hivyo, viwili vyakurubia kumalizika. Ndani ya mwezi huu kuna dhabihu na katika zama hizi pia kuna dhabihu; na tofatui ndiyo tofauti ya kitu na kivuli chake kionekanacho ndani ya kioo, na mfano wake umeishapita katika zama za Mbora[saw] wa mahuluku. Na dhabihu hasa ndio dhabihu ya roho, Enyi wenye busara. Dhabihu za mbuzi ni kama vivuli na alama, basi fahamu siri ya uhakika huu, nanyi baada ya masahaba[ra] mnayo haki na mnastahili kufahamu, na m wengine wao

mlioungana nao kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu na rehema yake. Na mfuatano wa zama umeishia kwa zama zetu kutoka kwa Yule Aliye Mmoja kama ilivyomalizika miezi ya Kiislamu kwa mwezi wa dhabihu. Na ndani mwake mna ishara iliyofichika kwa watambuzi na wenye busara. Nami ndimi ninayo daraja ya Khatam katika Uwalii jinsi Seyidi Mustafaa[saw] alivyokuwa kwenye daraja ya Khatam katika Unabii. Yeye ndiye Khatamul Ambiyaa, nami ndimi Khatamul Auliyaa, hakuna walii baada yangu isipokuwa yule atokanaye nami na kufungamana nami. Nimetumwa na Mola wangu kwa nguvu yote na baraka na heshima yote. Na mguu wangu upo juu ya mnara ambao kila kimo chaishia hapo. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu, Enyi watu, na nitambueni na kunitii na msife mkiasi. Zama zimekurubia. Na ni karibu kila nafsi iulizwe matendo yake na kupewa malipo. Mabalaa yapo mengi na hakuna kitakachowaokoeni isipokuwa imani. Hatia ziko kubwa na hakuna kitakachoziyeyusha isipokuwa nyinyi wenyewe kuyeyuka. Enyi wasaidizi wangu, iogopeni adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na kwa yule amchaye Mola wake kuna Pepo mbili, basi msikae na walioghafilika na walioyasahau mauti. Na Mkimbilieni Mwenyezi Mungu na wapandeni rikabu wenye mwendo wa kasi na waacheni ngamia wanyonge waendao chopi mkamfikie Mola wa viumbe. Jitengeni, jitengeni na vingine ili mjaaliwe muungano na ukaribu wa Mungu. Zivunjeni nyenzo zile, mkaumbiwe nyenzo nyingine. Jifieni ili

mkarudishiwe uhai, Enyi wapenzi. Leo hoja imekamilika juu ya wapinzani, na udhuru wote umevunjika wa waletao udhuru. Na makundi ya wapotezao na wenye kutia wasiwasi nyoyoni yamewakatieni tamaa. Ndio waliopoteza umri wao katika kutamani dunia, nao hawanayo hadhi katika dini, bali hao ndio kama vipofu. Leo Mwenyezi Mungu Amevunja uti wao wa mgongo na wamerudi wakikata tamaa. Leo ukweli umedhihirika kwa watazamaji na njia ya wakosefu imebainika. Na hakuna anayekengeuka isipokuwa yule aliyezuiliwa na kunyimwa tangu azali, wala hakuna mkana ila yule uliyemkataza uadui wa kitabia. Basi, twaachana nao kwa kusema 'salam.' Hoja imekamilika juu yao, na imeyakinika kuadhibiwa kwao. Na kama hata sasa wasijizuie, basi yafaa kusubiri, na Mwenye habari zao Atawatanabahisha.

## MLANGO WA PILI

Kisha baada ya hayo jueni, Enyi wenye busara, kwamba Mwenyezi Mungu ametaja ndani ya Kurani kuwa Yeye Alimtuma Musa[as] baada ya kuhilikisha nyimati za awali, na Akampa Kitabu na hukumu na Unabii na kuwajaalia wafuasi wake Ukhalifa na kuimarisha ndani yao silsila ya mwongozo na Akamfanya Ibni Mariamu, Isa[as], Khatam wa Makhalifa wa silsila hii, basi Isa[as] akawa ni tofali la msiwho la jengo hilo na kumfanya alama ya maanguko yake na ibra kwa aogopaye. Kisha Mwenyezi Mungu Akamtuma Nabii[saw] wetu Ummi katika ardhi ya Ummul Kura — Makka — na kumfanya kuwa mithili ya Musa[as], na kuifanya silsila ya makhalifa wake kama mithili ya silisila ya makhalifa wa Kaliim — Musa[as] — ili silsila hii kuitilia nguvu sisila ile. Hakika ndani yake mna ishara kwa aonaye. Na kama ukipenda uisome aya وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ — Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu — na usiifuate tamaa ya nafsi, kwani ndani yake mna ahadi ya Makhalifa kwa umati huu watakaokuwa mithili ya wale Makhalifa walioishapita hapo kabla ***katika Wana wa Israeli.*** Na mwungwana anapoahidi, anaitimiza. Nasi hatujui majina ya wale Makhalifa waliotutangulia katika umati huo hapo kabla isipokuwa wachache kati ya waliopita, wala Mola wetu Hakutuhadithia habari zao wote hao, wala hakutuambiwa majina yao. Hivyo, twawaamini kwa ujumla na utondoti wake twamwachia Mola wetu Mtukufu, lakini kwa sababu ya maandiko ya Kurani

hatuna budi kumwamini Khalifa mmoja miongoni mwetu atakayekuwa Khalifa wa mwisho juu ya nyayo za Isa[as]. Na mwaminio hawezi kuikataa, kwani hiyo itakuwa kukikataa Kitabu cha Mungu; na mkana hatafaulu popote afikapo. Basi, tafakari ndani ya Kurani ipasavyo kutafakari, na usiwe kama yule aliyetakabari na kukataa. Na hii ndiyo haki kutoka kwa Mola wetu. Uisome Sura An-Nuur kwa makini kabisa ili nuru hii ikudhihirikie kama mwanga wa mchana. Kadhalika uisoe aya صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ , na mashahidi hawa wawili wanakutosha kama unasikia na kuona.

Basi, kwa kifupi ni kwamba silsila ya Makhalifa wa Muhammd[saw] imekuwa mfano wa silsila ya Musa[as], ndivyo ilivyo ahadi ndani ya Kurani, kutoka kwa Mola wa mbingu zilizo juu. Kwani, Mwenyezi Mungu Aliweka silsila ya Makhalifa katika kaumu moja hapo kabla, yaani wana wa Israeli, na kuwateua na kuwajaalia heshima wana wa Israeli na kuweka ndani yao Unabii na kuwapatia muhula mrefu mpaka umri wao ukawa mrefu juu yao na wakatengana na uchamungu. Kisha ilipopita juu yao miaka mia tatu baada ya miaka elfu, toka siku alipotumwa Nabii Musa[as] ambaye Mwenyezi Mungu Aliongea naye na kumchagua, Mwenyezi Mungu Akamtuma Mtume wake Isa[as] bin Mariamu ndani yao na kumjaalia kuwa Khatam wa Manabii wao na kumfanya ishara ya saa ya kuhamisha Unabii pamoja na

adhabu, na Akawaonya na kuwaogopesha.[13] Yeye alikuwa hana baba kutoka miongoni mwa wana wa Israeli isipokuwa mamaake tu. Ndivyo Mwenyezi Mungu Alivyomuumba bila baba, na kutokana na jambo hili Akaashiria Aliyoashiria. Na hii ilikuwa ni ishara na alama fulani kwa Wayahudi na kuwahabarisha kwa kinaya kilichofichika na dokezo kwa kudhihiri kwa Nabii[saw] wetu, Mbora wa mahuluku. Na Mwenyezi Mungu Hakumfanya Masihi[as] kuwa Khatam wa silsila ya Musa[as] isipokuwa kwa kuwaghadhabikia Wayahudi. Basi, Akawahilikisha jinsi Alivyohilikisha nyimati za hapo kabla. Kisha Mwenyezi Mungu Akawachagua watu wengine na akazaliwa kwao mwana mwema ndani ya Ummal Kuraa — Makka. Naye ndiye Muhammad[saw], Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mpenzi wake aliyetumwa wakati wa kudhihirika ufisadi barani na baharini, na akafanywa kuwa mithili ya Musa[as] ili awaokoe watu na kila Firauni anayetawala kwa mabavu — juu yake amani ya Mungu na baraka zake mpaka siku

---

[13] Bi Mariamu alimzaa mwana asiyetokana na wana wa Israeli, na ikasemwa kuhusiana naye yaliyosemwa na kumwudhi kwa kupiga domo. Basi haya mambo mawili yalikuwa ni dalili ya uhamisho wa Unabii na kwamba kundi hili litaadhibiwa. Basi dhila ikawafikia Wayahudi kwa kufukuzwa katika bustani hii na kwa kughadhabikiwa na Mungu Mwenye nguvu Unabii ukahamishwa kwenye wana wa Ismeili. Kisha ikawasibu dhila na adhabu nyingine kutoka kwa wafalme wa zama, bali kila mfalme hadi wakati huu. Na humu mna ishara kwa wenye elimu na maarifa. Mwandishi.

atakapojaaliwa *Makami Mahmud* (Cheo Kilichosifiwa) na daraja za juu kabisa. Na Mwenyezi Mungu Ameanzisha kwa njia yake silsila nyingine mfano wa silsila ya Musa[as], ambaye yeye ndiye mithili yake hapa na huko Akhera. Na ahadi hii ilikuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ndani ya Torati na Injili na Kurani. Na ni nani atimizaye ahadi zaidi kuliko Mungu, na mkweli zaidi kwa usemi. Na wakati ambapo ahadi ya kushabihiana kwa silsila mbili za Ukhalifa ni ahadi iliyotiwa mkazo, kwa kutumia *Nuun Thakila*, na Mwenyezi Mungu, Mkweli wa kutimiza ahadi Ambaye ndiye wa kwanza kati ya watimizao ahadi, jambo hili lilihitaji kwamba Mungu Alete mwishoni mwa silsila ya Muhammad[saw], Khalifa ambaye awe mithili ya Isa[as]. Na Isa[as] alikuwa Khalifa wa mwisho katika dini ya Musa[as] kama ilivyoelezwa nyuma. Basi imewajibika kwamba Khalifa huyu asitokane na makureishi wala asije na upanga wala asiamuru kupigna vita, ili kushabihiana kutimilike, kama isivyofichika. Pia ililazimika kuwa adhihiri chini ya utawala wa kaumu nyingine, mfano wa kaumu ambayo katika zama za utawala wao Masihi alitumwe. Basi, uangalie kushabihiana huku kwamba ni wazi sana na kwang'aa mno. Nawe waelewa kuwa Isa[as] alikuwa amejikusanyia sifa hizi nne, na kadhalika Mwenyezi Mungu Alitaka hiyo hiyo kumhusu Masihi wa umati huu na Akatekeleza ili jambo la kulandana litimie, na lisiwe kama mgawanyo mbovu.[14] Na hii ilikuwa ni

[14] Ikisemwa kwamba Masihi aliumbwa bila baba kwa mkono wa

ahadi ya Mungu, na ahadi ya Mungu haibadiliki wala haisahauliki. Je hamsomi kitabu cha Mungu? Je haimo humo ahadi hii? Basi, Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye Kwake ndio marudio, na msiwe kama wale wasomao Kurani, lakini hawajali iliyoyaamrisha na kuyakataza Kurani. Na waambiwapo, 'Aminini Aliyoahidi Mwenyezi Mungu na msisahau hisa yenu katika rehema inayotarajiwa,' husema hatujui ahadi ni kitu gani. Nyoyo zao zimepigwa muhuri, hivyo hakuna kati yao asikiaye wala aonaye. Wala hawapokei haki ilhali tumewapatia dalili kama lulu zing'aazo. Je hawaiangalii Kurani, au kuna kifuniko juu ya macho yao? Basi, kwa hiyo hawakioni kilichochomoza na kuangaza. Na miongoni mwao kuna watu waliojaaliwa elimu, hata hivyo wanapita tu kama yule aliyekengeuka na kukana. Na ukiwauliza ni nini Aliyoahidi Mola wenu Mtukufu, wanasema kuwa Yeye Amewaahdidi waaminio kwamba Atawainua Makhalifa kutoka miongoni mwao jinsi Alivyowainua Makhalifa kutoka miongoni mwa kaumu ya Musa[as]. Basi wanakiri kushabihiana kwa sisila hizi mbili kisha wanakataa kama yule mwenye macho anayejisingizia kuwa kipofu.

---

Kudra, na hili ni jambo lililo kinyume na tabia ya Mungu basi habari za kushabihiana haitimii hapo, na ni wajibu kufanana kama isivyofichika kwa mwenye akili timamu, basi twasema kwamba imo ndani ya tabia ya Mungu Mweza Mwenye hekima kumwumba binadamu bila baba. Na hatukubali kuwa hii

Na katika hali Nabii[saw] wetu alipokuwa mithili ya Musa[as] na silsila ya Makhalifa wake kuwa mithili ya silsila ya Musa[as] kwa maneno ya wazi kabisa, basi imewajibika kuwa silsila ya Muhammad[saw] iishie kwa Khalifa aliye mithili ya Isa[as], jinsi silsila ya mwenye Fimbo — Musa[as] — ilivyomalizika kwa Ibni Mariamu[as], ili sisila hii ilingane na silsila ya awali, ili kwamba ahadi ya kufanana makhalifa wa silsila mbili kama ibainikavyo toka kwa neno *'kama'*. Basi, nionyesheni Khalifa yeyote minghairi yangu aliyekuja juu ya nyayo za Ibni Mariamu[as] kutoka miongoni mwenu na zama zake zilandane na zama zilizopita za Nabii Isa[as]. Na umeishapita muda kutoka kwa Nabii[saw] wetu hadi siku ya leo hii sawa na muda uliokuwa baina ya Musa[as] na Isa[as]. Ndani mwake mna ishara kwa watu watafutao mwongozo.

Basi, imekuwaje, kwa nini mwamngojea Masihi kushuka toka mbinguni? Je mmepitiwa muyasomayo ndani ya Kurani, au mmeridhika kukadhibisha maneno ya Mola wenu Mtukufu? Je mwakikadhibisha Kitabu cha Mungu ilhai ki bahari ya maarifa na maji safi kabisa.

---

ndiyo nje ya tabia yake na haifai kuikubali.★ Kwani pengine mtu amezaliwa kwa shahawa ya mwanamke peke yake, walau kwa nadra. Hili haliko nje ya kanui ya asili, bali ipo mifano yake na habari zake katika kila kaumu, na matabibu na wazoefu wameitaja. Naam, twakubali kuwa tukio hili linaadimika, lakini sio

---

★ Je hukuona Adamu[as] hakuwa na wazazi wote wawili. Basi, imekwisha thibitika tangu mwanzo wa zama kwamba tabia hii ni miongoni mwa tabia ya Mungu. Mwandishi

Mmependaje kutengana na Kurani Tukufu kwa ajili ya kauli za aina mbalimbali! Je mwabadili kilicho hafifu kwa kile kilicho bora? Na dhana haisaidii kitu mbele ya haki. Jua na mwezi vimekutanishwa kama ilivyotaja Kurani na vimeishapatwa katika Ramadhani kama mwezi ulivyopasuliwa katika zama za Mbora[saw] wa viumbe. Na ngamia wameishaachwa kwa yule aonaye, na tumejaaliwa rikabu wa aina nyingine ili tuweze kutalii zaidi kuliko Masihi[as] na tutekeleze jukumu la Tabligh kwa ukamilifu zaidi kuliko yeye. Itazameni fadhili ya Mungu ya kwamba Yeye akadhihirisha ushahidi mmoja kwa ajili yangu toka mbinguni na ushahidi mmoja toka ardhini na Akaonesha jambo kama mwanga wa mchana. Je Hamwoni kushabihiana katika Ukhalifa uliokuja na Ukhalifa uliopita. Ndani mwaka mna ishara kwa yule

---

kinyume na kanuni ya kuzaliwa. Na kadhalika ilikuwa kuzaliwa kwangu kutoka kwa Mungu Aliye wa pekee★ na mfano wake ulikuwa ni adimu. Na kiasi hiki chatosha kwa mtu mwema. Kwani nilizaliwa pacha, pamoja nami mtoto mmoja wa kike alizaliwa kijijini humu ambaye alifariki, nami nikabaki hai kwa amri ya Mungu Mwenye Enzi. Bila shaka tukio hili ni adimu kulingana na njia ijulikanayo inayoshuhudiwa. Na kwa kushabiahiana, kiasi hiki chatosha kwa kushirikiana katika kuwa nadra mbele ya wenye akili na utambuzi. Kwani, kufanana hakulazimishi isipokuwa kwa njia fulani moja wala hakutaki

---

★ Ishitoshe, mimi nimetumwa nikijivalia mashuka mawili ya njano, nami naishi na magonjwa mawili — ugonjwa mmoja katika sehemu ya chini ya mwili na ugonjwa mmoja katika sehemu ya juu. Basi uhai wangu ni wa kustaajabisha zaidi kuliko kuzaliwa kwa Masihi, na ni mwujiza kwa aonaye. Mwandishi

azindukaye na kujiondelea mbali usingizi. Je hamloli kwenye zama nilimotumwa, nami nimewajia baada ya Mtume[saw] Mteule wa Mungu katika muda sawa na ule uliokuwa baina ya Musa[as] na Isa[as]. Ndani mwaka mna ishara kwa wenye busara. Tazameni jinsi ishara zilivyojumuika toka kwa Mungu Mtukufu Aliye juu. Basi, mwei na jua vilipatwa katika mwezi wa saumu; ngamia waliachwa wasitumike kama rikabu; na zipo ishara nyingine pamoja na hizo. Je ishara kama hizo zimepata kujumuika siku yoyote kwa kadhabu azushaye uongo? Basi, iogopeni jahanamu iwalayo wakosefu, na mkosefu hafi ndani yake wala hahuiki. Je mwakitupa Kitabu cha Mungu nyuma ya migongo yenu na mnazifuata kauli zingine? Hii sio ila ni uasi na dhuluma na kutoka katika mwongozo. Na kila heri imo ndani ya

---

kushabihiana kwa sifa fulani. Tusemapo kimajazi, mathalai, 'mtu huyu ni simba', hatuwajibikiwi kuthibitisha kuwa mtu huyo anacho kila kitu kipatikanacho katika simba kama vile mkia, ngurumo, sura ya ngozi na mambo yanayotakiwa kwa mnyama mbuai. Tena uelewe kuwa kuzaliwa kwa Isa[as] bin Mairamu bila baba ndani ya Wana wa Israeli kwa njia hii ni onyo kwa Wayahudi na ni alama ya saa zao za maanguko na ni ishara kwamba hakuna budi Unabii utaondolewa kwao. Ama Masih wa umati huu, huyu amezaliwa pacha, mtoto wa kiumu na wa kike, na katenganishwa na hali ya kike. Ndani yake mna ishara kwamba Mungu Ataeneza katika kundi hili wanaume wengi wenye ikhlasi na utakaso. Basi, malengo ni tofauti katika kuzaliwa huku na huko, ndiyo sababu njia za kuzaliwa zimekuwa mbalimbali kutoka kwa Mungu Mtukufu. Mwandishi.

Kurani, na kushikamana nayo ndio adabu ya uchamungu. Kwa hakika ardhi na mbingu zimetoa ushahidi kwa ajili yangu; je hizo zaweza kushuhudia kwa minghairi ya mkweli adaipo?

Basi, fahamuni kuwa mimi ndimi Masihi Mau'udi, na Mahdi aliyekuwa ameahidiwa kutumwa na Mungu na Islam kuwa kama gharibu ili kwa njia yangu itimie ahadi ya haki. Na haya sio maneno yaliyozushwa. Kama ningekuwa mzushi, si mkwei, zisingejumuika ishara zilizojumuika; na Mwenyezi Mungu Hamsaidii aongopaye na kumtungia Mungu uongo na kupita mipaka. Kwa yakini kuna ishara kadhaa juu ya ukweli wangu katika zama zangu, mahali pangu, kaumu yangu na kaumu ya maadui zangu, kwa yule atafakariye na asiyatakabari wala haringi. Nami nimewajieni nikiwa Mwamuzi mwadilifu ili niwabainishieni baadhi ya mambo mnayohitilafiana ndani yao na kumwua kila nyoka akimbiaye.[15] Sikuwasili wakati usiofaa, bali nimefika mwanzoni mwa karne wakati wa fitina zilizofikia kileleni. Nami sikuja pasipo hoja, na ishara nyingi zimetokea toka mbingu za juu. Ndimi zimekana lakini nyoyo zimeyakinia. Na Mwenyezi Mungu Akamwongoza Aliyemtaka kuongoza. Je mwashuku katika jambo langu ilhali ukweli umebainika na hoja zimedhihirika nyingi mno zisizohesabika. Je hamwiangalii Kurani ilhali inanishuhudia kwa maelezo

---

[15] Yaani, kila bidaa iliyoenezwa. Mwandishi.

wazi sana na yang'aayo? Na je imekufikia Hadithi ya Mbora[saw] wa viumbe aliponena: 'Mtakuwaje atakaposhuka ndani yenu Ibni Mariamu naye ndiye atakuwa Imamu wenu kutoka miongoni mwenu'. Basi, uzingatie kauli yake *minkum*, na uitafakari kama amchaye Mungu. Na Hadithi hii kwa yakini inawaelezeeni ile ile inayowabainishieni Kurani. Basi msitofautishe baina ya Kitabu cha Mungu na kauli ya Mtume[saw] wake Mteule, na Muogopeni Mungu ambaye kila nafsi itarejea kwake ili apatiwe malipo ya amali zake. Je hamfahamu Aliyosema Mola wenu? Namaanisha hii kauli yake: وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ mpaka maneno لَا يُشْرِكُوْنَ بِىْ شَيْـًٔا. Basi imekuwaje nyinyi mwamshrikisha Mungu na Isa[as] na dajali pasipo elimu na mwongozo toka kwa Mwenyezi Mungu, na mwamngojea Masihi awateremkieni toka mbinguni. Na awezaje kuteremka aliyeishakufa na kuungana na wafu! Je mnayo hoja madhubuti kuhakikisha madai yenu ndiyo maana mwaifuata, au mmeitanguliza dhana iliyofichika juu ya yakini? Ni sikitiko kwenu kwamba mmepitiwa na kauli ya Mwenyezi Mungu na kauli ya Mtume[saw] wake — namaanisha *minkum* — na mkadhani kwamba Masihi atakuja toka kwa mbingu za juu. Je hii sio kutengana na Kurani na Hadithi, na sio mchafuko mkubwa? Mwawezaje kuiacha Kurani, na upo ushahidi gani mkubwa kuliko huu kwa aliyeongoka. Na Kurani inayo shani kubwa kuliko kila shani, nayo ndiyo Mwamuzi na mwangalizi, na imejumuisha dalili zote na

kuwasambaratisha maadui. Na hii ndio Kitabu, ndani mwake kila kitu kimefafanuliwa, na ndani yake kuna habari za mambo yajayo na yaliyopita. Na batili haiwezi kuijia toka mbele yake wala nyuma yake, na hii ndio nuru ya Mola wetu Mtukufu. Basi uachane na kila kisa kihitilafianacho na maelezo yake, na usiiasi kauli ya Mola wako isije ukapatwa na mashaka. Na wajua kuwa Nabii[saw] wetu alikuwa mithili ya yule aliyeitwa katika bonde takatifu, Tuwaa — Musa[as]. Makhalifa wake walikuwa kama Makhalifa wa Mtume[saw]. Na milolongo hii miwili ililandana katika urefu wa vipindi vyao. Na ndivyo Alivyonena Mola wetu, nawe umeishaisoma nyuma. Na hii ndio hakika isiyopasa kusitiriwa wala kufichwa. Basi asikuzuie katika hayo yule afuataye matamanio yake na aliyeacha njia iliyo sawa na hali anaona. Na umejua kuwa nimefika baada ya Seyidi Mteule[saw] katika muda sawa na ule muda wa ujaji wa mwana wa Mariamu Siddika baada ya Musa[as], na wajua kuwa Khatam wa Makalifa wa umati huu ndio kutokana na umati huu huu, wala sio toka katika kundi jingine. Basi wawezaje kumkatalia mbali? Je utaikufuru Kurani kwa sababu ya kauli tofauti mbalimbali. Na yule azingatiaye aya ***layastakhlifannahum*** — لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ — moyo wake utajaa yakini na imani na atayaacha yaelezwayo na yasimuliwayo kinyume chake, na atafunukiwa uhakika na atamkadhibisha yule alongaye na kusimulia dhidi yake.

Basi, ole kwa yule aliyesikiliza dalili hizi kisha akakadhibisha na kukana. Je anadhani kuwa Mwenyezi

Mungu akafanya ahadi kisha akaivunja au akasahau ahadi yake kama yule mtu aliye msahalifu sana na dhuli. Mungu Ameepukana na upungufu huo, Ametukuka na Yu juu kuliko sifa hizo mbovu. Basi ni Hadithi gani mtakayoiamini baada ya Kitabu cha Mungu? Je mwatanguliza dhana juu ya ile yakini iliyowajieni? Na ni nani mdhalimu zaidi kuliko aliyeiacha haki na kuifuata matamanio? Je imebaki shaka yoyote katika Khatamul Khulafaa na ndani ya hii kwamba yu kutoka miongoni mwenu? Na kama ndivyo hivyo, basi leteni Kurani. Na haki imekwisha bainika, hivyo msiitupie mavumbi wala msiifiche ndani ya udongo; Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye mtarejeshwa kwake mmoja mmoja; nami sioni kwamba mtakuwa na marafiki wa dunia pamoja nanyi. Hivyo, simameni mmoja mmoja na msimwangalie aliye mpenzi au adui, kisha mtafakari kwa moyo umchao Mungu na akili ng'avu. Je Hakusema Mola wenu [16] لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ? Ndani yake kuna hoja dhidi ya apitaye mipaka. Kwani, neno *kama* lalazimisha kwamba silsila ya Makhalifa katika umati huu iwe mithili ya silsila ya Musa[as], Nabii wa Mungu, iliyoishia kwa Isa[as] mwana wa Mariamu. Basi mwaenda wapi kwa kuacha aya hii? Na mwaifanya njia ya karibu kuwa mbali. Na Wallahi hamna ndani ya Kurani yenye kutoa uamuzi isipokuwa habari za kudhihiri Khatamul Khulafaa ndani

---

[16] Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao. (Sura An-Nuur, 24:56).

ya umati wa Mbora[saw] wa viumbe. Basi, msiyafuate msiyo na elimu nayo, ilhali mmeisha jaaliwa mwongozo kuhusiana na jambo hili; wala msitamke midomoni mwenu maneno tofauti ambayo ndio kama mshale unaotupwa gizani. Hakika ahadi hii ndiyo ahadi ya haki, hivyo yaiswadanganyeni muyasikiayo kwa wenye matamanio. Na ndani ya Sura Al-Faatiha inaashiriwa hii mara nyingine, na mwasoma katika sala 'Njia ya wale Uliowaneemesha', kisha mwagandamana na njia za kukana na mwashauriana kwa siri. Mmekuwaje, mwakanyagilia mbali kauli ya Mungu chini ya miguu yenu. Je hamtakufa au mtaachwa bure? Mwanitaja jinsi watajawavyo makafiri, na mwasema, 'Muueni mkiweza', na mnaandika fatuwa za aina hii. Na nafsi haiwezi kufa ila kwa idhini ya Mungu, na wapo pamoja nami walinzi wanilindao na maadui. Basi, kusanyeni hila yenu kisha tazameni hila haimwangukii ila yule aliyedhulumu. Na yaelekea kwamba mumhesabu mtu kuwa mwongo ilhali yu mkweli katika madai yake. Hivyo, msielekee kabisa mbali na haki. Yule atenganaye na uchamungu huanguka. Niambieni kama nimetoka kwa Mungu nanyi mnakadhibisha, basi itakuwaje hali ya yule aliyepita mipaka! Mwachukia kwamba mja wa Mungu — Isa[as] — ajifie, ilhali hamnufaiki na uhai wake, na kwa Mungu kuna makusudio makubwa katika kifo chake. Je yeye anashirikiana na Mola wetu katika mbingu kwa hiyo haachi mahali pake wala hateremki? Hivyo, msipigane na Mungu kwa ujahili wenu, na msalieni Nabii[saw] wenu

Mteule; yeye ndiye njia ya muungano baina ya Mungu na mahuluku wake; yupo baina ya pinde mbili — *upinde wa Uungu na upinde wa upinde wa ubinadamu* — au karibu zaidi.

Je mmepata kusikia kwangu isiyowasikilizisha Kurani? Au mmemshuhudia Isa[as] huko mbinguni kwa hiyo ni vigumu kwenu kuyakadhibisha macho yenu? Ama mmedhania tu hivyo? Na kwa hakika dhana haisaidii kitu mbele ya haki. Nanyi mmeishajua kuwa Kurani imemfisha na kumtawafisha. Basi, hadithi ipi mtaiamini baada ya yake, ilhali mnakataa Aliyoteremsha Mungu na kufunulia. Je mwaiacha yakini kwa ajili ya dhana iliyoihilikisha kabla yenu kaumu fulani na kuiangamiza. Ole wao wasemao 'tu wanachuoni', lakini hawakunisaidia bali wakawa wa kwanza walioniudhi, ili watimize kwa ndimi zao utabiri wa Mtume[saw] na yale yaliyosimuliwa kutoka kwa Mbora[saw] wa mahuluku. Mtu mmoja aliye mdhalimu mkubwa kuliko wao akasema, 'Muueni mtu huyo, nachelea kuwa ataiharibu dini yenu au atawadhalilisheni atakapowashinda.

Enyi wenye husuda na matmanio, ole wenu, kwa nini mwayatanguliza maisha ya dunia. Kwa hakika Kurani inashuhudia kuwa Khatamul Khulafaa wa umati huu ni mja mmojawapo wa umati huu huu, na kwamba Masihi[as] ameishakufa. Na ni nani madhalimu zaidi kuliko yule aiasiye Kurani na kuikataa, ilhali i mwamuzi toka kwa Mwenyezi Mungu, hakuna hukumu ila

hukumu yake bora. Je haikuwatosha aya '*Uliponifisha*', au wanayo misahafu mingine? Na Sura An-Nuur yawakadhibisheni na Sura Al-Faatiha yawafungulieni mlango wa mwongozo. Kwani Mungu ameanzia ndani mwake chanzo cha zama na kuzifanya zama za mwisho kuwa zama za 'wapotevu', nao ndio Manasara kama ilivyotufikia toka kwa Nabii[saw] wetu Mteule. Basi ipo wapi habari za Dajali wenu, hebu tuonyesheni huyu ndani ya Kurani. Ameangamia aliyeiacha Kurani na kuwa adui wa mahadimu wake na kuwachukia. Je Mwenye habari na Mjuzi alisahau yale mliyoyakumbuka? Ama mmezua uongo juu ya Kitabu cha Mungu? Na ni nani mdhalimu zaidi kuliko yule azushaye uongo! Na kwa hakika hii — Kurani — ni kauli ipambanuayo isiyo na mavumbi juu yake, na hayo ni maelezo yaliyo wazi sana na yang'aayo. Hii ndiyo haki, na ni nani mkweli zaidi katika kauli kuliko Mwenyezi Mungu? Na ni nani aliye mjuzi zaidi kuliko Mola wetu Mtukufu? Je mnayo hoja iwazuiayo kuifuata Kurani? Basi, ileteni kama mkimcha Mungu na kama hamuyafuati matamanio. Mwatambua kuwa Sura Al-Faatiha ni asili ya Kitabu, nayo inawaambieni kweli na ndani mwake mmetajwa watukufu wa umati uliopita kabla na pia wametajwa watu wao wabaya walioghadhibikiwa na Mungu hapa duniani na wametajwa wale ambao sura hii inaishia kwao, yaani 'waliopotea', na mwakiri kuwa hao ndio Manasara. Na Mwenyezi Mungu Ameahirisha kuwataja katika Sura hii ili itambulikane kwamba fitina

yao ndiyo ya mwisho kati ya fitina zote. Basi hapakubakia mahali pa kukanyaga kwa dajali wenu, Enyi wenye akili. Na hayo ni makundi matatu ya *Ahli Kitab*, na ndivyo yalivyo ndani yenu makundi matatu ambayo yanafanana baadhi ya makundi yenu na baadhi ya makundi yao na kushabihiana. Na Mwenyezi Mungu Amewasisitizia waaminio kuomba dua hii. Kisha Akaahidi ndani ya Sura An-Nuur kuwa lazima Atawafanya watu kutoka miongoni mwao — *Waislamu* — jinsi Alivyowafanya Makhalifa hapo kabla ili kuwabashiria waaminio kwamba dua yao imekwisha pokelewa na Mungu Mtukufu kwa ajili ya baadhi yao. Basi, Enyi wenye busara, maelezo yepi ni wazi zaidi kuliko maelezo haya? Je mwapatwa na taabu kwamba Masihi wenu atokane nanyi wenyewe, au mwataka kuikadhibisha ahadi ya Mola wenu? Enyi watu wangu, mmetahiniwa na Mola wenu, hivyo msizisogelee hatia. Na Mwenyezi Mungu Hakuwahabarishieni kuhusiana na Isa[as] isipokuwa tu kubashiri kwamba Masihi mmoja atatokea kutoka miongoni mwenu mfano wa Masihi wa wana wa Israeli. Hivyo, mchangamkie ahadi kutimia na msihasimiane kama yule akengeukaye na kupinduka. Na mwajua kuwa Isa[as] alikuja katika zama za mwisho za Wayahudi, na ndivyo hivyo Alivyokadiria Mwenyezi Mungu muda uliowekwa kwa Masihi wenu ili itimie kushabihiana baina yenu na baina ya wale waliopita kabla. Basi, mmekuwaje mwashika njia minghairi ya njia ya Mungu, na mwasahau jambo Alilonuia Mungu na

kuamua. Na zama zetu hizi ni zama za mwisho jinsi ziivyokuwa zama za Isa[as] kwa Wana wa Israeli. Na Isa[as] alikuwa ni dalili ya saa *za maangamio* ya Wayahudi; nami ni dalili ya saa ambamo watu watajumuishwa na kila nafsi itahuishwa ili kupatiwa malipo yake. Na zimekwisha dhihiri alama zake nyingi na Kurani imezitaja sana. Ngamia wameachwa; vimesarwa vitabu na maandiko matakatifu; mwezi na jua vimepatwa katika Ramadhani; mito imetiririshwa; njia zimefunguliwa; watu wenu wakaunganishwa na watu wa nchi za mbali; milima mingi ikavunjwa, nanyi hamwoni ndani yake kombo wala miinuko; na ngamia wameachwa wasitumike kubeba mizigo wala kama rikabu. Basi, imethibitika kwamba zama zetu hizi ndio zama za mwisho zilizotajwa ndani ya Kurani, na imeainishika kuwa wakati huu ndio wakati wa *Khatamul Khulafaa* kwa umati wa Nabii[saw] wetu, Mbora wa mahuluku, na uhakikisho wa jambo hili umefikia ukamilifu wake na Mwenyezi Mungu Hakubakiza shaka yoyote iwayo wala dukuduku. Na kuhusiana na jambo hili tumejazwa tele maarifa na elimu timilifu na mwanga dhahiri, kiasi hiki kwamba kama pazia liondolewe hata hivyo hatuna nafasi ya kuzidi kiyakini. Je mwamwona mtu minghairi yangu ndani ya zama hizi asemaye mimi ndimi Masihi Mau'udi na ameleta ishara kubwa kama nilivyoleta mie? Basi, mmekuwaje hamumkubali yule aliyekuja katika muda baada ya Nabii[saw] wake sawa na muda wa Masihi kutumwa baada ya Musa[as]. Nami

nimekariri mara nyingi, Enyi wenye akili, kwamba mimi ndimi Masihi aliyekuwa ateremke kutoka kwa Mungu Mtukufu. Na kudhihiri kwangu kulikadiriwa kutokea katika mwisho wa silsila ya Muhammad[saw] kama mfano wa yule Masihi aliyefika mwisho wa silsila ya Musa[as] kwa idhini ya Mola ili silsila hizi mbili zilingane barabara na ahadi itimie. Na mkarimu aahidipo hutimiza. Basi sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Asiyepunguza haki ya umati huu wala Hakuwanakisia thamani. Nami naona jambo hili la kushabihiana jinsi kiatu kimoja kifananavyo na kiatu kingine. Basi, huoni dhuluma wala kunyimwa. Hivyo, usilikufuru lililohakikika kutoka katika Kurani, na useme: 'Mola wangu, nizidishie elimu.' Umekuwaje huyafuati aliyonena Mwenyezi Mungu, na unazifuata kauli nyingine, ilhali mwongozo utokao kwa Mungu ndio mwongozo hasa. Mwenyezi Mungu Amewatimizieni ahadi, basi mwaenda wapi toka kwenye ahadi yake na mnazua visa tofauti. Nanyi mwanufaika nini katika uhai wa Masihi, Enyi majahili, isipokuwa tu mwawasaidia Manasara kwa njia hii! Je hamwangalii kwenye zama ilhali msiba mkubwa umewashukieni. Kundi kubwa la kaumu yenu na wapenzi wenu wametanasari; nchi zimeangamia na watu pia, na Arshi ya Rahmani imetikisika kwa yale yaliyoshuka, basi yakatendeka yaliyotendeka. Na kama Mwenyezi Mungu Angalitaka kateremsha yeyote toka mbinguni — jinsi mdhanivyo — ingalikuwa bora kwenu kwamba Angemteremsha Nabii[saw] wenu Mteule. Je hamkusoma

kauli yake Yule Aliyetukuka kwamba kama Tungalitaka kumfanya mwana Tungalimfanya toka kwetu, yaani Muhammad[saw]. Hivyo tafakarini sana. Hakika mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana navyo vikaambuliwa katika zama hizi ili watahiniwe watu wema na wabaya, na kila kundi lipatiwe malipo ya matendo yake. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akatoa toka katika ardhi vitu kadhaa vilivyokuwamo humu na kuteremsha toka mbinguni aliyotaka kuteremsha toka mbingu za juu. Basi kundi moja likafundishwa hila za ardhi na kundi jingine likajaaliwa katika mwongozo waliojaaliwa mitume. Na ushindi ulikadiriwa kwa wale wa mbinguni katika vita hii. Mwamini au msiamini, Mwenyezi Mungu Hatamwacha mja wake Aliyemtuma kwa mahuluku, wala jua halitapotezwa kwa sababu ya kipofu kulikana. Makundi mawili yanahasimiana kuhusikana na wema na matamanio. Kwa kundi moja ilifunguliwa milango ya ardhi mpaka kwenye chini ya udongo; na kwa la pili, milango ya mbingu mpaka kwenye mkunazi wa mwisho. Ama wale waliofunguliwa milango ya ardhi, hawa wanamfuata shetani wao aliyewashawishi; na wale walofunguliwa milango ya mbingu, hawa ndio warithi wa Manabii na watu waliotakaswa na tamaa na matamanio, hao wanaiita kaumu yao kwa Mola wao na wanawakataza vile ambavyo Mwenyezi Mungu Anashirikishwa navyo katika ardhi na mbingu za juu. Nami nimetumwa ndani yenu toka kwa Mwenyezi Mungu msiyemtukuza, ili niwaonye watu wapitao kiasi kumsifu Isa[as] mwana wa Mariamu.

## MLANGO WA TATU

Enyi watu, ni nini masanamu haya mnayotegemea? Je mwaliacha Neno la Mungu kwa kauli msizojua uhakika wake. Kefule kwenu na kwa hayo mnayoyazusha! Kauli hizi hazikuhakikisha kwenu wala wale wenye kutoa hizo; nanyi mwadhania tu. Je mwatanguliza dhana juu ya yakini, ilhali dhana haisaidii kitu mbele ya haki, wala hamuwezi kujiondolea lawama hii. Mwenyezi Mungu Ameahidi kuwa Atawafanya Makhaifa katika umati huu; je mwaikana? Naye hakuahidi kuwa Masihi wenu atateremka toka mbinguni; na kama ameahidi, basi tuionyesheni ndani ya Kurani, kama mkisema kweli. Na imethibitika kutokana na ahadi yake kwamba Khatamul Khulafaa atakuwa kutoka miongoni mwetu; je mna shaka ndani yake? Basi, ugomvi gani umebakia baada yake; mmekuwaje hamzingatii! Msipaaze sauti zenu dhidi ya Kitabu cha Mungu, na Kurani imekwishatoa uamuzi kuhusiana na ile mnayohitilafiana ndani yake. Je hamridhii iliyoamua Kurani? Na Mungu ndiye Anastahiki kwamba kauli yake ikubuliwe kama m waaminio. Na Mwenyezi Mungu Amemfanya wa kwanza wenu na wa mwisho wenu kuwa mfano wa silsila ya Musa[as]. Je mwashukuru? Mwangalieni mithili ya Musa[as] — Seyidi wenu na Nabii[saw] wenu — mwanzoni mwa silsila, basi yuko wapi mithili ya Isa[as] mwishoni mwake? Ama silsila hii imepungukiwa, Enyi wenye kutafakari! Je hamwoni fitina za wale watu wanaokuja mbiombio toka kila mahali pa juu? Nanyi mmefanywa

chini ya miguu yao kama adhabu toka kwa Mungu, hata hivyo hamrejei. Huenda Mola wenu Akawarehemu. Ole wenu, kwani hamsikii. Je mwatumaini kuwa Isa[as] atashuka toka mbinguni? Haiwi! Haiwi! Mnayotamani. Je mwatarajia kuwa Mungu Atavunja ahadi Yake na Atayafuata matamanio yenu, Enyi waongo! Lau kama Mwenyezi Mungu Angaliyafuata matamanio yenu, bila shaka ***Tauhid*** yote ingefutika kabisa na ushirikina ungekithiri na washirikina pia. Na Mwenyezi Mungu Hatumi mtume ardhini ila kuondolea mbali machafuko yaliyoichafua ardhi, basi angalieni machafuko haya, Enyi wenye akili. Ni sikitiko kwao, wanayatazama yaliyoiangukia Islam lakini hawaoni. Na kama ukiwaambia kwamba semeni kama mnajua kuwa Mtume[saw] wa Mungu Alimwita jina gani yule mtu aliyedai kuwa yuatoka kwa Mungu naye ndiye Masihi na amekuja katika zama za michafuko ya msalaba na akauvunja msalaba vipande vipande, ambaye mfano wake haupatikani katika zama zilizopita wala hautarajiwi katika zama zijazo, kwa yakini watasema huyu ameitwa Masihi na Mwana wa Mariamu kwa ulimi wa Mtume[saw] wa Mungu, na imebainishwa kwamba atakuwa kutoka katika umati huu. Sema, sifa zote njema ni za Mungu kwani Ameidhihirisha haki, lakini watu wengi hawatambui.

Enyi watu, uangalieni ukamilifu wa siku za upotevu, na msizikane siku za Mungu Mwenye jalali ikiwa m wachamungu. Je hamkushuhudia kupatwa kwa jua na

mwezi katika Ramadhani, mbona hamfuati mwongozi? Je hamkuona jinsi ilivyoenea tauni na matui yamekithiri? Basi, ile na hii ndio ushahidi kutoka kwa mbingu na ardhi kama manabii walivyohabarisha. Na yamejumuika yote yaliyotajwa ndani ya Kurani kuhusiana na alama za zama za mwisho. Mbona hamzinduki! Na ilipokwisha thibitika kwamba zama zimeishafika mwisho wake, basi yuko wapi Khalifa wa zama za mwisho, semeni mkijua. Enyi mkanao, amininі au msiamini, kwa yakini waliojaaliwa elimu ya Kitabu na hadhi katika wema, hao wananipokea nao hawakawii. Na wazionapo alama zilizotajwa ndani ya Kurani na huku Khalifa anawaita kwenye Rahmani, huangukia nyuso kusujudu, na hujuta juu ya makosa yao. Na utaona macho yao yanachuruzika machozi kwa sababu ya haki waliyoitambua, na utulivu unashukia nyoyo zao, na wanayaamini Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, nao hulia wakisema: Mola wetu, tumemsikia mwitaji, nasi tumemtambua mwongozi, basi na tughofirie dhambi zetu, sisi tunatubu. Na Mwenyezi Mungu Anasema: Hakuna lawama juu yenu, dhambi zenu zitasamehewa na mtaingia katika wale waheshimikao. Enyi jamii ya wenye akili, msingojee kwamba mtu yeyote atashuka toka mbingu; tambueni kuwa hii hii ndiyo siku yenu mliyokuwa mwaahidiwa. Mwenyezi Mungu Aliwaahidi walioamini miongoni mwenu kwamba Atawafanya makhalifa mfano wa makhalifa wa sheria ya Musa[as]. Hivyo, ikawajibika kuwa aje Khalifa wa mwisho juu ya

nyayo za Isa[as], naye awe miongoni mwa umati huu. Nanyi mwasoma Kurani, je hamuelewi? Ni ahadi ya Mungu, na msiidhani ahadi ya Mungu kama adhadi za watu waongo. Na ahadi ya Mungu itatimiaje pasipo kudhihiri Masihi kutoka miongoni mwenu. Imekuwaje, mbona hamtafakari katika aya za Mwenyezi Mungu na hamzingatii! Je yaipasa shani ya Mungu kuwaahidi kwamba Atainua kutoka miongoni mwenu makhalifa mfano wa wale waliopita kabla, kisha kuisahau ahadi yake na kumteremsha Isa[as] toka mbinguni? Ameepukana na Ametukuka na mnayozusha. Mmekuwaje, mwabishana kumhusu Masihi Mau'udi na mwakazania kuwa huyo ndiye Masihi bin Mariamu, nanyi mwasoma Kitabu cha Mungu kisha mnaghafilika. Hakika Mwenyezi Mungu Ameishahukumu baina yenu na baina yetu na Akafafanua ishara kwa watu wamchao Mungu. Yeye Alinuia kuwahami walioamini na kuzuia fitina za msalaba; je hampendi? Ni desturi yake kwamba Anatuma waja wake wakati wa mafuriko ya fitina; basi waulizeni wale wajuao kama mnashuku. Je mwatamani kuwa aje Masihi toka mbinguni sawa na dhana yenu, ilhali imeisha pita suna ya Mwenyezi Mungu hapo kabla. Je hamwelewi? Na hakuna mtume yeyote aliyekuja kwa njia waliyofikiria wadhanio, basi imekuwaje nyinyi mwatarajia aje sawa na dhana yenu! Kabla yenu Wayahudi nao wakadhani kwamba Masihi wao hatatokea ila baada ya kushuka Nabii fulani toka mbinguni, lakini Mwenyezi Mungu Hakusadikisha

dhana yao, hivyo wakamkataa Ibni Mariamu[as]; na sasa pia wanahasimiana. Kadhalika wakadhani kwa mithili ya Musa[as] atatokana na Wana wa Israeli, na alipoinuliwa toka katika wana wa Ismaeli [as], wakamkufuru na hadi leo hii hawaamini. Basi, hii ni suna ya Mwenyezi Mungu kwamba Anadhihirisha baadhi ya sehemu za utabiri na Anaficha baadhi nyingine. Hivyo, wale ambao mioyoni mwao mna upotofu, wanazifanya zilizofichika kuwa tegemeo la kukataa kwao, nao wanakengeuka zile zilizodhihiri, na hawatafakari, huenda huu ndio mtihani kwao. Ipo mifano mingi, lakini hawasomi.

Msishike njia isiyokuwa ya Kurani, Enyi wenye busara! Wala msiseme kwamba Isa[as] atashuka toka mbinguni. Jizuieni, itakuwa bora kwenu, Enyi Waislamu! Ninyi mmeshika itikadi isiyo na mfano wake ndani ya Manabii. Nasi tumeshika itikadi iliyo na mifano mingi katika Mitume na wateule. Basi ni kundi lipi katika mawili linalostahiki zaidi kuwa na amani na karibu zaidi na ukweli na uhalisi, Enyi wenye akili! Haikutokea hapo kabla kwamba nabii yeyote akashuka toka mbinguni; imekuwaje mwatarajia hii sasa? Wayahudi walioamini kama nyie kwamba nabii Ilyasa — Eliya — atashuka toka mbinguni kabla ya Masihi, nao walikuwa wanaing'ang'ania hiyo. Na alipokuja Masihi wakakadhibisha na wakasema: Tumkubalije ilhali Ilyasa[as] hajashuka, na Masihi wa kweli hatakuja isipokuwa baada ya ushukaji wake, nasi twamngojea. Lakini Isa[as] akapinga waliyodhania na akasema kwamba Yahya[as] — Yohana

Mbatizaji — aliyetumwa kabla yangu ndiye Ilyasa, ikiwa mnakubali. Lakini hawakukubali na wakamkufuru Isa bin Mariamu[as], Mtume wa Mungu. Hivyo, Mungu Akawaghadhibikia na kuwalaani na kuwateremshia tauni kwa sababu ya kukufuru kwao. Juu ya hayo, mliifuata itikadi yao kwa kusema kwamba Masihi atateremka toka mbinguni. Je Wayahudi waliwausieni ama zimefanana nyoyo na macho, hivyo matamanio yenu yakawa kama matamanio yao, na ni karibu kwamba muadhibiwe kama walivyoadhibiwa hao. Basi Mcheni Mungu na msizifuate suna za walioghadhibikiwa isije mkaadhibiwa na hali mwaisoma Sura Al-Faatiha; je hamtambui kwamba Mungu Akawaita Wayahudi hao kuwa 'walioghadibikiwa', na Akawatahadharisheni ndani ya Ummul Kitab — Sura Al-Faatiha — isije mkawa kama mithili yao na Akawakumbusheni kuwa walihilikishwa kwa tauni. Basi, mmekuwaje mwasahau hukumu za Mungu na hammwogopi Mola wenu wala hamtahadhari. Wala hamzingatii kauli ya Mwenyezi Mungu *Ghairil maghdhubi 'alaihim* — siyo ya wale waliokasirikiwa — na Hakusema *Ghairil Yahudi,* yaani siyo ya Wayahudi, kwani ndani mwake Ameashiria kwenye adhabu iliyowasibu na pia adhabu na alama zake zimedhihirika; ndani yake mna ishara kwa watu wanaotafakari. Mwenyezi Mungu Akawakasirikia Wayahudi kwa kauli yao kwamba waliyeahidiwa atateremka toka mbinguni kisha atakuja Masihi, hapo Mungu akasema kwa ulimi wa Isa[as] kwamba hao ndio

watu waongo. Mmekuwaje mnatarajia jambo Alilolibatilisha Mwenyezi Mungu hapo kabla, na mwaminio haumwi mara mbili katika shimo moja na anapata ibra kutokana na wengine ili wasimlaumu wenye kulaumu. Je mwakamilisha kushabihiana huku kwa ndimi zenu na mbalagha wenu kuhusikana na itikadi ya ushukaji, ilhai mwajua kwamba Masihi amepinga rai hii. Mmekuwaje mnampenda lakini mnaiasi hukumu yake na mnahitilafiana naye. Na tauni ipo karibu na nyumba yenu, na nafsi yoyote haijui itafanyiwa nini mwakani. Hivyo, msikufuru sana na tubuni kwa Mungu Ambaye mtarejea kwake. Na mwatambua kuwa hii ndio tauni iliyowashukia Wayahudi, kisha itawashukia wale wanaofanana nao ikiwa ni ghadhabu toka kwa Mwenyezi Mungu. Na hii ndiyo siri ndani mwa aya *Ghairil maghdhubi 'alaihim*, Enyi mnaotafakari! Ni sikitiko kwa watu kwamba wanaziona ishara za Mungu na siku zake, kisha waenda upande. Na waambiwapo aminini ile Aliyoiahidi ndani ya Sura An-Nuur na Sura Al-Faatiha, husema je tuamini walivyoamini majahili? Habedari! wao wenyewe ndio majahili lakini hawatambui. Na waambiwapo Mcheni Mungu na msiyafuate matamanio yenu, husema, sisi ndio wacha Mungu, ilhali wamiacha Kurani kidhuluma na kikiburi. Na waitwapo kwenye haki, hughadhibika. Na ni ujahili gani mkubwa zaidi kuliko jambo hili kwamba wamekubali kauli tofauti mbali mbali lakini hawaiamini ahadi ya Kurani, ilhali hii ni Kitabu

ambacho haitafikia batili mbele yake wala nyuma yake. Na je yakini na dhana zaweza kuwa sawa? Kwa hakika Hadithi zote zimekusanywa baada ya miaka mia au mia mbili, na madhehebu ya Islam yanazozana kuhusiana nazo. Ama Kurani, basi hakuna shaka ndani yake, na hii hii ndiyo iliyomteremkia Nabii[saw] wetu kwa kweli na uadilifu, na imetoka kinywai mwake; je mna shaka ndani yake? Basi, hadithi gani mtaiamini baada yake? Je mwaitanguliza dhana juu ya ile ambayo katika shani yake Mwenyezi Mungu Alisema: 'Hakika Sisi Tumeteremsha mauidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao.' Pia husema kuwa sisi tumewakuta baba zetu juu ya njia moja nasi tutafuata nyayo zao. Tazama jinsi wanavyokiri kuiacha Kurani, kisha tazama jinsi wazozanavyo. Na husema kwamba Hadithi zaafikiana na yale tunayoitakadi; nao wanaongopa tu. Wamejua kuwa Hadithi nyingi za Nabii[saw] zaafikiana na Kurani, na ile isiyowiana nayo, hiyo wameizusha wazushi. Kulindwa ni katika sifa maalum za Kurani, na matukio hayatenguki kama mnavyokiri. Hivyo, mtakimbilia wapi toka kwenye haki iliyobainika na mpaka lini mtabishana? Niambieni kwamba kama nimetoka kwa Mwenyezi Mungu na mmenikadhibisha, mtakuwa na hali gani, Enyi mnaokadhibisa! Na Mwenyezi Mungu Amehabarisha ndani ya Sura Al-Maaida kifo cha Masihi na Hadithi imetuambia kuwa umri wake ulikuwa ni miaka mia na ishirini. Na Mwenyezi Mungu Ametutolea bishara katika Sura An-Nuur kwamba Makhalifa watakuwa toka

katika umati huu. Basi, Khatamul Khulafaa alikuwa hana budi kutokea toka ndani ya Waislamu, naye ndiye Masihi Mau'udi pasipo shaka na wasiwasi. Hivyo, Mwenyezi Mungu Amekwisha amua baina yetu na baina yenu kama mnayo macho. Je baada ya haya imebaki shaka yoyote kwa watu wamchao Mungu? Tumejaaliwa toka kwa Mwenyezi Mungu hoja ikomeshayo, na mikononi mwenu hamna kitu isipokuwa kilichozushwa na wenye hatia. Na wakasema kuwa Masihi atateremka upande wa mashariki wa Dimashki — Damascus — na hii ndiyo haki kama mkitafakari. Kweli Masihi amedhihiri katika mashariki ya ardhi, kama alivyodhihiri Dajali huko. Hivyo, Masihi pia akwa katika mashariki na Dajali pia ndani ya mashariki na washirikina wakazidi katika ushirikina. Na kijiji changu kipo upande wa mashariki toka Damascus; basi muulizeni aijuaye kama nyinyi hamjui. Na nchi hii ya India ipo upande wa mashariki toka Hijaz, basi ikatimia aliyoashiria Nabii[saw] upande wa mashariki kuhusiana na Dajali na Masihi. Hivyo, ikatimia ahadi ya Mungu kwa kweli na haki, basi Enyi wenye papara, msipigane na Mungu. Mwashuhudia wenyewe jinsi watu wanavyotanasari na kuritadi dini ya Mungu, na bado mwatongoa kuwa hakuja mtume toka kwa Mwenyezi Mungu. Mmekuwaje, mnahukumuje! Na nchi hii imeipita ardhi nzima katika fitina zake. Je mwajua nchi yoyote  mfano wake; basi tuonyesheni ile nchi kama m wakweli. Hakika mbingu, ardhi, zama na mahali vimetoa ushahidi juu ya ukweli wangu, na

imeishapita karibu sehemu ya tano ya karne hii. Basi, ushahidi gani baada ya hayo utawazindueni. Mwenyezi Mungu Ameishaonyehsa ishara zipatazo mia tatu, na wameziona mashahidi ambao takriban laki moja bali wanazidi. Na kama mkidhani kwamba hao wameongopa, basi waleteni mashahidi waongo mfano wao ambao watoe ushahidi kwa ajili yenu ikiwa m wakweli katika madai yenu. Bila shaka msaada wa Mungu umewafikieni katika wakati wake, je mwaukatalia mbali? Mkijaribu kuhesabu dalili za ukweli wangu, hamtaweza kuzihesabu; na waongo hawapatiwi ishara wala hawasaidiwi. Kwa hakika Sura Al-Faatha yatosha kwa mwenye bahati nejma atafutaye haki na hapiti meble yetu kama wale watakabario. Kwani Mwenyezi Mungu Ametaja humo makundi matatu ya watu waliopita hapo kabla, nao ndio: walioneemeshwa, walioghadhibikiwa na waliopotea. Kisha Akaufanya umati huu kuwa kundi la nne, na Sura Al-Faatiha imeashiria kwenye jambo hili kwamba hawa watawarithi watu wa makundi hayo matatu. Ama watakuwa miongoni mwa walioneemeshwa, au miongoni mwa walioghadhibikiwa au waliopotea na wakatanasari. Na Akaamuru kwamba Waisalmu wamuombe Mola wao Awajaalie kuwa miongoni mwa kundi la kwanza na Asiwafanya toka miongoni mwa walioghadhibikiwa wala katika waliopotea wanaomwabudu Isa[as] na wamemshirikisha Mola wao. Kuna matabiri matatu ndani mwake kwa watu wamaizio. Na ulipowadia wakati

wa matabiri haya, Mwenyezi Mungu Akaanzia na 'waliopotea' kama mnavyoshuhudia. Hivyo Manasara wakajitokeza toka nyumba yao ya watawa kwa nguvu, hakuna nguvu iliyo sawa nayo, nao toka kila mahali pa juu waja mbiombio. Na ardhi ikatetemeka sana na ikatoa mizigo yake, na watu wengi sana miongoni mwa Waislamu wakatanasari jinsi mnavyoshuhudia. Kisha ukafika wakti wa utabiri wa pili, namaanisha wakati wa kujitokeza kwa walioghadhibikiwa kama ilivyokuwa ahadi ya Mola. Basi, kundi moja la Waislamu likawa na sera ya Wayahudi walioghadhibikiwa na Mungu; matamanio yao yakawa kama matamanio yao na rai zao kama rai zao, kisingizio chao kama kisingizio chao, uadui wao kama uadui wao, ukanusho wao kama ukanusho walo. Nao wanaongopa na wanafanya ufasiki na dhuluma na kiburi, na wanapenda kumwaga damu pasipo haki. Nafsi zao zimejaa tamaa, uchoyo na husuda. Ikapigwa juu yao dhila, hivyo hawaheshimiki mbinguni wala ardhini, na wanafukuzwa toka kila mlango. Kadhalika ardhi imejaa dhuluma na ukandamizaji, na watu wema wamepungua. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akaianglia ardhi na kuikuta watu wake wamo ndani ya giza la aina tatu: giza la ujahili, giza la ufasiki na giza la waitao kwenye Utatu na kwenye shetani atiaye wasiwasi nyoyoni aendaye kisirisiri kwa hila. Basi Akakumbuka, kwa fadhili na rehema, ahadi yake ya tatu ambayo walikuwa wanaomba waombeao, basi Yeye Akauneemesha umati huu kwa kutuma mithili

ya Isa; hakuna aikanaye ila vipofu. Na wale wanaoyaamini matabiri ya Kurani na ahadi zake na wakakataa yaliyo dhidi yake, hawa ndio waaminio kweli. Nao ndio Aliowaongoza Mwenyezi Mungu nyoyo zao, na hawa ndio walioongoka.

Hakuna Nabii wetu isipokuwa Muhammad[saw], na Kitabu chetu ila Kurani, hivyo tafuteni mwongozo ndani yake, Enyi watafutao mwongozo! Nasi tumefundishwa dua ndani ya Sura Al-Faatiha, na Mwenyezi Mungu Akakubali dua hii ndani ya Sura An-Nuur. Basi, mmekuwaje mnakiacha kiini cha Kurani na mnatosheka na ganda. Ahadi za Kurani hazikufichika bali zinabainika, ziko wazi kwa watu wafahamuo. Mmekuwaje mwakataa neema za Mungu baada ya kushuka hizi? Je m wanyama au watu wenye akili? Na Mwenyezi Mungu Hakutuelezea ndani ya Sura Al-Faatiha makundi matatu isipokuwa kuashiria kwamba umati huu utawarithi katika kila namna miongoni mwa namna zilizotajwa. Basi urithi huu umedhihiri kitimilifu ndani ya Waislamu wa zama zetu ambazo ni zama za mwisho, ambao kila nafsi inautambua pasipo kuhitaji kutafakari sana, kwani jambo hili halifichiki kwa wale wanaowatazama Waislamu wa zama zetu hizi na yale wayatendayo. Na kwa kila kundi la warithi hawa wa aina tatu kuna daraja tatu. Ama wale waliowarithi walioneemeshwa, basi miongoni mwao kuna watu wasiopata hisa yao ya neema isipokuwa kidogo katika itikadi au hukumu, nao wanatosheka kwayo. Na kati yao

kuna wenye hali ya wasitani, hawa wamesimama kwenye daraja ya wasitani na hawakufikia ukamilifu wa daraja. Na kati yao kuna mmoja ambaye Mola wake Akamteua na kumkamilisha na kumfanya mtangulizi katika mema. Yeye Humchagua Amtakaye na kumfanya mahususi kwa daraja za juu. Basi huyo mtu mahususi ndiye Masihi Mau'udi aliyedhihiri baina ya kaumu nao hawajui. Na ama wale walowarithi waliokasirikiwa, yaani Wayahudi, basi kati yao kuna watu Waislamu walioshabihiana nao katika kuziacha faradhi na mipaka, hawafungi wala hawasali, wala hawakumbuki mauti wala hawajali. Miongoni mwao kuna watu walioshika dunia kuwa mwabudiwa wao na wanafanya kazi kwa ajili yake usiku na mchana. Kati yao wapo waliowapita wengine katika maovu, na hawa ndio wanaowadhihaki wenye haki na wanawacheka na wanawafanyia uadui na kuwakufurisha na kuwatukana, na wanafanya matendo kwa kujionyesha kwa watu na kwa kuringa, nao hawana ikhlasi. Hawa wanamshambulia Masihi wa Mungu na kundi lake na kuwavuta kwa mahakimu na wanakalia kila njia na husema: 'Waueni, kwani wa makafiri.' Na waambiwapo njooni kwenye Neno la Mungu mkalifanye kuwa mwamuzi baina yetu na baina yenu, utaona macho yao yawa mekundu kwa ghaidhi na hupita wakitukana na kuhamaki. Na ni ishara ngapi za Mwenyezi Mungu walizoziona kwa macho yao kisha wanapita wakitakabari kana kwamba hawaoni. Wakatupa Kitabu cha Mungu nyuma ya migongo yao kwa dhuluma na

kiburi, na husema msizisikilize dalili zake na zipigieni makelele, huenda mtashinda.

Ama wale walowarithi 'walopotea', miongoni mwao kuna watu waipendao mienendo ya Manasara na sera zao na kuelekea kwazo. Utawakuta wanapenda mavazi yao na mashati yao, kofia zao, na mabuti yao, mtindo wa maisha yao na mazoea yao yote, nao huwacheka wanaofanya kinyume cha hayo. Wanawaoa wanawake kutoka miongoni mwa watu hao nao wanawaashiki. Na kati yao kuna watu waliovutika kwenye falsafa ya Manasara waliyoieneza, na wanaghafilikia mambo ya dini. Na maneno mangapi yanatoka vinywani mwao yasiyofaa na wanahakirisha dini ya Mungu na hawaijali. Na miongoni mwao kuna watu waliokamilisha upotevu wao nao wakauacha Uislamu na kuufanyia uadui kwa sababu ya ujahili wao, na wakatunga vitabu dhidi ya Islam, wakamshutumu Mtume[saw] wa Mungu na kuishambulia heshima yake. Na watu wa aina hii ni wengi sana nchini humu waliokuwa Waislamu mwanzoni. Basi yakatimia yaliyokuwa yameashiriwa ndani ya Sura Al-Faatiha. *Inna lillahi wa innaa ilaihi rajiuun*.

Na utabiri wa kwanza kati ya matabiri ya Ummul Kitab — Sura Al-Faatiha — uliodhihiri ndio Waislamu kutanasari na kutukana kwao na kushamulia kwao kama mbwa jinsi mnavyoshuhudia. Kisha ukadhihiri utabiri kuhusu 'walioghadhibikiwa'. Basi, utaliona jinsi kundi la

maulamaa na waliowafuata wapendao dunia na matajiri na madarweshi wanavyotakabari na hawajinyenyekezi; wanajionyesha kwa watu na hawana ikhlasi, na wananena wasiyoyatenda, na wakagandama kwenye ardhi na hawaelekei kwa Mungu, wala hawaziamini siku za Mungu, na wanaziona ishara za Mungu kisha wanazikataa. Wanataka kuifukia haki ndani ya ardhi na kurarua vazi lake kama mbwa, na hawatafakari kuhusu usiku wao wala mchana wao kwamba wataulizwa. Kama wangeweza kuniua, wangeniua tu. Na kama wangefanya njama ya siri kuniua wangeniua ghafula. Lakini Mwenyezi Mungu Hakuwafaulisha katika wanayokusudia. Wanafanya kila hila kwa kunihilikisha, lakini lashuka jambo toka mbinguni na kuifanya hila yao kupotea mavumbini, wasitambue. Pamoja nami Yupo Mweza Ambaye wahifadhi wake hawaondoki makazi yangu, wala rehema yake haiendi mbali nami hata kwa kitambo cha kupepesa macho, lakini wapinzani hawaoni. Bali, wananiona na wanakunja kipaji na kunitusi na kunitukana, na wanakula kiapo juu ya kiapo kuwa mimi ni mwongo. Hakuna siri iliyobakia isipokuwa imetoboleka, wala kadhia ila imeamuliwa. Na yatadhihri yaliyomo ndani ya moyo wangu na yale yaliyomo moyoni mwao na hayatabaki kufichika wanayoficha. Haya ndiyo makundi mawili ya walioghadhibikiwa na wenye msalaba. Mwenyezi Mungu Aliyataja ndani ya Sura Al-Faatiha na Akaashiria kwamba haya mawili yatakithiri katika zama za mwisho

na yatafikia kilele cha ufisadi wao. Kisha Mola wa mbingu Ataimarisha kundi la tatu katika zama za mwisho ili kukamilika kufanana na umati wa awali ili kwamba sisila mbili zilandane. Basi zama hizo ndio zama hizi hizi, na yametimia yote Aliyoahidi Rahmani. Na mmewaona Waislamu waliotanasari nao ndio wengi. Nanyi mmewaona Wayahudi wa umati huu na mienendo yao. Na nafasi ya tofali moja ilikuwa wazi katika jengo hili — namaanisha wale walioneemeshwa. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akataka kutimiza utabiri na kukamilisha jengo kwa kulijenga tofali la mwisho. Na mimi ndimi hilo tofali, Enyi watazamao! Isa[as] alikuwa ni ishara kwa wana wa Israeli, nami ni ishara kwenu, Enyi mpitao kiasi! Harakieni kutubua, Enyi mlioghafilika! Mimi nimefanywa kuwa mja aliyekamilika kabisa miongoni mwa walioneemeshwa katika zama za mwisho. Siyo fahari wala kujionyesha kwa watu, bali Mwenyezi Mungu Akafanya Alivyotaka na kupenda. Basi, je mtapigana na Mungu na mtakinzana. Mimi ndimi Masihi Mau'udi aliyekadiriwa ujaji wake katika zama za mwisho kutoka kwa Mungu, Mwenye hekima, Mwenye nguvu. Na mimi ndiye niliyeneemeshwa ambaye aliashiriwa katika Sura Al-Faatiha ujaji wake wakati wa kudhihiri makundi hayo mawili yaliyotajwa, na kutapakaa bidaa na fitina. Je mtakubali? Na kunikana kutasababisha majuto kwa watakaonikufuru. Na kwa hakika kunikubali kuna baraka kwa wanaoiacha husuda na wanaamimi. Na lau kama jambo hili na kazi hii

ingekuwa toka kwa minghari ya Mungu, Angeivunjilia mbali fika na kutujumuishia laana ya ardhi na laana ya mbingu, na Mungu Angewafaulisha maadui zangu kwa yote wayatakayo. Hapana, bali hii ilikuwa ni ahadi toka kwa Mungu nayo imetimia kwa ukweli na haki, na hii ndiyo habari njema kwa wale waliokuwa wanaingojea. Kadhia yetu imepelekwa kwa Mwenyezi Mungu, na karibuni kundi letu au kundi lenu litapata ushindi au ushinde. Basi, kimuhtasari ni kwamba Sura Al-Faatiha imebainisha kuwa umati huu ndio umati bora ambao unacho kipawa cha kupata maendeleo sana, huenda baadhi yao kuwa kama Nabii miongoni mwa manabii; na pia unao uwezo wa kuanguka hadi baadhi yao wakawa kama Wayahudi waliolaaniwa kama manyani wa porini, au wataingia katika waliopotea na kutanasari. Yakutosha dua hii uisomayo ndani ya sala zako tano ikiwa u miongoni mwa wale waitafutao haki na kuharikia Kwake. Hivyo, imethibitika kutokana na hayo kwamba wawepo ndani mwenu walioghadhibikiwa, na wawepo kati yenu waliopotea kwa kutanasari. Basi yawezekanaje kwamba Masihi Mau'udi asiwe kutoka miongoni mwenu ambaye ameashiriwa yeye na Jumuiya yake katika kauli yake: *an'amta 'alaihim*.[17] Basi msitofautishe baina ya makundi matatu ambayo nyinyi mwayarithi. Hatawajieni Myahudi kutoka wana wa Israeli, wala hatakuja Nabii toka mbinguni; haya ni

[17] Sura Al-Faatiha 1:7

majina ya umati huu huu ikiwa mwaelewa. Je, mnastaajabia kwamba Mwenyezi Mungu Awaite baadhi yenu kuwa Myahudi, na baadhi yenu Nasara na baadhi yenu Isa? Basi, msilikadhibishe Neno la Mungu na mtafakari katika Aliyoashiria, na mzingatie ipasavyo, Enyi wakosefu! Au mwatongoa: 'Hatuoni haja ya Masihi wala Mahdi, na Kurani inatutosha, nasi tumeishaongoka', ilhali wanaelewa kwamba Kurani ni Kitabu asichoweza kukigusa kiini chake isipokuwa waliotakaswa. Basi, ilisikika haja ya mwenye kufasili aliyetakaswa kwa mikono ya Mwenyezi Mungu na akaingizwa katika wale wenye busara. Ole wenu, mwakikataaje Kitabu cha Mungu na mwaukufuru utabiri wake! Je imani yenu inawaamuruni kukufuru matabiri ya Mungu? Semeni ikiwa m waaminio. Na kabla yenu imepita kaumu waliodhani kuhusiana na mitume wao jinsi mdhanivyo. Wakafikisha ukadhibishaji na dharau mpaka mwisho wake nao wakapita mipaka, hapo waliotumwa wakaangukia kwenye kizingiti cha Mola wao, basi wakashindwa waliozuia njia ya Mungu wala hawakukoma. Hivyo, Enyi wajasiri, zicheni suna za Mwenyezi Mungu na ghadhabu yake. Nyinyi mmemwacha Mungu basi na Yeye pia Amekuacheni, mmetenda kitendo cha Wayahudi na mmezifuata rai zao, na Mwenyezi Mungu Akawaonjesha Wayahudi malipo yao. Basi, tubuni kwa Mwumba wenu na njooni kwa niwaambiayo. Kama Alivyowaumbeni kwanza ndivyo mtarudi. Na mkiweza, fikisheni habari hii kwa

wafalme wenu na kuweni wasaidizi wa Mungu ili mpate kurehemiwa. Na hakuna kadhia yoyote wanayokazania watu wa ardhi isipokuwa hatimaye yaamuliwa mbinguni. Hii ni suna ya Mungu isiyobadilika, Enyi wadhalimu! Haimpasi Mwenyezi Mungu kuitelekeza haki na wenye haki mpaka apambanue mbaya katika mwema. Basi mmekuwaje hamwoni? Na kama nikiwa mwongo, basi uongo wangu ni juu yangu; na kama nikiwa mkweli, basi naogopa kwamba adhabu toka kwa Mungu itawasibuni; na ni hakika kuwa wapitao kiasi hawapati kufaulu. Tubuni, tubuni, kwani balaa lipo mlangoni kwenu, na harakieni kwenye Mungu wenu Apokeaye toba. Punguzeni kidogo kupiga fahari, na mhudhurie mbele ya Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu. Je mauti hayako karibu? Na adhabu ya Akhera ni jambo la kutisha; na hamna nafasi ya kujirekebisha baada ya kufa wala hamtarejea hapa tena. Na Mola wangu Alinifunulia wahyi kabla haijashuka tauni kuwa: 'Uunde safina mbele ya macho Yetu na sawa na Wahyi Wetu, na usinizungumze juu ya wale waliodhulumu, kwa yakini wao watazamishwa. Wanaofanya baiati yako, kwa hakika wanafanya baiati ya Mwenyezi Mungu, Mkono wa Mungu uko juu mikono yao'. Miaka imepita tangu nilipoeneza wahyi huu, na wanaoujua wapenzi na maadui. Na Mwenyezi Mungu Anaifikia ardhi Akiipunguza mipaka yake. Basi, tubuni kwa Mwenyezi Mungu, Enyi mlioghafilika. Na msinyanganye haki za Mungu na za watumishi wake, wala msiwe miongoni

mwa wanaodhulumu, na tubuni kwa Mungu toba iliyohalisika ili mpate kurehemiwa. Na Mola wangu Akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nafsini mwao. Kwa yakini Amekichukua kijiji hiki katika hifadhi yake." Yaani atakayeingia ndani yake atakuwa na amani. Mimi nachelea kwa wale wasiomwogopa Mungu wala hawaachi mabaya yao. Hivyo, inukeni toka katika mahali penu mkinyenyekea na sujuduni mkitubu, muwe wenye kujinasihi nafsi zenu na mtafakari mkitetemeka, wala musiwe kama mafasiki na wadhihakio. Bila shaka kuwakataa waliotumwa na Mungu ni jambo zito. Na yule aliyepigana nao vita, huyo amejitupa katika jahanamu. Basi, Enyi wapiganao, hamna heri yoyote katika vita. Nanyi mwasoma ndani ya Sura Al-Faatiha habari za watu Aliowakasirikia Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kumkufuru Masihi Isa bin Mariamu[as]; wakamkufurisha na kumwudhi na kumhakirisha, wakamkamatisha na kunuia kumuua msalabani ili watu wadhani kuwa yu mwenye bahati mbaya na maluuni. Basi tafakarini ndani ya Ummul Kitab — Sura Al-Faatiha — ipasavyo kutafakari kwamba kwa nini Mwenyezi Mungu Akawatahadharisheni kughadhibi-kiwa. Mmekuwaje, hamzingatii? Basi, jueni kuwa siri iliyomo ndani yake ni kwamba Mwenyezi Mungu Alikuwa na elimu kuwa atatokea miongoni mwenu Masihi wa pili, kana kwamba ndiye huyo hasa; na Akajua kuwa kundi moja toka miongoni mwenu

litamkufurisha na kumkadhibisha na kumhakirisha na kumtusi, na watataka kumwua na watamlaani. Hivyo, Yeye Akawafundisheni dua hii kwa kuwahurumia na kuashiria kwenye habari Aliyokadiria. Basi, ameishawajieni Masihi wenu. Na kama hamtajizuia kudhulumu, basi mtaulizwa. Na imehakikika katika sehemu hii kuwa muradi wa 'waliokasirikiwa' mbele ya Mungu Mjuzi[18] ndio Wayahudi waliokosa kuhusu habari ya Isa[as], Mtume wa Mungu Rahmani, na wakamkufurisha na kumuudhi, na wakalaaniwa kwa ulimi wake ndani ya Kurani, na kadhalika wale miongoni mwenu waliofanana nao katika kumkufurisha Masihi wa zama za mwisho na kumkadhibisha na kumuudhi kwa uilmi na kwa kutamani kumuua walau kwa masingizio kama mnavyofanya. Na muradi wa kauli yake 'waliopotea' ni Manasara waliopita mipaka kuhusiana na Isa[as] na kumsifu kupita kiasi na kusema kwamba hakika Mungu ndiye Masihi naye ndiye mmoja katika watatu, yaani ndiye mmojawapo aliyepo ndani ya watatu, jinsi waaminivyo. Na muradi wa kauli yake

---

[18] Hakika neno 'waliokasirikiwa' limekabiliana na neno 'waliopotea'. Namaanisha hili lipo kwenye mkabala wa lile, kama isivyofichika kwa watazamao. Basi ikathibitika kabisa na kwa yakini kuwa waliokasirikiwa ndio wale waliokosa kuhusikana na Isa[as] kwa kumkufurisha na kumsumbua na kumhakirisha, jinsi 'waliopotea' waliovyopita kiasi kuhusiana naye kwa kumchukua kuwa Mola wa walimwengu. Mwandishi.

'Uliowaneemesha' ndio manabii na waja wema miongoni mwa Wana wa Israeli waliomsadikisha Masihi na hawakupunguza au kuzidisha kwa kauli mbalimbali kuhusiana naye. Na kadhalika muradi wake ni Isa Masihi ambaye juu yake silsila hiyo iliishia na Unabii ukahama na kwa sababu yake chemchem ya baraka ikazibwa, kana kwamba yeye akawa ni kizibo, naye alikuwa kama ishara na alama ya Unabii kuhamishwa, au alikuwa ni ufufuo au kiama, kama mjuavyo.

Na kadhalika muradi wa 'Uliowaneemesha' ndani ya aya hii ndiyo silsila ya waja watukufu — *Ma-Abdali* — wa umati huu waliomsadikisha Masihi wa zama za mwisho na kumwamini na kumpokea kwa ukweli wa dhamira na moyo, namaanisha yule Masihi ambaye sisila hii imeishia kwake. Na hili ni kusudio kubwa la kauli Yake 'Uliowaneemesha' kama ulinganifu unavyotaka, na wenye kutafakari hawawezi kukataa. Kwani inapojulikana kabisa kwa yakini na kwa uwazi na kuelezwa bayana kwamba 'walioghadhibikiwa' ndio Wayahudi waliomkufurisha Masihi na kumdhania kuwa maluuni kama karina ya kauli yake 'waliopotea' inavyoongoza kwake, basi utaratibu haunyoki wala mpango wa maneno ya Rahmani hauwi mzuri isipokuwa 'Uliowaneemesha' limaanishe kuwa ni Masihi wa zama za mwisho. Kwani kutia maanani ulinganifu ndio miongoni mwa njia ya Kurani na ni katika mambo ya muhimu ya balagha na ufasaha wa kusema, na hawaikatai habari hii isipokuwa majahili. Basi,

imebainika katika sehemu hii dhahiri shahiri kikamilifu kwamba aliyeomba dua hii ndani ya sala yake au nje ya sala, huyo akamwomba Mola wake kwamba Amuingize ndani ya Jumuiya ya Masihi ambaye watu wake watamkufurisha na kumkadhibisha na kutomridhia na kumhesabu kuwa mbaya zaidi kuliko mahuluku na kumwita dajali na mpagani na mpotevu jinsi Wayahudi maluuni waliovyomwita Isa[as]. Na ilipohakikika hii, basi bainisheni ni nani aliyesimama kati yenu minghairi yangu aliyedai kuwa yu Masihi Mau'udi nanyi mmemkufurisha na kumwita kwa majina hayo na kumjeruhi kwa mishale ya fatuwa. Je mwakadhibisha utabiri mlioutimiza kwa ndimi zenu, Enyi waudhi? Je hamwoni haya kwamba mwamuomba Mola wenu katika Sura Al-Faatiha kwamba Awaingizeni katika Jumuiya yangu, kisha mwakengeuka? Nanyi mlikuwa mwasema, 'Hakuna sala ila kwa kusoma Sura Al-Faatiha,' basi msiwe wa kwanza kuikataa, Enyi wenye kumwamini Mungu Mmoja! Ni ajabu kabisa kwamba mnasoma dua hii ndani ya Sura Al-Faatiha mkifahamu maana zake, katika nyakati tano, kisha mnasahau na kugeuka. Hii siyo ila ni bahati mbaya inayosababisha ghaidhi ya Mola, kwani huku ni kuyapuuza mnayoamuriwa. Nami siwaombi ujira wa niliyowaleteeni, wala sisemi kwamba tupeni mali yenu kwa mikono yenu nikazichukue; bali mimi nawapeni mali; je mtachukua? Enyi fukara, hakuna kitu kilichobakia mikononi mwenu katika dunia na Akhera, hivyo msijidhulumu nafsi zenu ilhali mnajua.

Na kama mnayo shaka kunihusu mimi, nitahinini jinsi mpendavyo, nanyi msisahau suna za Mwenyezi Mungu zinazohusikana na wale wanaotumwa. Na tambueni kuwa mmekanyaga juu ya nyayo za wana wa Israeli, hivyo msipitiwe na yaliyowasibu hao, kama m wenye akili, kwani Mwenyezi Mungu Aliwaghadhabikia mara mbili kama asivyoghadhabika hapo kabla wala baadaye na Akawaita jina 'walioghadhabikiwa', na Akawalaani mara moja kwa ulimi wa Daudi[as] na mara ya pili kwa ulimi wa Isa[as]. Hivyo, ghadhabu kali ikawahusuru mara mbili kama isivyofichika kwa wanaotafakari. Na Akanena Mungu Mwenye Enzi: 'Na Tukawafunulia wana wa Israeli katika Kitabu kuwa bila shaka mtafanya uharibifu katika ardhi mara mbili na kwa yakini mtafanya uasi mkubwa'. Basi, je mwakumbuka? Na ufisadi wa pili uliosababisha ghadhabu ya Mola ulikuwa ni kumkufurisha Masihi na kunuia kumfisha msalabani kama ilivyoashiriwa ndani ya laana mbili zilizotajwa, na vimeafikiana juu yake Vitabu vya Mungu na pia wanahistoria. Basi, wale Aliowaita Mungu 'walioghadhabikiwa' ndani ya Sura Al-Faatiha ndio Wayahudi walomkadhibisha Masihi[as] na wakataka kumuua msalabani, na wanaijua wajuao. Na neno 'waliopotea' ndio karina hasa kwa maana hii hii, na hakuna anayeshuku humu isipokuwa majahili. Kwani, 'waliopotea' ni watu waliopita kiasi kuhusiana na Isa[as]. Hivyo, imethibitika kutokana na haya kwamba 'walioghadhabikiwa' ni watu waliopunguza kuhusu yeye.

Na Enyi watazamaji, majina haya mawili yanakabiliana. Kisha Mungu Akawaogofya kuwa mithii yao isije ikawashukieni ghadhabu kama ilivyowashukia maadui wa Masihi na ikawapata laana yake iliyotajwa ndani ya Kurani. Enyi wakana, ndani mwake mna onyo kwenu. Na Mwenyezi Mungu Amewalazimishieni kusoma Sura Al-Faatiha katika kila rakaa kwa shabaha hii hii, Enyi wenye akili. Hivyo, msitoe udhuru wenu wa uongo, na hoja ya Mungu imekamilika juu yenu, basi mwakimbilia wapi? Na Wayahudi hawakumkufuru Masihi isipokuwa kwa sababu wakamdhania kuwa amehitilafiana na itikadi yao wala hakuja kama walivyokuwa wanatarajia, na kwa kumdhania kuwa hayupo kutoka miongoni mwa wana wa Israeli na kwamba mama yake amehini. Basi Mwenyezi Mungu Akawaghadhabikia na kuwahilikisha watu waletao ufisadi. Basi, kumbukeni Sura Al-Faatiha mnayoisoma katika kila rakaa, na hakuna sala minghairi ya usomaji wa Sura Al-Faatiha. Hivyo bebeni mliyobebeshwa ndani yake, na msiwe kama wale wanaosoma lakini hawatendi. Wala msiikaribie Sura Al-Faatiha na hali hamuitambui, wala msiikaribie na hali hamuiamini. Je mwakidhania kiraa cha Sura Al-Faatiha na usomaji wake ndani ya kila rakaa ni kama kutenda sawa nayo. Ni mabaya mnayodhania. Kwa kweli hamhusiani nayo — Sura Al-Faatiha — hata kidogo , wala hamuamini hata herufi moja katika herufi zake mpaka mumwamini Masihi aliyeinuliwa baina yenu kutoka miongoni mwenu, na Sura An-Nuur imeshuhudia juu yake; basi, je mtaamini? Na msipoiamini wala kutenda

sawa nayo, ghadhabu ya Mungu itawashukieni kama ilivyowashukia Wayahudi kabla yenu. Hivyo, Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye mkimuasi Atawaondoleeni dini na mali na kuwapa hizo watu watakaotii. Na mwatambua Wayahudi waliyofanyiwa baada ya Masihi[as], na wakosefu hawawezi kumshinda yeye. Na Mwenyezi Mungu si Mhitaji kwa walimwengu kama wasijizuie. Nami sikuyasema kutoka kwa nafsi yangu, bali Mwenyezi Mungu Aliye Mola wenu aliyanena. Je hamkusoma: 'Na Aone jinsi mtakavyofanya', na 'Hakika amri Yake Anapotaka chochote hukiambia kuwa, basi kinakuwa', 'Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliomo nafsini mwao'. Nanyi mmebadili hali yenu, hivyo karibuni mtaona matokeo yake. Mnasema: 'Tu Waislamu', na Mwenyezi Mungu Anajua myatendayo, Enyi waringaji! Je haujafika wakati kwamba nyoyo zenu zinyenyekee na mhofie onyo la Mungu, nanyi mmeona siku zilizo kama siku za Wayahudi? Je hamuangalii? Tubuni, tubuni kabla ya kuhilikika. Msimkasirikie mwitaji kwenye Mungu wala msipigane na Mola wenu. Je mwaweza kukataa Aliyotaka Mwenyezi Mungu? Nasi twajua kwamba hamuwezi. Hivyo Mcheni Mwenyezi Mungu na msighafilike na mauti. Na ahadi ya Mungu ni haki, basi mzihofie dhoruba kali, Enyi wamchao Mungu! Yu Mmliki, Humpa ufalme Amtakaye na Humwondolea ufalme Amtakaye. Je hamuangalii kauli ya Mwenyezi Mungu: 'Na Aone jinsi mtakavyotenda'! Mmeambiwa

waliyoambiwa Wayahudi, na mwatambua matokeo ya mambo yao, nanyi si majahili. Ogopeni, ogopeni, na acheni kiburi, na mnyenyekee na msidhulumu. Na Mcheni Mwenyezi Mungu mtakayerejeshwa kwake. Halipo jina lolote huko mbinguni ila jina la waliokuwa wa Mungu pekee. Hivyo, jaribuni kuwa majina yenu yaandikwe huko mbinguni. Na Enyi Waislamu! Msifurahie ganda la Islam. Zimesogea karibu siku za Mungu, naye Atawaondoa mafasiki toka miongoni mwenu na Ataleta watu Atakaowapenda nao watampenda; watamkumbuka, naye Atawakumbuka na kuwatimizia neema zote Alizowaahidieni na hamtaweza kumdhuru kitu, basi mmekuwaje hamuogopi? Kwa hakika mfano wa Nabii[saw] wetu mbele ya Mungu ni kama mfano wa Musa[as]. Na Musa[as] aliwaahidi watu fulani lakini akaitimiza kwa watu wengine. Na Mwenyezi Mungu Akawahilikisha baba zao jangwani, kwani walikuwa watu waasi. Na ndivyo Atakavyowafanyieni, Enyi mpitao kiasi! Na Atawarehemuni, Enyi watu wema! Hivyo, shuluhisheni mambo baina yenu na rekebisheni mliyoharibu, na msikae na wale wanaotakabari. Je mwaweza kumshinda Mola wa mbingu kwa nguvu yenu na kumhadaa kwa ughushi wenu? Sivyo! Bali mwajidhulumu nafsi zenu. Nami sisemi kwenu ninayo elimu na nguvu. ***Subhanallah!*** Mimi siye ila ni mtumishi dhaifu, na Amenijaalia kusema Yule Alieyewajaalia mitume wake kusema. Basi, mnakuwaje hamfahamu? Ama iacheni

Sura Al-Faatiha au tendeni sawa nayo kwa kuona haya mbele ya Mungu kama m wacha Mungu. Je mwaisoma ilhali haipiti kooni mwenu, Enyi wajionyeshao kwa watu! Na walioghadhibikiwa ndio Wayahudi ambao Mwenyezi Mungu Amewatahadharisheni kwamba msifanane nao waliokosa kuhusiana na Isa[as]. Basi, waulizeni wenye kumbukumbu ikiwa nyinyi hamjui. Je mwamngojea Masihi minghairi yangu ambaye asumbuliwe kama mimi, nanyi mumkufurishe na kumkadhibisha na kumtukana kama mimi, na mfanye njama ya kumuua? Unawatosheni mzigo huu mlioubeba kwa kunikufurisha. Hivyo msimtafute Masihi mwingine ili kumkufurisha. Je mwaweza kubeba mizigo miwili, Enyi mpitao mipaka? Nyinyi hamna budi kumkufurisha Masihi wa kweli ili utimie utabiri wa Mungu, nanyi mmeishanikufurisha na imetimia mliyokadiriwa. Hivyo, kama m wenye akili, msitafute kukufurisha kwingine. Utondoti wa sehemu hii ni kwamba Mwenyezi Mungu Amehabarisha kuwahusu baadhi ya Wayahudi ndani ya Sura Al-Faatiha kwamba hao walighadhabikiwa na Mwenyezi Mungu katika zama za Isa[as] bin Siddika, kwani walimkufurisha na kumsumbua na kuchochea fitina ya kila aina, kisha Akaashiria kwenye jambo hili kwamba kundi moja la watu kutoka miongoni mwenu watamkufurisha Masihi wao kama hao na watakamilisha kila jiha ya mshabaha, na watamtenda waliyokuwa wakitenda hao, nanyi mwaisoma aya *Al-maghdhubi 'alaihim,* lakini hamzingatii. Je Mwenyezi Mungu

Aliwafundisheni Sura hii bure kama kukiweka kitu katika mahali pasipokuwa pake, au Ameiandika kwa kukumbusha dhambi mtakayotenda? Mmekuwaje hamzingatii? Mwenyezi Mungu hakuwakasirikia Wayahudi hao isipokuwa kwa sababu walimkufurisha Mtume Wake Isa[as] na kumkadhibisha na kumtusi na walikuwa karibu kumuua kwa husuda na matamanio. Na Mwenyezi Mungu Amewaandikieni kadri yake kwamba mtamtenda Masihi wenu kama waliovyomtenda Masihi wao. Nanyi mmenitenda hivyo hivyo. Basi, Enyi kundi la maadui, je bado yamebakia matamanio yenu ya kumkufurisha na kumkadhibisha na kumwudhi mtu mwingine pia kama milivyonitenda? Ndimi zenu na kalamu zenu na njama zenu zimeshuhudia kwamba nyie mmetimiza yaliyoashiriwa katika Sura Al-Faatiha. Hivyo, mhurumieni Masihi mwingine, Enyi mnaomngojea, na msameheni kumpa 'heshima' kama hii. Je hamjashiba kwa kiasi hicho? Je mwapenda ateremke Isa[as] bin Mariamu toka mbinguni kisha mumtende jinsi Wayahudi walivyomtenda hapo kabla, na ijumuike kwake misiba miwili, kukufurishwa kuwili na dhila mbili na aonje laana mara mbili, bali mara tatu.[19] Na Mwenyezi Mungu katu hatamjumuishia

[19] Imethibitika kutokana na maana ya kauli yake *Ghairil maghdhubi 'alaihim* kwamba imekadiriwa kwa Masihi Mau'udi kuwa watamlaani wale watakaosema sisi ni Waislamu ambao Mungu aliwaghadhibikia kama Alivyowaghadhibikia Wayahudi, nao wasitambue. Na kama tukifikiria kuwa Masihi Mau'udi yule ndiye

laana tatu, kama ndiyo dhana yenu. Mmemlaani Masihi mmoja aliyekujieni toka miongoni mwenu na mmeishatimiza yaliyoandikwa ndani ya Kitabu cha Mungu, basi huyu huyu ndiye Masihi Mau'udi kama mkitafakari. Watasema: tutahudhuria mbele yake kwa unyenyekevu na utii, basi tutamkufurishaje na kumwudhi ilhali tutamwamini? Sema: Hii ni takdiri ya Mungu iliyoandikwa kuhusu kundi moja kutoka miongoni mwenu ndani ya Sura Al-Faatiha. Na Enyi majahili, takdiri ya Mungu haibadilishwi. Je Enyi mzifuatao Hadithi, hamsomi sasa Sura Al-Faatiha, nanyi mlikuwa mwaisisitiza sana? Leo Sura Al-Faatiha imekuwa adui yenu nanyi m adui yake na hukumu yake imekuwa adhabu kwa nafsi zenu kana kwamba i funda lisilomezeka, mwataka kulimeza msiweze. Yaelekea hamtaisoma Sura hii sasa isipokuwa mkiumia, wala hamtasoma *Ghairil Maghdhubi 'Alaihim* isipokuwa mtajikasirikia nafsi zenu na mtajuta. Na mtaiona ni adhabu kali kila mara mkiisoma, hapo nyoyo zenu zitaungua kwa moto wa majuto, na mara nyingi mtapenda kuacha kuisoma.

---

aliyeteremshiwa Injili, basi kwa sura hii zitamjumuikia laana tatu: Laana toka kwa Wayahudi, na laana toka kwa Manasara na laana toka kwa Waislamu watakaomkufurisha atakaposhuka na kuwakadhibisha. Basi siri katika kumteremsha Isa[as] ndiyo kukamilisha habari za laana na kuwaingiza Waislamu katika wale wanaolaani. Mwandishi.

## MLANGO WA NNE

Wale wadhanio kuwa Isa[as] amepaa mbinguni, hawanayo hoja, bali wanaongopa. Je Mwenyezi Mungu Ameiandika ndani ya Kurani, ndiyo maana wanaifuata, au Mtume[saw] Akaisema basi nao wanaisema? Siyo, bali wanazusha. Hutaikuta katu hata aya moja kuhusiana na habari hii wala Hadithi ya Nabii[saw] wetu Mtakatifu, wala akili timamu haikubali, Enyi wenye akili. Na husema kuwa Masihi alirufaishwa mpaka mbingu ya pili, na mahali pake mtu mwingine aliuawa msalabani. Utazame uongo wanaozua. Je walihudhuria wakati wa tukio hili? Au wamelikuta ndani ya Kitabu au Suna? Basi watutolee hilo kama wa wakweli. Siyo! Bali wanatunga uongo juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume[saw] wake, na hawaogopi. Wala hawatafakri nyoyoni kuwa akili inakipinga kisa hiki, na hawakisadikishi wenye busara, kwani yule aliyesulubishwa mahali pa Isa[as], kama alikuwa mwaminio basi Mwenyezi Mungu Alimwachaje asulubishwe ilhali Mungu Alisema ndani ya Torati kwamba aliyesulubishwa ndiye aliye maluuni. Je Alimlaani mtu ilhali Alijua kwamba yu mwaminio? Ameepukana na upuuzi na Yu juu kuliko yale wanayomsifa nayo. Na ndani ya Torati Mungu Amemlaani kila aliyesulubishwa; waulize, basi wenye Torati kama u miongoni mwa wasiojua. Na kama aliyesulubishwa alikuwa miongoni mwa maadui wa Isa[as] na alikuwa kati ya makafiri, kwa nini alikaa kimya aliyesulibishwa wakati wa kutundikwa msalabani na

hakuhakikisha kujiondolea lawama, na kwa nini habari zake zikabaki kufichika? Na waliokuwa wanatundikwa msalabani walikuwa hawafi ila hadi siku tatu au zaidi; muda huu ulikuwa wa kutosha. Hivyo, waulize waliomsulubisha adui mmoja miongoni mwa maadui wa Isa[as] kwamba alinyamaaje muda huo wote. Je wenye akili wanaikubali? Je hawakubaki kwa ajili yake mashahidi kama vile mamake, mkewe, nduguze, majirani zake, wapenzi wake, marafiki zake, hata na wasiri wake waliomjua sana? Hayawi, hayawi mnayodhania! Kuna tofauti kubwa baina ya haki na uzushi huu. Je hamkubakiwa na akili hata kiduchu mnayoweza kwayo kufikia lubu? Bali visa hivi ni porojo tu visivyo na asili yake, ambavyo tabia njema haivikubali, wala havikuashiriwa waziwazi au kwa kuficha ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu wala ndani ya Hadithi za Mtume[saw] wake. Hivyo, wanaovifuata visa hivyo, wanalifuata porojo tu, nao wanatangatanga ovyo.

Ama ushukaji wa Isa[as], basi uelewe kuwa neno *nuzuul* ni la Kiarabu, latumika kuheshimu na kutukuza, na Enyi wanachuoni mwajua maana ya *naziil* — mfasiri. Na ndani ya vitabu vya Hadithi hatukuona Hadithi yoyote ya Mtume[saw] wa Mungu iliyo *marfu' muttasil* inayofahamika kwayo kwamba Isa[as] atateremka toka mbinguni, wala hatukukuta neno *Samaa* ndani ya Hadithi yoyote iwayo miongoni mwa Hadithi Sahihi imara. Na hili ni jambo la wazi sana wanalolielewe

wataalamu wa Hadithi, na halikani isipokuwa jahili au ajisingiziaye kuwa jahili, wala hakuna alikataaye ila vipofu. Isitoshe, jambo hili pia ni kinyume na Kurani na ni dhidi yake. Basi, baada ya Kurani mtaiamini hadithi gani? Na Mwenyezi Mungu Subhana Amesema: 'Siye Muhammad ila yu Mtume. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume' (Aali 'Imraan, 3:145).[20] Hivyo Akabainisha kuwa Manabii na Mitume waliokuwa hapo kabla wamekwisha fariki wote. Na hii hii ndiyo aya aliyoisoma Hadhrat Abu Bakr[ra] Siddik, Mungu Amwie radhi, wakati masahaba walipokuwa wanahitilafiana. Namaanisha kwamba baadhi ya watu miongoni mwa masahaba walipohitilafiana kuhusu kifo cha Mtume[saw] wa Mwenyezi Mungu, na Hadhrat Umar[ra] akasema kuwa yeye atarejea kama atakavyorejea Isa[as], na ndivyo walivyosema baadhi yao waliokosea, basi Hadhrat Abu Bakr[ra] akasikia maneno yao na waliyokuwa wakidhania, hapo yeye akasimama juu ya mimbari na akalonga: Nisikilizeni! nao walikuwa wamejumuika wote kwa sababu ya kifo cha Mtume wa Mungu, ***Sullallaahu 'alaihi wa Sallam***. Basi, wakasikia ***aya hii*** na wakaathirika ajabu kana kwamba aya hii ilishuka siku hiyo hiyo, nao wakalia

---

[20] Kuna desturi maalum ya wenye lugha ya Kiarabu kuhusu neno *Khalaa.* Wasemapo, mathalani, *Khalaa Zaid min hadhihiddari au min hadhihiddunia*, wanamaanisha kutokana na kauli hii kuwa huyo hatarejea abadan. Na Mwenyezi Mungu Amechagua neno hili kwa kuashiria kwenye msemo huu kama isivyofichika. Mwandishi.

na kusadikisha. Na siku hiyo hakubaki yeyote awaye miongoni mwao isipokuwa akaamini kwa moyo wote kwamba Manabii wote wameishafariki na mauti yamewajia. Hivyo, haikubaki kwao fursa ya maombolezo juu ya kifo cha Mtume[saw] wao wala nafasi ya kumwonea wivu yeyote kwa ajili ya mpendwa[saw] wao, na wakafahamu kufariki kwake, na macho yao yakatiririsha machozi nao wakatamka: Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Na wakawa wanaisoma aya hii mitaani, masokoni na nyumbani huku wakilia. Na Hadhrat Hassaan[ra] bin Thabit, baada ya hotuba ya Abu Bakr[ra] akasoma beti hizi kuhusiana na kifo cha Mtume[saw] wa Mungu:

كُنْتَ السَّوَادَ لِنَاظِرِيْ ۝ فَعَمِيْ عَلَيْكَ النَّاظِرُ
مَنْ شَاءَ بَعْدَكَ فَلْيَمُتْ ۝ فَعَلَيْكَ كُنْتُ أُحَاذِرُ

> Ulikuwa mboni ya jicho langu, basi jicho langu limepofuka kwa kifo chako. Baada yako atakaye na afe, mie nilikuwa nahofia kifo chako tu.

Anataka kusema kwamba hofu yangu yote yalikuhusu wewe tu. Na ulipofariki, basi sijali kuwa afe Musa[as] au Isa[as]. Tazameni jinsi walivyompenda Nabii[saw] wao, na namna zilivyokuwa zinadhihiri toka kwao adabu za mahaba na alama zake, Enyi mgombanao! Angalieni jinsi ilivyodai ghera yao kwamba hawakuuridhia uhai wa Nabii yeyote baada ya kifo cha Mtume[saw] wa Mwenyezi Mungu. Basi wakaongozwa kwenye njia iilyonyoka kama wapenzi waongozwavyo, nao zikaafikiana nyoyo

zao na muradi wa aya *Kad Khalat min Kablihir Rusul* na wakauamini na wakaufurahia. Kisha mkaja nyie baada ya masahaba; hamkumheshimu Nabii[saw] wenu kama ipasavyo kumheshimu, na mwasema mnayoyasema. Je mapenzi yenu kwa Nabii[saw] wenu yanawaamuruni kwamba Isa[as] abaki hai huko mbinguni ilhali miaka elfu na takriban theluthi yake imepita juu ya kufariki kwa Mtume[saw] wa Mungu? Ni mbaya sana mnayohukumu. Je mmeridhia kwamba Nabii[saw] wenu awe amezikwa ndani ya ardhi katika Madina, lakini Isa[as] awe hai hadi wakati huu? Mcheni Mungu, Enyi mnaojasiri! Ijima ya masahabu juu ya kifo cha Isa[as] ilikuwa ni ijima ya kwanza iliyofanyika katika Islam kwa wote kuafikiana, hata mtu mmoja hakuwa nje yake kama mjuavyo. Na hii ndiyo hisani ya Hadhrat Siddik[ra] juu ya Waislamu wote ya kwamba akathibitisha toka katika Kurani mauti ya Manabii wote pamwe na mauti ya Isa[as]. Je mnashukuru? Kisha wakawaandamia nyuma yao wazao wanaoiacha Kurani na kumwasi Rahmani na kumtungia Mungu uongo, nao wanatambua kuwa Kurani inamfisha Masihi na kukariri kueleza wazi kabisa na inamzuia kupaa mbinguni na kuwapa habari njema Waislamu kwamba Khatamul Khulafaa na Masihi wa umati huu ndiye toka katika umati huu huu. Basi, mwamngojea Masihi yupi tena baada yangu? Na husema kuwa hatuoni haja ya Masihi na yatutosha Kurani; hao wanakikadhibisha Kitabu cha Mungu hali wanajua. Kama wangeifuata Kurani wasingenikadhibisha, kwani Kurani inanishu-

hudia, lakini hawa wananikadhibisha. Hivyo, ikathibitika kwamba wanajigamba tu na hawaiamini Kurani. Ndimi zao zinaongopa. Hamna nyoyoni mwao isipokuwa dunia na kwayo wanaelekea. Wanaona nchi imetetemeshwa, na kifo kinashuka na mauti yananguruma, hata hivyo hawarudi. Je hawakuona machafuko ya ardhi ili wangekuwa na mioyo ambayo wangefahamu kwayo? Lakini hawa ni watu wanaotakabari. Je wanamkufuru Adamu wa zama hizi, ilhali juu ya ardhi kila aina ya mnyama amezalika; je hawaoni? Wanawaona baadhi ya watu kama mbwa, na wengine kama mbwamwitu, baadhi yao kama nguruwe, wengine kama punda, na baadhi yao kama nyoka wanauma. Hakuna mnyama isipokuwa limedhihiri kundi miongoni mwa watu mithili yake nao wanatenda mfano wa wanyama. Kadhalika ardhi imepasuka ipasavyo kupasuka. Je bado haujaja wakati kwamba Mwenyezi Mungu Amuumbe Adamu baada ya wanyama hao, na kumpulizia roho Yake? Enyi wenye akili, suna ya Mungu haibadiliki.

Na waambiwapo harakieni kuhudhuria mbele ya Khalifa wa Mungu na yafuateni Aliyomfunuliwa Mwenyezi Mungu ili mpate kurehemiwa, utawaona macho yao yanakuwa mekundu kwa ghaidhi na husema tumekuwaje kwamba tumfuate jahili, nasi tunayo elimu zaidi kuliko yeye, hivyo ni juu yake afanye baiati yetu. Je tufanye baiati ya yule asiye na elimu yoyote, nasi tu wataalamu. Basi, wasubiri tu hadi warejee kwa Mola

wao na wajichungulie sura zao; basi waache na hila zao. Mwenyezi Mungu Amewatia kovu juu ya pua zao na Amedhihirisha uhakika wa elimu zao, hata hivyo hawajuti. Na waitwapo kwenye haki, utaona chuki juu ya nyuso zao, nao hupita wakitusi. Hao ndio wale Aliowapiga Mungu muhuri juu ya nyoyo zao na kupofusha macho yao na kupindua nyuso zao, basi hawanao usuhuba. Wanamngojea Masihi aje toka mbinguni na wanafurahia maneno yaliyoingizwa kwa hila kupitia wale Manasara waliokuwa wanasilimu. Yawezekanje ateremke yule aliyeshukiwa Injili ilhali Kurani imesema 'miongoni mwenu'.[21] Basi, ni waongo tu ndio wanaohilikishwa. Je imewateremkia Kurani nyingine, au wameshabihiana na Wayahudi na wakabadili jinsi walivyokuwa wakibadili hao. Na Kurani imemfisha Masihi, na Masihi ameikiri ndani ya Kurani. Je hawazingatii kauli yake: *Falammaa Tawaffaitani*, au je nyoyo zao zimetiwa kufuli, au hao ndio vipofu? Bila shaka Kurani imeashiria ndani ya idadi kwa hesabu ya

---

[21] Nimewahi kusikia kuwa baadhi ya majahili wanasema kuwa Mahdi atatokana na Bani Fatima, basi namna gani mtu huyu anasema kuwa mimi ni Mahdi alyeahidiwa ilhali hayuko miongoni mwa Bani Fatima? Jawabu lake ni kwamba Mwenyezi Mungu Anajua uhakika wa hali na uhakika wa nasaba na ali. Pamoja na hayo, mimi ni Mahdi aliye Masihi aliyeahidiwa, aliyengojewa. Na kuhusiana naye haikuelezwa kuwa atatokana na Bani Fatima. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na Saa ipondayo. Mwandishi.

*jummal* ya Sura Al 'Asr kwenye muda uliopita toka Adam[as] mpaka Nabii[saw] wetu sawa na kalenda ya mwezi. Basi, pigeni hesabu mkishuku. Na hii ilipohakikika, basi eleweni kuwa mimi nimezaliwa katika elfu ya sita ndani ya nyakati za mwisho kama alivyoumbwa Adamu katika siku ya sita katika saa za mwisho. Hivyo minghairi yangu hakuna kwa Masihi mwingine mahali pa kukanyaga baada ya zama zangu ikiwa mnatafakari na hamdhulumu. Basi, mimi ni mwenye zama hizi, hakuna zama baada yangu. Hivyo, Enyi waongo, katika zama gani mtamshusha Masihi wenu wa kudhaniwa? Torati na Injili na Kurani zimeafikiana juu ya zama hizi; waulizeni, basi, watu wa Kitabu kama mkishuku. Na umeishapita mwisho wa elfu ya sita na haukubakia wakati wa Masihi kushuka baada yake. Ndani mwake mna ishara kwa watu watafutao ukweli. Na hii ilikuwa ni miongoni mwa alama za aliyeahidiwa ndani ya Kurani nayo wanaijua wanaotafakari. Na elfu ya sita ni kama ile siku ya sita alimoumbwa Adamu[as]. Na siku moja kwa Mola wako ni kama miaka elfu mnayoihesabu.

## MLANGO WA TANO

Enyi wenye busara na uchamungu miongoni mwa wasikilizaji, tambueni kuwa zama zetu hizi ni zama za mwisho[22] nami ni kati ya wale walio wa mwisho. Kwa hakika zama zetu hizi ni siku ya Ijumaa na ndani yake wamejumuishwa watu wa kila sehemu na kila nchi, na vimejumuishwa vyote walivyohitaji watu vya mema ya dunia na dini na namna mbalimbali za elimu na maarifa na siri za sheria imara. Nafsi zimeunganishwa, na utaona kila garimoshi asubuhi na jioni linaleta makundi ya watu watokanao na mashariki na magharibi na yamekusanywa kwa sababu yake matunda ya mashariki na magharibi kwa idhini ya Mungu Mrehemevu kuliko warehemevu wote. Na yatarajiwa kwamba hatimaye Mwenyezi Mungu Atasuluhisha mambo ya dini yetu kwa rehema yake juu ya umati huu na walimwengu wote, na Atawaokoa mahuluku ukingoni mwa shimo walikosimama. Hii ni ahadi ya Mungu, naye ndiye Mkweli kuliko wakweli wote. Na Islam itazishinda dini zote zile. Na utaona makundi toka kwa kila kaumu

---

[22] Haiwezi kusemwa kwamba kwa kuwa saa ya kiama imefichika hivyo haijuzu kusema kwa zama zozote kuwa ni za mwisho, kwani hatuainishi saa maalum, bali twasema kuwa hiyo ni katika saa zilizoainishwa. Na hamna shaka kwamba Kurani imezifananisha elfu za dunia na siku za kuhuluku. Na yote tuliyolonga yanatokana na hii hii jinsi isivyofichika kwa wenye busara. Mwandishi.

yataingia ndani yake kwa kutubu. Hivyo, hamna shaka kuwa zama zetu hizi ni Ijumaa; ardhi na mbingu zinashuhudia juu yake. Ndani mwake yote yamejumuika yaliyotawanyika baina ya wale wa awali. Nami nilizaliwa katika Ijumaa hii saa za Alasiri zilizokuwa za dhiki kwa Islam na Waislamu, jinsi Adamu[as] Mteule wa Mungu alivyoumbwa katika saa za mwisho za Ijumaa. Kwa hakika zama zake zilikuwa ni mfano wa wakati huu, na wakati wake wa Alasiri ulikuwa ni kivuli kwa zama hizi ambamo Islam ilikabwa na misiba iliiangukia dini yetu na ilikuwa karibu jua la dini lichwe. Na mwaona siku hizi nuru ya Isalm imefifia kwa sababu ya kiza kinene na wingi wa watu waovu na mashambulizi ya wapinzani kwa kalamu na wakadhibishao. Na ilikuwa karibu hata alama yake isibaki lau kama fadhili ya Mungu Mkarimu Msaidizi isingehifadhi. Hivyo, ghera ya Mungu ilitaka kumuinua Mujadidi ndani ya siku hii afananaye na Adamu[as]. Basi, Akaniumba siku ya leo hii wakati wa Alasiri, namaanisha saa za dhiki, na Akanifundisha Mwenywe na kunipa heshima na Akaniingiza ndani ya waja wake walioheshimika, na Akanifanya mwamuzi kwa watu wanaohitilafiana, Naye ndiye Hakimu bora kuliko mahakimu. Watu wakashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu Amenisaidia na na katika kila jambo Ameniauni. Watu wakanifukuza, lakini Yeye Akanipa makao, wakanishambulia naye Akanihami na Akazidisha Jumuiya yangu na Akaimarisha silsila yangu. Hivyo, ikawaduwaza fadhili ya Mungu iliyo juu yangu na

kuongeza dhana yao mbaya na wakasema: Je Mwenyezi Mungu Anamuweka mtu kuwa Khalifa katika ardhi ambaye atafanya uharibifu humu na kumwaga damu? Basi, Mungu Akawajibu kupitia mimi na Akasema: Mimi Najua zaidi msiyoyajua. Na wakasema mtu fulani ameuliwa kiudhalimu — yaani mtu fulani miongoni mwa Wakristo ameuawa. Na wakanasibisha mauaji haya kwangu ili waniingize katika wale wanaofanya uharibifu ardhini na kuwaua watu kidhuluma na kiufisadi; lakini Mwenyezi Anajua kuwa sihusikani na jambo hili, na maneno yao haya ni masingizio tu juu yangu, na Mwenyezi Mungu Anawajua sana wadhalimu. Hapo Mwenyezi Mungu Akanifunulia wahyi Akisimulia kauli yao: 'Je Utaweka humu' mpaka kauli yake: 'Hakika Najua sana msiyoyajua', ikiwa ni ibra kwa wajasiri. Na kauli zao hizo hazikutoka ndimini mwao isipokuwa kwamba watimize utabiri wa Mungu uliotajwa hapo kabla, na ili wathibitishe kushabihiana kwangu na Adamu[as] katika masingizio ya kuleta ufisadi na kumwaga damu. Basi Mwenyezi Mungu Akawajibu katika wahyi wake, na wahyi huo ulichapishwa na kuenezwa kabla hajauawa huyo mshirikina ambaye kuhusiana naye wanadhani kana kwamba nilimuua, na wanadhani kwamba kabla ya kifo cha huyo Mkristo watu wangu walimshambulia ili kumuua. Basi, sifa zote njema ni za Mungu Aliyenitetea kwa maneno yaliyosemwa kumhusu Adamu, naye ndiye Mbora wa wateteao. Ndiye Yule Yule Aliyerudisha jua la Islam baada ya kukaribia

kuchwa, kana kwamba likachomoza toka katika magharibi yake na likawadhihirikia walitafutao.

Kwa kweli mfano wangu mbele ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adamu[as]. Nami sikuumbwa ila baada ya kukithiri juu ya ardhi wanyama wenye miguu minne, wanyama mbuai, vidudu na fisi. Na wakakithiri wanyama wa kila aina juu ya uso wa ardhi, wakahitilafiana wao kwa wao, na kulikuwa hamna Adamu yeyote kuwatawala na kuwa mwamuzi kwao na kutoa uamuzi baina yao. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akanifanya Adamu na kunijaalia yote Aliyomjaalia baba wa binadamu — Adamu — na pia Akanifanya kivuli cha Khatamun Nabiyyina na Sayyidul Mursalina. Na siri ndani mwake ni kuwa Mwenyezi Mungu aliamua tangu azali kwamba Atamwumba Adamu atakayekuwa Khatamul Khulafaa katika zama za mwisho kama Alivyomwumba Adamu aliyekuwa Khalifa wake wa kwanza mwanzoi mwa zama ili duara la asili likamilika na ili mwisho ulandane na mwanzo, na kwamba kufanana huku kuwe ni dalili bayana kwa Tauhid, na kwamba kilichoumbwa kiwe kinahakikisha uwepo wa Aliyekiumba kwa dalili ya kidhahiri. Kwani, hali ya kuwa duara hufanana na umoja, bali humaanisha Umoja, na ndiyo sababu hupatikana uduara katika kila kitu cha asili, na hakuna cochote cha asili kisichokuwa duara. Na hii ndiyo ili watu watambue kuwa Mungu ni Mmoja wa pekee Ambaye Akakipa kila Alichoumba hali ya umoja ili kwamba watambue kuwa Huyo ndiye Mola

wa walimwengu. Basi, kimuhtasari, Mungu ni Mmoja naye Hupenda kuwa Mmoja. Hivyo, Umoja wake ulitaka kuwa yule mtu aliye Khatamul Khulafaa ashabihiane na Adamu aliyekuwa wa kwanza kujaaliwa Ukhalifa mkubwa kabisa na wa kwanza aliyepuliziwa roho na Mola wa mahuluku, ili zama za mwanadamu ziwe kama duara ambalo nukta yake ya mwisho iungane na nukta yake ya kwanza na ili iashirie kwenye Umoja ule alioitwa kwake binadamu. Na umoja ni kitu Anachokipenda sana Mola wetu Mtukufu, kwa hiyo akachagua hali ya duara kwa binadamu wakati wa kumwuumba. Hivyo, Akamaliza kwa Adamu kama Aliyoanzisha kwa Adamu katika mwanzo wa zama. Ndani yake kuna ishara kwa wanaotafakari. Kwa hakika Adamu wa zama za mwisho ndiye Nabii[saw] wetu na uhusiano baina yangu na yeye ni kama ulivyo uhusiao baina ya mwalimu na mwanafunzi, na kwenye hii hii Mungu Subhana Aliashiria katika kauli yake *Wa Akharina Minhum Lamma Yalhakuu Bihim.* Basi, tafakari ndani ya kauli yake *Akharina.* Mwenyezi Mungu Ameniteremshia baraka ya Mtume[saw] huyu, Akaitimiza na kukamilisha, na Akauvuta upole[saw] na ukarimu wake[saw] kwangu mpaka dhati yangu ikawa dhati yake. Hivyo, aingiaye ndani ya Jumuiya yangu akaingia ndani ya Masahaba wa Seyidi Mbora[saw] wa Mitume, na hii ndiyo maana ya *Wa Akharina Minhum* kama isivyofichika kwa wenye kuzingatia. Na yule aliyetofautisha baina yangu na Mteule[saw], huyo hakunitambua wala hakuniona. Kwa

kweli Nabii[saw] wetu alikuwa Adamu wa mwisho wa dunia na siku za mwisho na akaumbwa kama Adamu baada ya kuumbwa juu ya ardhi kila namna ya vidudu na kila aina ya wanyama mbuai na wanyama wenye miguu minne. Na Mwenyezi Mungu Alipokwishaumba mahaluku hawa, yaani namna mbalimbali za wanyama na wanyama mbuai na vidudu juu ya sehemu mbalimbali ya ardhi, namaanisha kila kundi la watu waovu na makafiri na walioitanguliza dunia juu ya dini, na kuumba mbinguni nyota zake na miezi na majua, yaani watu mastadi yaani waliotakasika na wenye nuru, baadaye Akamuumba Adamu huyo aitwaye jina Muhammad[saw] na Ahmad[saw], naye ndiye kiongozi wa wanadamu wote, na mcha Mungu zaidi na mwema sana kuliko wote na Imamu wa mahuluku. Kwenye hii hii Mungu Akaashiria ndani ya kauli yake: 'Na Mola wako Alipowaambia Malaika, 'Hakika Mimi Nitamweka Khalifa katika ardhi'. Naapa kwa heshima ya Mungu na jalali yake kwamba neno *Idh* ni dalili imara kabisa juu ya makusudio hayo, na muktadha wa aya hii ni dalili juu yake ikiwa wewe si kama Wayahudi. Hivyo, hamna shaka kwamba Yu Adamu wa zama za mwisho, na umati wake ni kama dhuria kwa Nabii[saw] huyu msifiwa, na kwenye hii hii Aliashiria ndani ya kauli yake: 'Hakika Tumekupa *Kauthar*'. Basi, izingatie na kutafakari kwa makini na usiwe miongoni mwa waloghafilika. Na zama za kiroho za Nabii[saw] wetu, amani juu yake, zilianzia toka elfu ya tano na kumalizika kwenye mwisho wa elfu ya

sita, na kwenye jambo hili Akaashiria ndani ya kauli Yake: 'Ili Aishindishe ***dini ya haki*** juu ya dini zote.' Na utondoti wa sehemu hii ni kuwa Nabii[saw] wetu amekuja juu ya nyayo za Adamu[as] na ruhania ya Adamu ikatokeza katika siku ya tano, kwani mpaka siku hiyo vyote vilikuwa vimeishaumbwa vilivyo viambato vya dhati yake na hakika ya asili yake. Maana, ardhi pamoja na viumbe vyake vyote, na mbingu pamwe na vilivyoumbwa ndani yake, vyote hivyo vilikuwa ni kiini cha dhati ya Adamu. Tuseme maada ya Adamu ikauhama uhakika wa vitu visivyo na uhai kwenda kwenye uhakika wa kimimea, kisha toka uhakika wa kimemea kaihamia hali ya uzima. Kisha baada ya hapo ikahama ikiwa katika hali ya kiroho toka sifa kamilifu za nyota kwenye sifa kamilifu za mwezi; tena toka nuru za mwezi kwenye miale ya jua. Mahawilisho hayo yote ndiyo maonyesho ya maendeleo ya ulimwengu kwenye daraja za juu za uhakika wa mtu. Tuseme kana kwamba mtu wakati fulani alikuwa katika hali ya kitu kisichokuwa na uhai, na katika kipindi kingine katika hali ya mimea na baadaye akawa na uzima. Kisha akawa nyota na mwezi na jua mpaka katika siku ya tano vyote vilijumuika ilivyohitaji tabia yake ya asili, yaani nguvu za kiardhi na za kimbingu, kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, Mbora wa waumbaji. Hivyo, uumbaji wote ukawa mtu mmoja kamili kwa ajili ya Adamu au kioo kwa ajili ya uwepo wa yule Aliyempa heshima na adhama. Kisha Mwenyezi Mungu Akataka kuonyesha

sifa hizo zote, zilizofichika, kwa ukamilifu ndani ya mtu mmoja ambaye awe dhihirisho la sifa hizo zote, basi ruhania ya Adamu ikadhihirika kwa mng'ao mkamilifu mtimilifu katika saa za mwisho za Ijumaa, yaani siku ya sita miongoni mwa siku sita. Kadhalika ruhania ya Nabii[saw] wetu ikatokeza ndani ya elfu ya tano kwa sifa zake za kiijmali. Na zama hizo hazikuwa kilele cha maendeleo yake, bali ilikuwa ni hatua ya kwanza kwa daraja za juu kabisa za sifa zake kamilifu. Kisha ruhania hii ilikamilika na ikang'arika mwisho wa elfu ya sita, yaani wakati huu kama alivyoumbwa Adamu mwisho wa siku ya sita kwa idhini ya Mungu, Mbora wa waumbaji. Na ruhania ya Nabii[saw] wetu, Mbora wa mitume, ikachukua dhihirisho lake toka katika umati wake ili kufikisha kikamilifu kutokeza kwake na kutapakaa nuru yake jinsi livyokuwa imeahidiwa ndani ya Kitabu kibanishacho. Nami ndimi dhihirisho lile lililoahidiwa na nuru iliyoahidiwa. Hivyo, amini na usiwe miongoni mwa wakataao. Ukipenda uisoma kauli Yake Mtukufu: 'Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili Aishindishe juu ya dini zote.' Basi tafakari kama walioongoka. Huu ni wakati wa ushindi na wakati wa kudhihiri kikamilifu ruhania toka kwa Mungu Jabari, Enyi jamii ya Waislamu! Kwa sababu hii hii imesimuliwa katika Hadithi kwamba Mtume[saw] alitumwa katika elfu ya sita ilhali kutumwa kwake kulikuwa ndani ya elfu ya tano kwa yakini kabisa. Basi hamna shaka kuwa hii ni ishara kwenye wakati wa

kudhihirika kitimilifu na kutimia makusudio kikamilifu na kudhihiri kwa ruhania kwa ukamilifu na siku za mfuro wa mawimbi ya baraka za Muhammad[saw] ulimwenguni. Na huu ndio mwisho wa elfu ya sita iliyo zama zilizoahidiwa kwa Masihi Mau'udi kushuka jinsi inavyofahamika kutokana na vitabu vya Manabii. Na zama hizi ni mahali pa kuweka mguu wake[saw] toka kwa Mungu Mmoja kama inavyofahamika kutokana na aya *Wa Akharina Minhum* na aya nyingine za Maandiko Matakatifu. Basi tafakari ikiwa u miongoni mwa wenye akili. Na utambue kuwa Nabii[saw] wetu jinsi alivyotumwa ndani ya elfu ya tano ndivyo alivyotumwa katika mwisho wa elfu ya sita kwa njia ya kumchagua Masihi Mau'udi kuwa kivuli chake. Na hii yathibitika kutokana na Kurani, basi hamna nafasi ya kukataa, na haikani yeyote isipokuwa yu miongoni mwa vipofu. Je hamzingtii aya *Wa Akharina Minhum,* na muradi wa neno *Minhum* utakuwaje sawa kama Mtume[saw] asiwepo ndani ya wale wa mwisho kama alivyokuwepo ndani ya wa awali? Hivyo, hakuna budi kukubali tuliyoeleza, na kwa wakanao hakuna mahali pa kukimbilia. Na yule akanaye hili kwamba kutumwa kwa Nabii[saw] kunahusikana na elfu ya sita kama kuhusikanavyo na elfu ya tano, mtu huyo amekataa haki na maneno ya Kurani na akawa miongoni mwa wadhalimu. Haki yenyewe ni kwamba ruhania yake[saw] ndiyo yenye nguvu zaidi na madhubuti na kamilifu siku hizi kulingana na miaka ile, bali ni kama mwezi mpevu. Kwa hiyo hatuhitaji upanga wala kundi

la wapiganao. Kwa ajili hii Mungu Subhana Amechukua, kwa kumwinua Masihi Mau'udi, hesabu ya karne sawa na hesabu ya usiku wa mwezi mpevu, toka katika hijra ya Seyidna Mbora[saw] wa ulimwengu wote ili hesabu hii iwe dalili juu ya daraja kamilifu timilifu katika daraja za maendeleo, na hiyo ndiyo karne ya nne baada miaka elfu toka kwa Khatamunu Nabiyyina, ili itimie ahadi ya kuishindisha dini, iliyotangulia ndani ya Kitabu kibanishacho, yaani kauli yake: 'Na bila shaka Mwenyezi Mungu Aliwasaidieni katika Badri hali nyinyi mlikuwa dhaifu. Basi angalia aya hii kama wenye busara, kwani hii inatoa dalili juu ya Badri mbili kwa yakini. Badri moja iliyopita kwa kuwasaidia wa awali, na Badri nyingine iliyo ishara kwa wale wa mwisho. Hivyo, hamna shaka kwamba aya hii ni ishara nyepesi kwenye zama zijazo zifananazo kihesabu na usiku wa mwezi mpevu, yaani miaka mia nne baada ya miaka elfu, na huu ndio usiku wa mwezi mpevu kiistiara mbele ya Mola wa walimwengu, ingawaje aya hii inayo maana nyingine pia inayohusiana na zama zilizopita pamoja na maana hii kama isivyofichika kwa wenye elimu. Kwani, aya hii ina jiha mbili, na msaada ndio misaada miwili na Badri ni Badri mbili: Badri moja ihusikanayo na zama zilizopita na Badri moja inayohusiana na mustakabali katika zama Waislamu watakapofikiwa na dhila kama mnavyoona katika zama hizi. Islam ilianzia kama hilali na ilikadiriwa hatimaye kuwa Badri — mwezi mpevu — katika zama za mwisho kwa idhini ya Mungu Jalali.

Hivyo, hekima ya Mwenyezi Mungu ilitaka kwamba Islam ipate kuwa mwezi mpevu katika karne inayofanana na Badri sawa na hesabu. Kwenye hii hii ikaashiria kauli yake: 'Na bila shaka Mwenyezi Mungu Aliwasaidieni katika Badri.' Basi tafakari kikamiifu na usiwe miongoni mwa walioghafilika. Na neno 'Aliwasaidieni' limetumika hapa kwa jiha nyingine, yaani kwa kumaanisha 'Atawasaidieni' kama isivyofichika kwa watambuzi.

Basi, kimuhtasari, Mwenyezi Mungu Alikuwa Amekadiria kwa Islam heshima mbili baada ya dhila mbili, ingawaje kwa Wayahudi Akawakadiria dhila mbili baada ya heshima mbili kama adhabu toka Kwake jinsi msomavyo ndani ya Sura Banii Israaiil habari za mafasiki na wadhalimu miongomi mwao. Na ilipowasibu Waislamu dhila ya kwanza huko Makka, Mwenyezi Mungu Akawaahidi akisema: 'Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Mwenyezi Mungu anao uwezo wa kuwasaidia.' Akaashiria ndani ya kauli Yake 'kuwasaidia' kwamba itawasibu makafiri adhabu kwa mikono ya Waaminio. Na Akatimiza Mwenyezi Mungu ahadi hii siku ya Badri na Akawaua makafiri kwa panga za Waislamu. Kisha Akawahabarisha kuhusu dhila ya pili kwa kaui Yake: 'Hata watakapofunguliwa Yajuja na Majuja'[23] (yaani watapata utawala na ushindi na hakuna

[23] Sura Al-Ambiyaa, 21:97

atakayeweza kukabiliana nao). 'Nao toka kila mahali pa juu watakuja mbiombio'[24]… 'Na Tutawaacha baadhi yao siku hiyo wakiwasonga wengine.'[25] ★ Na muradi wa 'toka kila mahali pa juu' ni ufaulu wao na kufuzu kwao kupata makusudio yao yote na kupanda kwao kwenye kila sehemu na kwamba wawe wanautawala kila utawala. Na muradi wa 'Tutawaacha baadhi yao siku hiyo wakiwasonga wengine'[26] ni kwamba katika zama zile moto wa vita utawaka baina ya kila dhehebu miongoni

---

[24] Sura Al-Kahf, 18:100

[25] Sura Al-Kahf, 18:103.

★ Mwenyezi Mungu baada ya aya hii Ameashiria ndani ya aya kadha mfululizo kwamba Yajuja na Majuja ndio Wakristo. Je huoni kauli Yake: 'Je waliokufuru wanadhani ya kwamba watawashika watumishi Wangu kuwa walinzi badala Yangu;' kadhalika kauli Yake: 'Sema, je Tuwaambieni wenye hasara zaidi kwa vitendo? Ni wale ambao bidii yao imepotea katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanazifanya vema sana' — Sura Al-Kahf, 18:104-105 — vile vile kauli Yake: 'Sema, kama bahari ingalikuwa wino (kuyaandika) maneno ya Mola wangu.' — Sura Al-Kahf, 18:110. Hamna shaka Manasara ndio watu waliomshika Masihi kuwa mwabudiwa minghairi ya Mungu, na wameelekea mambo ya dunia na wamewapita wengine katika kuvumbua sanaa mbalimbali na wakasema kuwa Masihi ndiye Neno la Mungu na vitu vyote vinatokana na Neno hili. Basi aya hizi zinakanusha madai yao. Mwandishi.

[26] Sura Al-Kahf, 18:100

mwa madhehebu ya wenye dini, nao watatumia rundo la dhahabu na fedha ili kukadhibisha Islam na kuifutilia mbali na kuwaritadisha Waislamu. Na watatunga vitabu vitakavyojaa maneno ya kuidhalilisha. Na Mwenyezi Mungu Ameashiria katika mahali pengi kwamba siku zile zitakuwa ni siku za ugeni kwa Islam, na hapo Waislamu watakuwa kama waliohusuriwa. Dhoruba kali za mifarakano zitavuma juu yao, nao watasambaratika. Ama kauli Yake: '*Ba'dhahum Yaumaidhin Yamuju fii ba'dhin*', Anamaanisha kwa hii kwamba dhehebu moja litateketeza dhehebu lingine, na Yajuja na Majuja watapata maendeleo ya juu sana na mtasikia habari za kutokezea kwao ardhini. Katika siku hizo Islam itakuwa kama ajuza, isiyokuwa na nguvu wala heshima, na itaisibu dhila juu ya dhila na itakuwa karibu izikwe pasipo kuvishwa sanda na kadhalika. Na itaisibu misiba ambayo mfano wake hakuna sikio liliosikia hapo kabla, na makundi kwa makundi ya majahii wataiacha dini wakiilaani na kuihakirisha na kuikadhibisha. Na mambo yote yatapinduka chini juu, na misiba itaishukia sheria na wenye sheria na mwezi wake utarudia kuwa kama kole la mtende la zamani machoni mwa watazamao, na hii ndiyo dhila isiyoiangukia dini hapo kabla, wala haitaisibu hadi siku ya kiama. Hapo ndipo msaada toka mbinguni utashuka na alama za heshima toka kwa Mungu Mtukufu pasipo upanga, mikuki na wapiganao

vita,[27] na kwenye hii kuna ishara ndani ya kauli Yake Aliye Mtukufu: 'Na itakapopulizwa baragumu, ndipo Tutawakusanya wote pamoja.'[28] Enyi kundi la wenye akili, hii ndiyo yamaanisha kuinuliwa kwa Masihi Mau'udi.[29] Na katika neno *nuzuul* liliokuja ndani ya

---

[27] Nabii Isa[as] hakupigana vita wala hakuamuru kupigana, na ndivyo alivyo Masihi Mau'udi, kwani yeye ni mfano wake toka kwa Mungu Jalali. Na siri ndani yake ni kwamba Yeye Ametaka kutuma Khatamul Khulafaa wa Bani Israeli na Khatamul Khulafaa wa Islam pasipokuwa na mkuki na upanga ili kufuta shaka zilizozalika hapo kabla ndani ya tabia za watu na ili kwamba watu waelewe kuwa kueneza dini kwa amri ya Mungu si kwa kukata shingo na kuwaua watu. Kisha, kwa kuwa Wayahudi katika zama za Isa[as] na Waislamu katika zama za Masihi Mau'udi wametoka wengi wao katika uchamungu na kuziasi amri za Mola Wadudi, hivyo ilikuwa mbali na hekima ya Mungu kwamba makafiri wauawe kwa ajili ya mafasiki hawa. Basi utafakari ipasavyo kutafakari na usiwe miongoni mwa walioghafilika. Mwandishi.

[28] Sura Al-Kahf, 18:100

[29] Na kadhalika imeashiriwa kwenye Masihi Mau'udi ndani ya Kitabu Kitukufu, namaanisha ndani ya Sura At-Tahriim, na ndiyo kauli ya Mungu Mtukufu: 'Na (mfano wa) Mariamu binti Imran aliyejilinda uchi wake, na Tukampulizia humo roho Yetu.' Hamna shaka kuwa muradi wake hapa ni Isa bin Mariamu. Basi muhtasari wa aya hii ni kwamba Mwenyezi Mungu Aliahidi kumfanya mja aliye mcha Mungu zaidi katika umati huu kuwa

Hadithi mna ishara kwamba katika zama za Masihi amri na msaada vyote vitateremka toka mbinguni pasipo kupitia mikono ya wanadamu wala jihadi ya mujaahidi na mambo yatashuka toka juu bila ya tadbiri ya wenye busara. Ndiyo kusema kana kwamba Masihi atatermka kama mvua toka mbinguni akiweka mikono yake juu ya mbawa za malaika, siyo juu ya mbawa za hila za dunia na tadbiri za binadamu. Na tabligh yake na hoja zake zitafikia hadi kando za ardhi haraka sana kama umeme unavyodhihiri kwenye upande mmoja na mara hung'ara pande zote. Basi, hivyo ndivyo itakavyokuwa katika zama hizi. Hivyo, na asikie aliye na masikio mawili! Na itapulizwa baragumu kwa kutapakaza mwanga, na wenye akili timamu watapaza sauti ili kujipatia mwongozo. Hivyo makundi ya mashariki na magharibi na kaskazini na kusini yatajumuika kwa amri ya Mungu Mtukufu, ndipo nyoyo zitazinduka na mbegu zitaota kwa maji hayo, si kwa moto wa vita na kwa kumwaga damu. Na watu watavutwa kwa mvuto wa kimbingu uliotakaswa na michanganyiko ya kiardhi, kwani hii itakuwa ni mfano wa hukumu toka kwa Mmiliki wa siku

---

Masihi bin Mariamu na kumpulizia roho yake kwa njia ya kuwa *Buruuz* — kivuli. Basi hii ndiyo ahadi toka kwa Mungu kwa sura ya mfano kwa mcha Mungu zaidi miongoni mwa Waislamu. Hivyo zingatia jinsi Mwenyezi Mungu Alivyowaita baadhi ya waja wa umati huu kuwa Isa bin Mariamu, na usiwe miongoni mwa majahili. Mwandishi.

ya malipo. Na Mwenyezi Mungu Ameahidi wakati wa fitina kubwa katika zama za mwisho na balaa kubwa kabla ya siku ya Kiama kwamba Ataisaidia Mwenyewe dini yake katika siku zile, na ndipo Islam itakuwa kama mwezi mpevu kamili, kwenye hii hii Mungu Subhana Ameashiria ndani ya kauli Yake: 'Na itapulizwa baragumu, ndipo Tutawakusanya wote pamoja.'[30] Na Akahabarisha ndani ya aya kabla ya aya hii kuhusu mfarakano mkubwa akisema: 'Na Tutawaacha baadhi yao siku hiyo wakiwasonga wengine', kisha kwa kauli Yake 'Na itapulizwa baragumu',[31] Akatoa habari njema ya kujumuisha baada ya kufarakana. Na kujumuika huko hakutakuwa isipokuwa ndani ya karne ya Badri ili sura hii iwe dalili juu ya maana yake, kama msaada wa kwanza ulivyokuwa katika Badri. Hivyo, hapa pana bishara mbili njema kwa waaminio, nazo zinang'ara kama lulu ndani ya Kitabu kibainishacho. Na ni hakika kuwa wakati wa ushindi dhahiri umeishapita katika zama za Nabii[saw] wetu Mteule, na umebaki ushindi mwingine nao ndio adhimu sana na mkubwa kabisa na dhahiri zaidi kuliko ushindi wa kwanza. Na imekadiriwa kuwa wakati wake ndio wakati wa Masihi Mau'udi toka kwa Mungu, Raufu, Wadudi na Mrehemevu kuliko warehemevu wote. Kwenye hii hii kuna ishara katika kauli Yake: 'Utukufu ni wa Yeye Ambaye Alimpeleka

---

[30] Sura Al-Kahf, 18:100

[31] Sura Bani Israaiil, 17:2

Mtumishi Wake usiku kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake.'[32] Basi tafakarini ndani ya aya hii na usipite kama walioghafilika. Na katika neno 'Msikiti Mtukufu' na neno 'Msikiti wa Mbali' ambao kuusifu imesemwa sentensi 'ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake,' kuna ishara nyepesi kwa wenye kuzingatia. Na ishara yenyewe ni kuwa neno 'Haraam' linadhihirisha kuwa makafiri waliharamishwa katika zama za Nabii[saw] kuidhuru dini kwa njama au kuijia kama mwindaji, na Mwenyezi Mungu Akamhifadhi Nabii[saw] wake na dini yake na mashambulizi ya washambulizi na dhuluma za wadhaimu. Na Mwenyezi katika zama hizo Hakuwang'olea mbali maadui wa dini ipasavyo kuwang'olea, walakini akaihifadhi dini na mashambulizi yao na kuwaharamishia kupata ushindi katika mapigano. Hivyo, jambo la kuisaidia dini likaanzia toka kwa Msikiti Mtukufu, yaani kutetea na waovu. Kisha jambo hili litatimia kwenye Msikiti wa Mbali ambao ndani mwake mtafika nuru ya dini kwa upeo wa mwisho kama mwezi mpevu mtimilifu, na kila baraka itapatikana kwake inayoweza kutazamiwa wakti wa ukamilifu ambao hakuna ukamilifu tena zaidi yake. Na hii ndiyo ahadi ya Mungu Mjuzi. Basi ٱلْمَسْجِدُ الْحَرَامُ — Msikiti Mtukufu — unatoa habari njema ya kuondoa shari na kuhifadhi na machukizo. Lakini ٱلْمَسْجِدُ الْأَقْصَى —

---

[32] Sura Bani Israaiil, 17:2

Msikiti wa Mbali — unamaanisha kupatikana mema na baraka za aina aina na kufikia kwenye maendeleo ya juu. Basi jambo la dini yetu likaanzia na kuondoa madhara na litatimia kwenye ukamilifu wa heri. Na ndani mwake mna ishara kwa wenye kuzingatia. Kisha aya ya Israa inaongoza kwenye habari ya ndani ambayo hakuna budi kuitaja kwa ajili ya marafiki ili wazidi katika elimu na yakini, kwani mali bora ndiyo elimu na yakini. Na habari yenyewe ni kwamba Israa — Safari ya usiku — iliwajibika kizama kama ilivyowajibika kimakani, ili safari ya Nabii[saw] wetu kizama na kimakani itimilike, na ili Miraji ya Khatamun Nabiyyina ikamilike. Na hamna shaka kwamba zama za mbali sana za Miraji ya kizama ni zama za Masihi Mau‘udi, nazo ndizo zama za ukamilifu wa baraka, na kila mwaminio atalikubai jambo hili bila kukataa, na hamna shaka kwamba msikiti wa Masihi Mau‘udi kulingana na Msikiti Mtakatifu ni Msikiti wa Mbali kwa jiha ya zama, nao ndio umejazwa toka kila janibu baraka na nuru kama mwezi mpevu mtimilifu, ili likamilike kwao duara la dini. Kwani Islam ilidhihiri toka Msikiti Mtakatifu kama hilali, kisha ikawa mwezi mpevu ilipofika kwenye Msikiti wa Mbali. Na kwa sababu hii hii Masihi alidhihiri sawa na hesabu ya mwezi mpevu, kwa kuashiria kwenye daraja hii. Kisha kuna dalili nyingine hapa juu ya kuwajibika Israa ya kizama kwa amri ya Mola, nayo ndiyo kwamba Mungu

Aliyetukuka Ameashiria ndani ya kauli yake, 'Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao'[33] kwenye jambo hili kwamba Jumuiya ya Masihi Mau'udi mbele ya Mwenyezi Mungu ni miongoni mwa masahaba bila tofauti ya kuiita jina hili. Na daraja hii haithibitiki kwao pasipokuwa Nabii[saw] baina yao kwa nguvu yake takatifu na baraka za ruhania kama alivyokuwa ndani ya masahaba, yaani kwa kupitia Masihi Mau'udi aliye dhihirisho lake au kama joho lake. Hivyo, imethibitika kutokana na maandiko wazi ya Vitabu Vitukufu vya dini ya kwamba Miraji ya Nabii[saw] wetu jinsi ilivyokuwa ya kimakani ndivyo ilivyokuwa ya kizama, na hataikana isipokuwa aliyepoteza macho yake na akawa miongoni mwa vipofu. Na hakuna shaka wala wasiwasi kwamba Miraji ya kizama ilikuwa lazima kwa kuhakikisha maana ya aya hii, la sivyo maana ya aya hii ingebatilika kama isivyofichika kwa wenye kutafakari na wenye ujuzi. Basi, imehakikika kwamba Masihi Mau'udi ni dhihirisho la uhakika wa Ki-Muhammad na ameteremka ndani ya mavazi ya kijalali, na kwa sababu hii hii kudhihiri kwake mbele ya Mwenyezi Mungu ni kudhihiri kwa Nabii[saw] Wake Mteule, na zama zake zimehesabiwa kuwa upeo wa Miraji ya kizama kwa Mtume Mteule[saw] na kilele cha onyesho la ruhania ya Seyidna Mbora[saw] wa viumbe, na hii ilikuwa ni ahadi imara ya Mola wa walimwengu. Na kwa kuwa Masihi Mau'udi alikuwa kwa dhati ya Nabii[saw]

[33] Sura Al-Jumu'ah, 62:4

wetu kama kioo na mwenye kutimiza jukumu lake kwa kueneza baraka na kuishindisha Islam juu ya dini zote zile kwa ishara nyingi, basi Nabii[saw] akaishukuru bidii yake kama baba wawashukuruvyo wana wao na akausia salamu yake afikishiwe ikiwa ni ishara kwenye usalama wake na upandaji wa daraja yake. Lau kama muradi wa Masihi ungekuwa Isa[as] bin Mariamu aliyeteremshiwa Injili, wasia wa kufikisha salamu ungebatilika na kunakuwa hamna sababu yake. Kwani, Isa[as] atakaposhuka toka mbinguni, sawa na kauli yenu, basi hamna shaka kuwa Mtume[saw] wetu alikuwa anamjua kama marafiki, bali walikuwa wanasalimiana wakati wa kuonana, hapo kuweka amana ya salamu inakuwa hakuna maana na inakuwa bure kama kudhihaki, kwani kusalimiana kwao kulifanyika mara nyingi huko mbinguni na ilijulikana kabla ya kujulisha na kufahamisha. Isitoshe, yajulikana kwamba Yeye[saw] alionana na Isa[as] usiku wa Miraji, hivyo hamna shaka kwamba yeye hakuusia ila kwa ajili ya mtu ambaye alikuwa hakumuona na akawa na shauku yake ya kumsalimia. Ina maana gani ya kuusia kwa ajili ya mtu ambaye Mtume[saw] wa Mungu alimwona mara kadha kabla ya kifo na baada ya kifo na kumsalimia usiku wa Miraji, na hakuachana naye baada ya kufariki wakati wowote uwao. Je jambo hili halikuyumkinika ila kupitia mtu mmojawapo wa umati? Basi, tafakari kama hujawa mwenye wazimu. Je hutambui kuwa Nabii[saw] alipofariki alikuwa akipata nafasi ya kuonana na Isa[as] wakati

wowote, na kamwona Isa[as] pia usiku wa Israa. Hivyo milango ya kumsalimia ilikuwa wazi pasipo kupitia watu wa zama hizi. Basi usiipuueze salama ya Mtume [saw] wa Mungu, na zingatia ipasavyo kuzingati. Mola wangu Umfikishie salamu toka kwetu, na hapa ndipo mwisho wa maelezo.

**TAMATI**

## KASIDA KWA KILA MWENYE TABIA NJEMA

1. Naona mafuriko ya maafa Aliyokadiria Mwenye kukadiria, na ndani ya mahuluku kuna mabaya yanayosambazwa na kuenezwa.
2. Kwenye kila upande moto wa shari umepata kuwaka, na ndani mwa kila moyo mlidhihirika ugumu.
3. Na kwa upepo huu ukatingishika mti utoao kivuli chenye kutuliza na kutoa matunda.
4. Namwona kila aliyeghafilika anaililia dunia yake, basi yu nani aililiaye dini inayohakirishwa.
5. Dini imekuwa magofu, nami nayaona kama mwenye majonzi, na machozi yangu yanatiririka kwa kukumbuka majumba yake.
6. Upotofu umedhihirika kama upepo mkali wenye kung'olea mbali, na usiku wenye kiza kinene umening'iniza pazia lake.
7. Naona kiza, laiti ningekufa kabla ya kukiona, na kuonja kikombe cha mauti, au ningesaidiwa.
8. Upepo mkali unavuma kana kwamba ni wanyama mbuai katika ardhi ya India wanaolia vikali na kunguruma.
9. Mimi naona mafasiki, wafisadi na makundi yao tu; wema wa watu umepungua na upotovu umekithiri.

10. Naona chemchemi ya dini ya Mwenyezi Mungu imechafuka na ndani yake wanapita palahala na swala na kwenda ng'ambo ya pili — yaani haikubakiwa na mrithi wake.

11. Naikuta dini kama wagonjwa, imefunikwa na vumbi ardhini, na kila jahili anakwenda huko na huko akitamba ndani ya tamaa ya nafsi.

12. Hamu yao ndiyo kwa ajili ya furaha ya nafsi zao, na bidii yao ni kwa ajili ya maisha ya anasa yazidishwayo.

13. Wakasahau njia ya dini kwa sababu ya maovu na mghafala, na vimewapendeza uhalifu, ufasiki na kamari.

14. Na mafuriko ya ufasiki uangamizao yalipopita mipaka, nikatamani laiti yangetokea maradhi ya kuenea kote yahilikishayo.

15. Kwani, mbele ya wenye busara, kuangamia kwa watu kwapendeza zaidi, na ni afadhali kuliko upotofu uhilikishao.

16. Sisi tumesubiri juu ya dhuluma ya watu wote, lakini hatuwezi kuvmilia mafuriko ya bahati mbaya.

17. Kwa sababu ya misiba ya dini yetu moyo wangu ukayeyuka, nami nayajua msiyoyajua na kuyaona.

18. Na sikitko langu na huzuni yangu imepita mipaka yake; kama isingekuwa fadhili toka kwa Rahmani ningekuwa nimeishaangamia.

19. Machozi yangu yametokeza kutoka kwenye kona za macho yangu. Napiga kelele lakini akufurishaye haoni.

20. Maombi yangu yanapaa mbinguni, maneno yangu yanaathiri ndani ya jiwe.

21. Nami nimejaaliwa athari kutoka kwa Mungu Muumbaji wangu, hivyo kila moyo uliotakaswa unaikimbilia kauli yangu.

22. Kwa yakini moyo wangu unavutia kwa sababu ya unadhifu wake, na maelezo yangu yanaiathiri miamba.

23. Nilichimba milima ya nafsi yangu kwa kujaaliwa nguvu na Mungu Mtukufu, nao ukawa kama mfereji utiririkao.

24. Nami nimejaaliwa heba toka mbinguni wakati wa unyamavu wangu, na kauli yangu ni mkuki au upanga uliochomolewa.

25. Hili ndilo jambo lililompendeza Mmiliki wangu, Amenituma kwa ukweli na kwa haki, ili niwaonye.

26. Makundi ya maadui wa dini yangu waliponikadhibisha, nikasema: Nendeni mbali, mambo yaliyofichika yatadhihirika karibuni.

27. Watu waungwana hawanikatai, lakini kundi la wenye shari likaniudhi na kunikana.

28. Hao wakaweka vikwazo katika kila jambo nililolinuia, lakini Mola wangu Akanisaidia, hapo wakakimiba na kugeuza mgongo.

29. Na waliasije! Wallahi siri yake haikufahamika, ilhali mwanga wa ukweli wangu ulikuwa wazi zaidi kuliko jua.

30. Nikashikamana na subira wakati wa dhuluma ya watu dhalili kati yao, na jamaa zangu wa karibu nao walikuwa wakiuma kama nge.

31. Na huu ndio msiba mmojawapo juu ya Islam kwamba anakadhibishwa na kukufurishwa mithili yangu kwa matamanio ya nafsi.

32. Hivyo, nimeapa kwa Mungu Ambaye shani yake ni Tukufu, juu ya kwamba Atawadhalilisha maadui nami nitapata kuheshimika.

33. Upotevu una alama kadha na uongofu nao unazo alma mfano wake, hivyo inukeni kuzichanguza alama na kuzingatia.

34. Mwadhani kwamba nimezusha uongo kusudi kwa hila, ilhali baadhi ya dhana inakuwa dhambi na maovu.

35. Yawezekanaje hivyo ilihali Mwenyezi Mungu amedhihirisha utakaso wangu na Ameleta ishara zing'aazo na zaonekana wazi!

36. Itakufikia ahadi ya Mwenyezi Mungu namna usiyoiona, lakini yataitambua macho makali yaonayo sana.

37. Hakuna duniani awezaye kuuvunja upanga wa haki, na yule ainukaye kuuvunja kwa ubahili atavunjwa mwenyewe.

38. Ni nani yule anayenifanyia uadui ilihali Mola wangu Ananipenda, na yu nani awezaye kuniua ambapo Mwenyezi Mungu Ananisaida.

39. Na Mola wangu Anajua siri ya moyo wangu na siri zao, na kila kilichofichika kipo mble Yake.

40. Na kama ningekataliwa na Mfalme, pasi shaka uadui wa wanikadhibishao na kunihakirisha ungenidhuru.

41. Lakini nimefanya urafiki halisi na Mola wangu, hivyo zikanijia ishara za Mwenyezi Mungu jinsi uonavyo.

42. Dhuluma za mahuluku si jambo geni kwetu, kwani udhia wao ni suna isiyogeuka.

43. Nilipoambiwa kwamba u mtume, nikafikiria kuwa nimeitwa kwenye jukumu litakalokuwa zito kwa mahuluku.

44. Ewe unayenikufurisha, punguza kidogo kutumia nguvu, na uiogope ghadhabu ya Mola Aliyenena 'Usifuate usiyo na elimu nayo, na ujitahadhari.'

45. Na niliposema, mimi ni Mwislamu, ukasema u kafiri. Ewe mjasiri, uchamungu umepotea wapi?

46. Kama huogopi, sema tu: Wewe si mwaminio. Na zaja zama utakapoulizwa na kuhabarishwa.

47. Mimi nimetengana na nafsi yangu na mahuluku na matamanio ya nafsi, hivyo matusi hayaniudhi wala kunisifu hakunifaharishi.

48. Na kuna adui wengi walionijia baada ya kufikishia udhia upeo wake, lakini siwapi kisogo, nami sina tabia ya kuwapa watu kisogo.

49. Naona alama ya dhuluma inabaki juu ya pua, lakini alama za udhia hupata kubadilika.

50. Na Wallahi nimemfuata Muhammad[saw], na kila wakati naangazwa kwa mwanga wake.

51. Namstaajabia yule kipofu asiyetibu macho yake, lakini kwa dhuluma ya kijahili anagombana nasi na kutudhihaki.

52. Je umeshahau uchafu ambao uliridhika kuula, nawe unamsingizia mtu asiye na hatia na kuendelea kuitajataja.

53. Inapopungua elimu ya mtu, uchamungu wake nao hupungua, naye anakwenda mbiombio njiani mwa bahati mbaya na analaghai.

54. Nami simo miongoni mwa wale ambao upanga unaweza kuzuia makusudio yao; basi, anawezaje mkufurishaji kuniogofya kwa matukano.

55. Twapata kila siku msaada baada ya msaada; basi Ewe mwenye kuungua ndani ya moto wa husuda, kufa wewe katika moto unaowasha wewe mwenyewe.

56. Tumeahidiwa na Rahmani heshima na uongozi, basi inuka ukafute nakshi hii ikiwa unao uwezo.

57. Habedari! Zama zarudi kwenye mwongozo, kutumwa kwangu kuwe ni baraka kwenu. Hivyo mchangamke na kufurahi.

58. Acheni amri isiyokuwa ya Mungu, na jitahidini kufuata amri Yake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wetu, basi Mtiini na kuhudhuria mbele yake.

59. Habedari! Hakuna atakayebaki duniani minghairi ya Mwenyezi Mungu; kila mwenzi minghairi ya Mungu atatenganishwa.

**TAMATI**

**Maelezo Ya Pembeni Kuhusu Hotuba Iliyofunuliwa:**

## Kuna Tofauti Gani Baina Ya Adamu Na Masihi Mau'udi

Mwenyezi Mungu Alimuumba Adamu ili awalete watu kutoka hali ya kutokuwepo kwenye kuwepo na kutoka umoja Alete kwenye wingi. Na Akawafanya mataifa, makabila, makundi na jumuiya tofauti ili Aonyeshe namna mbalimbali za uwezo wake, na ili kujaribu nani miongoni mwao ni bora kimatendo na kuwapita wengine. Na Akamfanya Adamu dhihirisho la sifa yake iliyo chanzo cha ulimwengu, yaani sifa ya kuwa *Al-awwal* — wa kwanza — kama ilivyotajwa ndani ya Kitabu Chake bayana kauli yake *Huwal Awwalu* — Yu wa kwanza — na kwa sababu 'mwanzo' hutaka vingine baada yake, nafsi ya Adamu ilitaka wanaume na wanawake wengi. Hivyo amri ikashuka, na wanawake wakazaa sana na watu wakakithiri na ardhi ilijaa mahuluku. Kisha muda mrefu ukapita juu yao na makundi yao na maoni yao yakawa mengi na matakwa yao na matamanio yao yakahitilafiana. Wengi wao wakawa mafasiki na wakaanza kushambuliana wao kwa wao na wakazidi katika ufasiki na uasi na wakataka kwamba mwenye nguvu kati yao ammeze mnyonge, kama mdudu mmoja anavyommeza mdudu mwingine. Na walikuwa wameghafilika mpaka upotevu wa kila namna ulipojumuika ndani yao, uliokuwa ni jambo la lazima kwa zama za Masihi Mau'udi, na kila msiba ukaiangukia Islam hata ikawa kama mtu aliyezikwa

akiwa hai, na siku zikafikia mwisho wake na zikawa katika giza kama usiku, na zama zikataka vita iliyo vita ya mwisho,[34] hapo Mwenyezi Mungu Akamtuma Masihi wake kwa vita hii ili kutowesha kiza cha kufuru na kuwaangamiza wadhalimu kwa hoja, si kwa mkuki na

---

[34] Maelezo ya pembeni: Mwenyezi Mungu Alikuwa Amekadiria tangu azali kwamba vita kali itapiganwa mara mbili baina ya shetani na binadamu, mara ya kwanza ndani ya zama za awali na mara nyingine katika zama za mwisho. Ahadi ya kwanza ilipowadia shetani aliye chatu wa kale akampoteza Bi Hawa na akamtoa Adamu katika Pepo, na Iblisi akafaulu kupata utashi wake, na akawa kati ya wale walioshinda. Na ilipowadia ahadi ya mwisho, Mwenyezi Mungu Alitaka kumpa Adamu ushindi juu ya Iblisi na jeshi lake na kumuua dajali huyu kwa silaha kutoka Kwake. Hivyo, Akamuumba Masihi Mau'udi ambaye ni Adamu katika maana hii kwamba amhilikishe chatu huyo na ayaangamize kabisa aliyoyashinda huyo chatu. Basi ulilazimika ujaji wa Masihi ili hatimaye Adamu apate ushindi, na hii ilikuwa ni ahadi iliyotakiwa kutimizwa. Na Mwenyezi Mungu Amekwisha ashiria kwenye ushindi huu mkubwa na kuuawa kwa Dajali wa kale ambaye ndiye Shetani. Katika kauli yake Akasema: Bila shaka u miongoni mwa waliopewa muda.★ Yaani, kazi ya kukung'olea mbali kikamilifu na kuyaangamiza uliyoyashinda, yaani ushirikia wa namna mbali mbali na kufuru, na ufasiki, itafanyika katika zama za mwisho na wakti wa Imam wa zama, Masihi. Ufahamu, basi, kama u miongoni mwa wenye akili. Mwandishi.

★ Sura Al A'raaf, 7:16

pigo la upanga, na kukata mzizi wa makafiri, na ili watu warejee kwenye umoja na kujipoteza ndani ya huba ya Mungu baada ya kuhitilafiana. Basi, ikathibitika hapa kwamba Masihi Mau‘udi katika sifa hizi anakabiliana na Adamu kama kitu chenye hitilafu kinakabiliana na kitu kingine. Kwa yakini ndani mwake mna ishara kwa wamchao Mungu.

Kisha uelewe kuwa kuhitilafiana huku baina ya Adamu na Masihi Mau‘udi si kitu kilichofichika na nadharia tu, bali ni jambo wazi kabisa na ni miongoni mwa kweli zing’aazo zisizohitaji uthibitisho kwa hoja. Kwani Adamu alikuja ili kuwalta watu kwenye maisha ya dunia na kuwasha baina yao moto wa hitilafu na uadui, na Masihi wa nyimati amewasili ili kuwarudisha tena kwenye kujipoteza ndani ya huba ya Mungu na kuondoa hitilafu baina yao na ugomvi na inda na mzizi wa mifarakano na kusambaratika, na kuwavuta kwenye umoja na kujipoteza ndani ya Mungu na kukana vyote minghairi ya Mungu na kuleta kwenye urafiki halisi wa Mungu. Na Masihi ni dhihirisho la sifa *Al-Aakhir* ya Mungu Ambaye ndiye Khatam wa silsila ya mahuluku. Na kwenye sifa hii hii imeashiriwa ndani ya kauli yake *Huwal Aakhiru*, kwani sifa hii ndiyo alama ya mwisho wa ulimwengu. Hivyo, kwa sababu hii nafsi ya Masihi ilitaka silsila ya wingi kukomesha kwa kukithiri vifo au kwa kuyarudisha madheheu mbalimblai kwenye dini ambamo mna mauti ya nafsi kimatamanio na kiutashi, na ambamo sheria asilia ifuatwe inayoendelea sawa na

masilahi ya Mungu, na kuwaokoa watu katika kusamehe na kulipiza kisasi, mahaba na uadui, vilivyo matokeo ya maelekeo ya nafsi. Kwani, sheria ya kiasili inayotumia nguvu zote za binadamu kwa njia ya kufaa hairidhiki kuihudumia nguvu moja tu. Haizifungii ndani ya duara la 'msamaha' wala daura la 'kulipiza kisasi' tu, bali inaihesabu kuwa huluka mbovu; inaipa kila nguvu haki yake sawa na masilahi, kuafikiana na hali na haja inayosikika, na hubadilisha amri ya kusamehe na kulipiza kisasi, urafiki na uadui sawa na mabadiliko ya masilahi ya wakati. Hii hii ndiyo matui ya nafsi na matamanio na jazba za kinafsi, na kuingia ndani ya waliojipoteza katika huba ya Mungu. Basi kwa kifupi ni kwamba Masihi Mau'udi atawapeleka watu kutoka kuwepo kwenye hali ya kutokuwepo. Na atawakumbusha siku za nyumba iliyobomoka na kuwahamisha kwenye makao ya wafu, ama kwa kuwafisha kimwili kwa njia mbalimbali za maafa ya kimbingu au kiardhi, au kwa njia ya kufisha *nafsi Ammarah* — nafsi inayoamrisha kutenda mabaya — na kwa kifo kiwafikiacho wenye mwamko wa pili kwa kufagilia mbali nafsini mabaki ya athari za mungu yeyote mwingine, na kuondoa giza la utamanifu na kukamilisha daraja za kujipoteza ndani ya Mungu. Ndani mwake mna mwongozo kwa wanaotafakari. Kisha uelewe kuwa Masihi Mau'udi ndani ya Kitabu cha Mungu siye Isa bin Mariamu[as] aliyepewa Injili na alikuwa mwenye kutumikia sheria ya Musa[as], kama

walivyodhania baadhi ya majahili miongoni mwa watu wahalifu na kundi la waliokosa, bali yu *Khatamul Khulafaa* wa umati huu kama Isa[as] alivyokuwa Khatamul Khulafaa wa silsila ya Musa[as], na alikuwa ni tofali la mwisho kwa silsila hiyo na Khatamul Mursalina. Hii ndiyo haki. Basi, ole wao wasomao Kurani kisha wanapita wakikana. Kwa yakini Furkan imekwishatoa uamuzi baina ya wagomvi wawili kuhusiana na suala hili. Katika Sura An-Nuur imebainishwa kwa kauli yake *Minkum* kwamba Khatam wa Maimamu ndiye miongoni mwa dini hii. Kadhalika ikafafanua jambo hili katika Sura At-Tahriim, Al-Baqara na Al-Faatiha. Basi mwaenda wapi mkizikimbia nususi hizi imara bayana. Je kuna haja ya dalili nyingine baada ya Kurani kwa mwenye akili. Maneno gani mtayaamini baada ya sahifa zilizotakasiaka. Na Mwenyezi Mungu Amewaahidi waaminio ndani ya Sura At-Tahriim kwa kauli yake, 'Na Tukampulizia humo roho Yetu'[35] kwamba atamuumba Ibni Mariamu kutoka miongoni mwao, naye atalirithi jina hili na atakuwa Isa pasipo tofauti yoyote kitabia. Hivyo imeishatolewa katika aya hii ahadi toka kwa Mwenyezi Mungu kwamba mtu mmoja wa umati huu atapewa jina Ibni Mariamu na baada ya takwa kamili atapuliziwa roho Yake. Basi, mimi ndimi yule Masihi ambaye mnanilaumu kwa sababu hiyo. Na hakuna awezaye kubadili maneno ya Mungu Mwenye kudura na

[35] Sura At-Tahriim, 66:13

heshima. Je mwafanya hadhi yenu katika ahadi ya Mungu kuwa muwe Wayahudi kama Wayahudi wa umati wa Musa[as] katika maovu na uasi mkubwa, na hamtaki kuwa Masihi awe kutoka miongoni mwenu kama Masihi wa silsila ya Musa[as]? Ole wenu! Mmeridhika kushabihiana nao katika shari na hasara, lakini hamtaki muwe mwashabihiana nao katika heri. Wallahi, hata adui hamtendei adui yake yale mnayajitendea nafsi zenu. Mmetupa Neno la Mungu nyuma ya migongo yenu. Tuliwakumbusheni lakini mlisahau kusudi. Tuliwaonyesheni lakini mlijifanya vipofu. Na tuliwaiteni lakini mkakataa na mkaifuata *nafsi Ammara* katika kila jambo mlilolipinga, Enyi kundi la maadui! Je mtaachwa bure? Au mtasamehewa yote mliyoyatenda kwa matamanio ya nafsi yenu? Mmekuwaje hamtafakari ndani ya Kurani wala hamuoni aliyonena Mola wenu kwa kufafanua vizuri? Je haikuwatosheni aya ya Sura At-Tahriim, au mwajitenga na Neno la Mungu Mtukufu? Angalieni jinsi Mwenyezi Mungu Alivyopiga mfano wa Mariamu kwa umati huu ndani ya Sura hii kwa njia hii kwamba Ibni Mariamu atatokana nanyi wakati wa uchamungu kamili. Na ililazimika kuhakikisha mfano huu uliotajwa ndani ya aya hii kwamba mtu mmojawapo wa umati huu awe Isa bin Mariamu ili mfano huu uhakikike kidhahiri pia pasipo shaka wala wasiwasi. La sivyo, mfano huu utakuwa bure na batili ambapo mja yeyote miongoni mwa waja wa umati huu asisadikike kuutimiza. Na

jambo hili ni miongoni mwa mambo yasiyostahili kwa shani ya Mungu Mtukufu Mwenye heshima. Na hii hii ndiyo haki aliyonena Mungu Jalia. Basi, baada ya haki kuna nini isipokuwa upotevu? Ama Isa[as] ambaye ndiye mwenye Injili, basi yeye ameishafariki na Mola wetu Ametoa ushahidi ndani ya Kitabu Chake Kitukufu. Haiwezekani kwake kurejea duniani na kuwa Khatamul Ambiyaa ilhali Unabii umehitimishwa juu ya Nabii[saw] wetu, hivyo hamna baada yake Nabii isipokuwa yule aliyeangazwa kwa nuru yake na kufanywa mrithi wake toka kwa Mungu Mtukufu. Jueni kwamba Muhammad[saw] alijaaliwa Ukhatam tangu azali, kisha akajaaliwa yule ambaye roho yake[saw] ilimfundisha na kumfanya *kivuli* chake. Basi ni mwenye mibaraka yule aliyefundisha na aliyefundishwa.[36] Kwani Ukhatam

---

[36] Maelezo ya pembeni: hii ndiyo ishara kwenye wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ulioandikwa ndani ya Barahine Ahmadiyya, na muda zaidi ya miaka ishirini umekwishapta juu yake. Mwenyezi Mungu alinifunulia wahyi na Akasema: 'Kila baraka ni kutoka kwa Muhammad[saw], basi ni mwenye mibraka yule aliyefundisha na aliyefundishwa', yaani Nabii[saw] alikufundisha kwa njia ya athari ya ruhania yake na kujaza kikombe cha moyo wako rehema tele ili kukuingiza ndani ya masahaba zake na kukushirikisha katika baraka zake na ili utabiri wa Mungu *wa Aakhariina Minhum* utimie kwa fadhili na hisani Zake. Na kwa kuwa utabiri huu ulikuwa ni msingi imara na dalili kubwa juu ya madai yaliyomo ndani ya Kurani, hivyo Mungu Subhana

halisi ulikadiriwa ndani ya elfu ya sita iliyokuwa siku ya sita katika siku za Rahmani ili Khatam wa binadamu ashabihiane na *Abul Bashar* — Adamu. Na masilahi mengine yalitaka kwamba Mtume wetu[saw] atumwe katika siku ya tano, yaani ndani ya elfu ya tano baada ya Adamu, kwani siku ya tano ni siku ya mkusanyiko wa ulimwenu kabiri, nayo ndiyo kivuli cha Adamu ambaye Mwenyezi Mungu Alimpa heshima na taadhima. Kwani, Adamu alijikusanyia nafsini mwake vyote vilivyopo ulimwenguni na kuviunganisha vilivyokuwa vimesambaratika. Hivyo, hamna shaka kwamba ulimwengu kabiri katika sura zake mbalimbali ulikuwa mahali pa uumbaji wa kwanza wa Adamu. Basi kwa maana hii Adamu aliumbwa katika siku ya tano bila shaka wala wasiwasi. Kisha Mwenyezi Mungu alinuia kumuumba Nabii wetu[saw] aliye Adamu, kwa namna nyingine ndani ya elfu ya sita baada ya uumbaji wake wa kwanza kama alivyomuumba hapo kabla mteule wake Adamu mwisho wa siku ya sita katika siku za mwanzo wa uumbaji ili ikamilika kushabihiana baina ya uumbaji wa kwanza na mwingine. Na hii hii ndiyo siku ya Ijumaa ya kweli, na Ijumaa ya Adamu ilikuwa ni kivuli chake mbele ya wenye akili. Kisha Mwenyezi Mungu

---

Aliashiria kwayo katika Baraahine Ahmadiyya ili kutajwa kwake iwe ni hoja juu ya maadui kwa kulingana na urefu wa zama. Mwandishi.

Akamfanya mmoja wa umati wake kuwa dhihirisho lake kwa njia ya kivuli, ambaye katika jina lake na uasili wake ni kama huyo huyo, na Mungu Akamuumba katika siku ya sita sawa na hesabu ya siku za kuanzisha uumbaji kwa kukamilisha kushabihiana kwake, yaani katika mwisho wa elfu ya sita ili ashabihiane na Adamu kuhusu siku ya kuumbwa kwake, nayo ndiyo siku ya Ijumaa hasa, kwani Mwenyezi Mungu Alikadiria kujumuisha makundi mbali mbali katika siku hiyo kwa rehema yake kamili. Na itapulizwa baragumu, yaani kwa kuwajumuisha Mwenyezi Mungu Ataonyesha dhihirisho lake, na mara wote watakusanyika katika dini moja isipokuwa wale wenye bahati mbaya kwa utashi wa Mungu na gereza la bahati mbaya likawazuia. Kwenye hii hii Mungu Subhana Aliashiria ndani ya kauli Yake *wa Aakharina Minhum* katika Sura Al-Jumu'ah akiashiria kwenye siku ya Ijumaa ya kweli. Akataka kwa kauli hii kuwa Masihi Mau'udi atakayekuja baada ya Khatamul Ambiyaa ndiye atakuwa ni Muhammad kwa kushabihiana naye kikamilifu, na marafiki zake watakuwa kama masahaba, na huyu huyu ndiye Isa Mau'udi kwa umati huu. Hii ndiyo aliyoahidi Mungu ndani ya Sura At-Tahriim na An-Nuur na Al-Faatiha. Hii ndiyo kauli ya haki wanamoshuku. Haiwezekani kwamba Nabii yeyote aje baada ya Khatamul Ambiyya isipokuwa aliyefanywa mrithi wake kutoka katika umati wake na kupewa jina lake na asili yake, na wajuzi hujua jambo hili. Hivyo, huyu ndiye Masihi wenu

mnayemwona lakini hamtambui, na mwainua macho yenu upande wa mbingu. Je mwadhani kwamba Mwenyezi Mungu Atamrudisha Isa[as] bin Mariamu[as] duniani baada ya kifo chake na baada ya Khatamun Nabiyyin[saw]? Hayawi, hayawi mnayodhania. Na Mwenyezi Mungu Amekwisha ahidi kuzuia ile roho Aliyoikidhia matui, na Mwenyezi Mungu Havunji ahadi yake, lakini nyinyi m watu majahili. Je mnadhani kuwa Yeye Atamtuma Isa[as] duniani na kumfunulia wahyi miaka arobaini na kumfanya Khatamul Ambiyaa na Atasahau kauli yake ***walakin Rasulallahi wa Khataman Nabiyyiina.*** Ameepukana na upungufu na Yu juu kuliko yale mnayomsifu nayo. Nyiye mnayafuata maneno msiyoelewa hakika yake. Kama mngeyarudisha kwenye Mwamuzi kutoka kwa Mungu aliyetumwa kwenu ingekuwa bora kwenu kama mkijua. Ni sikitiko kwenu, mmeichukulia elimu ya dini kuwa visa tu, na mnazozana juu ya msingi huu kwa uchoyo na husuda; na Mungu Amepiga muhuri juu ya nyoyo zenu hivyo hamwoni. Je hamwangalii kwenye silsila mbili zinazokabiliana, au bahati yenu mbaya imewashindeni hivyo hamwoni? Na mnalonga kuwa ndani ya Kurani hamna habari ya Masihi Mau'udi ilhali Kurani imejaa habari zake lakini vipofu hawazioni. Habedari! Laana iwe juu ya waongo wanaokadhibisha Kitabu cha Mungu na kukibadilisha na hawaogopi. Na wanapoambiwa, njooni tukawabainishieni hoja za Mwenyezi Mungu, husema sisi tumeishapata mwongozo, ilhali mikononi mwao

hamna kitu isipokuwa visa vya uongo, na hawanayo takwa. Na wanawafanyia masihara walioamini ilhali wanatambua. Na sio ujaji wangu mwishoni mwa silsila ya Muhammad[saw] isipokuwa kukamilisha mshabaha na kutimiza uzani wa mkabala ili baada ya ushindi wa shetani, Adamu ajaaliwe kushinda.[37] Basi, imekuwaje hawazingatii! Je ilikuwa vigumu kwa Mwenyezi Mungu kumuumba Isa mwingine kama Isa bin Mariamu? Ameepukana na upungufu. Anapoamua kufanya jambo, huliambia, kuwa, nalo huwa. Yeye ndiye Aliyemtuma mithili ya Musa[as] mwanzoni mwa silsila ya Muhammad[saw], hivyo ikawa dhahiri shahiri kutokana nayo kwamba yeye Anataka kumuumba mithili ya Isa[as] mwishowe ili silsila mbili zishabihiane kwa mshabaha kamili. Basi, mmekuwaje hamwamini? Enyi watu, aminini au msiamini, Mwenyezi Mungu Hataiacha silsila

---

[37] Mwenyezi Mungu Alimuumba Adamu na kumfanya kiongozi na hakimu na amiri wa kila mwenye roho yaani watu na majini kama inavyofahamika kutokana na aya ‘*Usjuduu Li Adama*’. Kisha shetani akamtelezesha na kumtoa katika Pepo na utawala akapewa huyu chatu, na katika vita hii Adamu akapata dhila na feheha na soni. Katika vita pengine upande mmoja unashinda na wakati mwingine upande wa pili unakuwa mshindi, na mbele ya Mungu wachamungu ndio hupata mwisho mwema. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akamuumba Masihi Mau‘udi ili Ampe shetani ushinde katika zama za mwisho, na hii ndiyo ahadi iliyopata kuandikwa ndani ya Kurani. Mwandishi.

hii mpaka kuitimiza wala Hatamwacha nyoka wa Adamu mpaka kumuua. Basi, kama mnao uwezo, batilisheni Aliyotaka Mwenyezi Mungu. Je mnakataa neena ya Mungu baada ya kuteremka, Enyi mlionyimika? Na ahadi ya Mwenyezi Mungu imetimia kwa ukweli na haki, basi Enyi wenye kuhasirika, msinunue upotevu. Je mnafanya ubahili katika yale ambayo Mwenyezi Mungu Alimneemesha nayo mja mmoja miongoni mwa waja wake? Je mwaweza kumshinda Mwenyezi Mungu kwa ndimi zenu na hila zenu na mbinu zenu? Basi, jikusanyieni hila zenu zote na waiteni kuwasaidieni waliowapiteni katika hila na uongo na kaeni katika kila njia wala msinipe muhula, nanyi mtaona kwamba Mungu Atawadhalilisheni na kuwarudishieni hila zenu, na hamtaweza kumdhuru hata kidogo wala hamtasaidiwa. Je mnadhani kwamba binadamu ameifanya kazi hii kwa hiari ya nafsi yake? Sivyo, bali ni Mwenyezi Mungu Anayerekebisha ardhi baada ya kuchafuliwa kwake. Je ardhi haikunajisika kwa ufisadi? Mmekuwaje, mbona hamwangalii? Kwa yakini mnaachana na njia iliyo sawa, basi na Mungu Amewaacheni na kuondoa nuru ya mioyo yenu. Na ndivyo walipavyo wakosefu. Je mwastaajabia kwamba Imamu mmoja kutoka miongoni mwenu amewajieni katika zama za mwisho ili silsila mbili ziwe sawa kama vitanga viwili vya mizani. Mmekuwaje, mwawezaje kustaajabia? Ikawa hivyo ili itimie ahadi ya Mungu iliyomo ndani ya Sura At-Tahriim, An-Nuur, Al-Faatiha

na Al-Baqarah. Imekuwaje, hamtafakari. Ishara zimeisha teremka na haki imebainika na dalili wazi zimedhihirika, hata hivyo mnakengeuka. Hamkutaka hoja ila mkapewa hoja tele, hata hivyo hamjizuii. Je hamuioni ardhi yenu namna Mwenyezi Mungu Anavyoendelea kuipunguza mipaka yake, na shingo ziko chini ya mguu wangu huu zikinyenyekea, na watu toka katika kila njia wanakusanyika kwangu? Kama jambo hili lingkuwa minghairi ya Mungu nisingebaki baina yenu miaka thelathini kama mshuhudiavyo na ningalihilikishwa kama wazushi waangamizwavyo. Je nimeleta kitu kigeni, ilhali mlikuwa mkingojea hapo kabla? Na mlilia sana katika maombi ili Mola wangu Anihilikishe kama wapotofu, lakini nilijaaliwa baraka juu ya baraka na maneno yenu yakalaaniwa na dua zenu zikakataliwa moja kwa moja na mkawa wenye kuhakirishwa na kudhalilishwa kwani mlikuwa mnabeza. Mwenyezi Mungu Hatanihilikisha kabla ya kutimia jukumu langu. Ninayo siri fulani na Mwenyezi Mungu wasiyoijua hata malaika, basi Enyi majahili mahasidi, mwawezaje kunitambua? Na daraja yangu mble Yake si kwa sababu ya matendo yangu ya dhahiri wala maneno yangu wala elimu wala kuhojiana, bali kwa sababu ya siri iliyomo moyoni mwangu iliyo nzito kuliko milima. Na siri yangu huwahuisha wafu na kuotesha mimea katika nchi kame na kuonyesha ishara. Basi, je yupo mtafutaji miongoni mwa wenye busara, na je wapo watu watafutao? Nami nimefanywa na Mola wangu kuwa ishara kwa Islam na

hoja toka kwa Mungu Mjuzi sana, na karibuni wakanao wataelewa. Watasikia na wataona vizuri vilioje siku watakayomfikia! Hawa wamemaliza umri wao duniani kama vipofu, wanakumbushwa lakini hawajali. Nimekuja ili kwa amri ya Mola Mwenye Enzi[38] niwapeleke watu toka uwepo kwenye kutokuwepo na kuwaonyesha kiama kabla ya kiama. Na mnaona kwamba magonjwa yanazagaa na watu wanahilikika, na karibuni watu wataonja mauti yaliyo matui ya matamanio yahusikanayo na kutengana na Mungu. Na nimekuja kwa kuwapeleka watu kwenye umoja kutoka kwa wingi, na kwenye mwafaka toka kwa hitilafu, na kwenye kujumuika toka kusambaratika. Na kwa ajili hii vyanzo vimevumbuliwa na milango yake imefunguliwa. Je hamwangalii namna njia zilivyobainishwa wazi na stima ziendeshwavyo baharini, na ngamia wa kike wenye mimba ya miezi kumi walivyoachwa, na habari

---

[38] Maelezo ya pembeni: Tumekariri mara kwa mara kwamba uhamisho toka uwepo kwenye kutokuwepo hautakuwa kwa upanga wala mshale, bali utakuwa kwa amri ya Mungu Mmiliki wa malipo. Kwani, Mwenyezi Mungu Ameandika ndani ya Vitabu Vyake kwamba alama ya kudhihiri Masihi Mau'udi ni kuwa mtasikia habari za vita katika sehemu na maeneo mbalimbali na habari za kutapakaa ugonjwa wa kuambukiza katika nchi mbalimbali. Tena alama mojawapo ya Masihi ni kwamba yeye atawavutia watu kwenye nukta kamilifu ya takwa, na hii nayo ni namna fulani ya kifo. Mwandishi.

zilivyokuwa rahisi kufikishwa, na maoni yanavyobadilishanwa, na nafsi zinavyounganishwa? Na mwaona kwamba watu wanahamishwa kutoka katika dunia hii kwenye mava kwa sababu ya vita ambazo moto wake uliwashwa baina ya wafalme, na kwa namna mbali mbali za magonjwa ya kuambukiza, tena kwa uenezi wa kiini cha mafundisho ya Kurani na uhakika wa Kitabu cha Mungu Rahmani ambao nimetumwa kwa ajili yake katika zama hizi, kwani, mafundiho hayo nayo huita kwenye mauti, yaani kwenye matui yanayoiangukia nafsi kwa kutengana na hali ya kutomjali Mungu na matamanio ya nafsi, na yanaita kwenye kuipoteza ndani ya sheria ya asili, na kwenye hali kama hali ya mtu aliyekufa na kuhilikika, na yanavuta kwenye kutengana kikamilifu na harakati za hiari, na kwenye kuafikiana na fatuwa ambazo moyo hujaaliwa kila wakati kutoka kwa Mwenyezi Mungu Ashushaye takdiri. Na katika hali hii binadamu anajihilikisha dhati yake na haitii amri ya nafsi yake na jazba zake hata kwamba hainasibishwi kwake kutulia wala kutikisika wala kuacha wala kushika, na hali yake inakuwa mbali na mabadiliko. Wala haipatikani ndani mwake alama ya azimio na nia. Huwa hana habari ya kusifiwa au kulaumiwa. Huwa kama wafu. Na hii ndiyo namna ya mauti, kwani mwenye kupata daraja ya matui haya hana hiari ya kutikisika wala kutulia, wala kusikia uchungu wala ladha, wala raha wala taabu, wala huba wala uadui, wala msamaha wala kulipiza kisasi, wala ubahili wala ukarimu, wala woga wala ushujaa, wala

ghaidhi wala upole. Basi yu maiti mikononi mwa Mwenye Uzima, Mhifadhi wa milele, haikubaki ndani mwake hali ya kutikisika wala matamanio, wala hainasibishwi kwake hali yoyote katika hali hizi kama isivyonasibishwa kwa wafu. Na hamna shaka kwamba hali hii ndiyo mauti, na hali hii ndio mwisho wa daraja za utumwa wa Mungu na kuondoka maisha ya kinafsi na kwenye hii huishia safari ya Mawalii wamwendao Mungu Mmoja. Hayo ndiyo mafundisho ya Kurani, na mafundisho mengine yote ya kuvutia kwenye Rahman ni duni kuliko haya. Na hakuna baada yake daraja yoyote miongoni mwa daraja za kumfikia Mungu na kupata maarifa yake mbele ya wenye akili na wenye kutafakari na kuzingatia. Na Torati iliwaelekeza watu kwenye kulipiza kisasi, sawa nayo hamna kimbilio na kusalimika. Na Isa[as] aliuamuru umati wake kwamba mmoja wao akipigwa kofi kwenye shavu moja, basi na amgeuzie la pili pia yule aliyempiga kofi, na asitake kulipiza kisasi. Bila shaka haya makundi mawili hayalingani na sheria ya asili, na yanazifuata tu amri za kanuni. Ama mfuasi wa Muhammad[saw], yeye ameamurishwa kuifuata sheria ya asili pia kama anavyoifuata sheria ya kanuni, na kuhusiana na jambo lolote akate shauri la mwisho baada ya ushahidi wa sheria ya asili, na kwa hiyo Islam imeitwa dini ya asili kwa sababu ya asili kuambatana na dini hii. Na kwenye hii hii Nabii wetu[saw] ameashiria akisema: 'Jiulize fatuwa moyo wako ingawaje mamufti waendelee kukutolea

fatuwa zao.' Basi, tazama jinsi alivyoelekeza kwenye sheria ya asili na hakuridhika na wasemayo maulamaa. Basi Mwislamu kamili ni yule azifuataye sheria mbili, na anaona kwa macho mawili, hapo anaongozwa kwenye njia iliyonyoka, na walaghai hawawezi kumlaghai. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Akieleza sifa bora za Islam Akataja kuwa hii ndiyo dini ya asili aliposema 'Shikeni tabia ya asili ya Mungu Aliyowaumbia watu.'[39] Na hii ndiyo miongoni mwa fadhila za dini hii na sifa bora za sheria hii, kwani ndani ya mafundisho haya tegemeo la kila jambo ni juu ya nguvu takatifu iamuayo ambayo ipo ndani ya mwamko wa pili wa binadamu, inayofikisha kwenye ukamilifu utimilifu katika daraja za kujipoteza ndani ya Mungu. Basi pamoja na hiyo haibaki nafasi yoyote ya madaraka ya kibinadamu, kwani ndani yake itafanywa sawa na ushahidi wa tabia ya asili. Ama Torati na Injili, basi hizi zamwacha mtu kwenye mpaka ulio mbali kutoka kwa ushahidi mtakatifu wa asili na karibu zaidi na kuingiliwa na wingi wa nguvu ya ghaidhi au upungufu wa nguvu ya kifikiria, hata kwamba wakati mwingine mbele ya wenye akili itawezekana kama aitwe mwenye kulipiza kisasi kuwa mbwamwitu muudhi; au aitwe mwenye kusamehe au kufumbia macho pasipofaa — mathalani wakati wa kumwona mkewe akizini — kuwa mtu asiye na haya wala ghera, mbele ya watu wenye kuona haya na ghera. Na kwa hiyo baadhi ya

[39] Sura Ar-Ruum, 30:31

wakati utamwona mtu ambaye mafundiso ya kusamehe yanampendeza anatengana na uhakika wa msamaha na rehema na anaruka mipaka ya ghera ya kibinadamu, kwani msamaha sio wenye kusifiwa kila mahali mbele ya mwenye akili. Kadhalika kulipiza kisasi kila mahala si vizuri mbele ya wazingatiao. Basi, hamna shaka kwamba aliyejilazimisha kila mahali kusamehe kwa kuifuata Injili, yeye baadhi ya wakati akafanya hisani pasipofaa. Na yule aliyejilazimisha kulipiza kisasi kila mahali kwa kuifuata Torati, basi pengine akalipiza kisasi pasipofaa na akaanguka toka kwenye daraja za wema. Ama Kurani, basi hii imeelekeza katika mahali kama hapo kwenye ushahidi wa sheria ya asili ibubujikayo toka katika chemchem ya nguvu takatifu na kuteremka kutoka Roho Mwaminifu ndani mwa nyoyo safi. Kurani inanena: 'Malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao. Lakini anayesamehe na kusuluhisha, basi ujira wake ni juu ya Mwenyezi Mungu.[40] Basi, iangalie nukta hii ya ruhania, kwani hii imeamuru kuisamehe hatia sharti msamaha urekebishe nafsi, la sivyo malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao. Na kwa kuwa Kurani ni *Khatamul Kutub* na kamili kuliko Vitabu vyote na ni bora na vizuri zaidi kuliko Vitabu vyote, hivyo imeweka msingi wa mafundisho yake kwenye kilele cha upeo wa mwisho, na ikaifanya sheria ya asili kuwa mwenzi wa sheria ya kanuni katika hali zote ili kuwakinga watu na upotevu,

[40] Sura Ash-Shuuraa, 42:41

na ikataka kumfanya mtu kama mfu akiwa hatikisiki upande wa kuvuli wala kuuke wala hana hiari ya kusamehe wala kulipiza kisasi isipokuwa kwa hukumu ya masilahi toka kwa Mungu Mwenye jalali. Basi, haya ndiyo mauti ambayo Masihi Mau'udi ametumwa kwa ajili yake ili ayatimize kwa idhini ya Mola Mtendaji bora. Ndiyo sababu nilisema kuwa Masihi Mau'udi atawahamisha watu toka uwepo kwenye kutokuwepo. Hii ndiyo namna ya uhamisho, na habari yake kidogo imeishatangulia. Kuna tofauti kubwa mno baina ya mafundisho haya yenye shani na mafundisho ya Torati na Injili, basi waulize waliokubali wasiwasi wa dajali. Kwa hakika mafundisho haya yanaongoza kwenye yale yaliyonyoka kabisa, hamna ndani yake kuzidi kiasi wala kupunguza, wala hayaachani na masilahi na hekima wala hayapuuzi muktadha wa wakati na hali, bali yanafanya kazi chini ya maamrisho ya sheria ya asili na fatuwa za nguvu takatifu wala hayaachi njia ya wasitani. Na tangu azali ilikadiriwa kuwa Masihi Mau'udi ataeneza barabara mafundisho haya yasifiwayo ili kuwapa wenye bahati njema mauti kabla ya mauti ya Kiama. Basi, hapa watu wema watakufa kwa sababu ya utii kamili. Na mauti haya hujaaliwa kwa nyoyo safi zilizosalimika. Wanakunywa kikombe cha kujipoteza ndani ya huba ya Mungu na wanatoweka ndani mwa bahari ya Umoja wa Mungu baada ya kuvua vazi la kutojihusisha na Mungu. Ama wale walio na bahati mbaya hatimaye wataangukiwa na adhabu toka mbinguni kwa njia ya

aina mbalimbali ya magonjwa ya kuambakiza au kwa vita na kumwagwa damu. Na baina yao yatapita mauti kwa ghafula na matui yafishayo papo hapo kama maradhi yanayowashika kondoo, ikiwa ni takdiri ya Mungu Mtukufu. Vita zitakithiri juu ya ardhi, vita moja ikiisha nyingine itaanza, na mtasikia toka kila upande habari za wafu. Na haya yote yatakuwa hususan kwa uwepo wa Masihi Mau‘udi, kwani Mwenyezi Mungu Amemteremsha kama mwenye kung’olea mbali mizizi. Na hii ndiyo kati ya alama zake kubwa na sifa hasa za dhati yake. Yeye anakabiliana na Adamu katika sifa hizi pamwe na baadhi ya mambo yafananayo. Ama kuhusu mambo yafananayo, haya yanapatikana katika namna ya kuumbwa. Maana Bi Hawa aliumbwa kwa mkono wa kudura kutokana na Adamu namna ya pacha. Kadhalika Masihi Mau‘udi akazaliwa pacha, na pamoja naye akazaliwa mtoto wa kike, jina lake Jannat, aliyefariki baada ya miezi sita tangu siku ya kuzaliwa na akaenda peponi, lakini Hawa hakufa ili awe njia ya kukithiri watu. Kwani Adamu alidhihiri kwa kuwahamisha watu kwenye uwepo toka hali ya kutokuwepo, hivyo ilikuwa haki ya kuwa kwake pacha kwamba aishi ili kumsaidia Adamu kutimiza makusudio. Ama Masihi Mau‘udi, huyu amedhihiri ili kuwahamisha watu kwenye mauti kutoka kwa uhai, hivyo ilikuwa haki ya pacha wake kuondolewa duniani ili awe ni alama ya makusudio yaliyodhamiriwa. Tena Adamu aliumbwa siku ya Ijumaa, na ndivyo alivyoumbwa Masihi Mau‘udi siku hii hii

ndani ya saa yenye baraka. Vilevile Adamu aliumbwa katika siku ya sita, na kadhalika Masihi Mau'udi akaumbwa katika elfu ya sita. Na yale maafa ambayo kudhihiri kwayo kulikadiriwa katika wakati wa Masihi, miongoni mwa makubwa yao ni kutoka kwa Yajuja na Majuja na kutoka kwa dajali potofu. Hawa ndio fitina kwa ajili ya Waislamu wakati wa kuasi kwao na kumkimbia Mwenyezi Mungu Wadudi, na ni balaa kubwa walilotawaliwa nalo kama Wayahudi walivyotawaliwa nalo. Tambua kwamba Yajuja na Majuja ni mataifa mawili yanayotumia moto na ndimi za moto katika vita zao na katika vitu wanavyotengeneza na kwa hiyo wanaitwa majina haya mawili. Mwako ni sifa ya moto, na ndivyo vita yao inavyokuwa kwa kutumia vitu vya kulipuka, na kwa njia hii ya kitali wanawashinda wote wa ardhini. Nao kutoka kila mahali pa juu wanakuja mbiombio, na bahari haiwazuii wala mlima wowote miongoni mwa milima, na wafalme wanaanguka mbele yao wakihofia, wala yeyote hana uwezo wa kukabiliana nao. Na wataendelea kuwakanyaga chini ya miguu yao hadi saa iliyoahidiwa. Yeyote atakayeingia baina ya mawe haya mawili, atasagwa jinsi nafaka inavyosagwa ndani ya kinu hata kama anayo mamlaka makubwa. Ardhi yatetemeka vikali kwa sababu yao na milima yatikisika, na upotevu unaenezwa, na dua yote haisikilizwi wala kilio chochote hakipati kuwasilia arshi. Na msiba unawasibu Waislamu unaoendelea kula mali zao na heshima zao na daraja

zao. Na siri za wafalme wa Kiislamu zinatobolewa na huwadhihirikia watu kuwa wanaangukiwa na ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya uasi wao na hatia zao. Wamenyanganywa heba yao, heshima yao, shani yao na jalali yao kwa sababu hawashiki takwa. Wanakabilana na adui kwa njia moja na wanapata kushindwa kwa njia saba kwa sababu hawafanyi wema. Wanajionyesha kwa watu na hawamfuati Mtume[saw] wa Mungu na suna yake wala hawashikamani na dini barabara. Hawa ndio taswira tu pasipo roho ndani mwao. Hivyo, Mwenyezi Mungu Hawaangalii kwa rehema wala hawasaidiwi. Na Mwenyezi Mungu Anataka kupokea toba yao ikiwa wananyeyekea. Lakini hawakutubu wala hawakujinyenyekeza, basi adhabu itawaangukia wakosefu isipokuwa wale wanyenyekeao. Wataona siku za misiba na mausiku yake kama walivyoona waliolaaniwa. Hapo ndipo atakaposimama Masihi mbele ya Mola wake Jalia na kumwomba usiku mrefu kwa vilio na huzuni na atayeyuka jinsi theluji iyeyukavyo juu ya moto, na ataomba kwa kulia sana mno kwa sababu ya msiba uliozingukia nchi, na atamkumbuka Mungu kwa machozi yatiririkayo na kumchuruzika usoni. Hapo dua yake itasikilizwa kwa sababu ya daraja yake mbele ya Mungu na watateremka malaika wenye kuhami, basi Mungu Atafanya Atakayoyafanya na kuwaokoa watu katika maradhi ya kuambukiza. Wakati ule Masihi atatambuliwa ardhini kama alivyotambuliwa huko mbinguni, na ukubali wake utatiliwa nyoyoni mwa watu

wa kawaida na maamiri, na wafalme watatafuta baraka katika nguo zake. Haya yote yatakuwa toka kwa Mwenyezi Mungu na mintarafu yake, na yatakuwa ya ajabu machoni mwa watu. Basi, tafakari ndani ya Kurani na Hadithi kama unashuku. Na sikusema haya kutoka kwangu, bali ndio itikadi ya Waislamu Masalih na imeandikwa ndani ya kitabu cha Mola wa walimwengu.

## Hali iliyopo yamwita Masihi Mau'udi na Mahdi Mau'udi

Kwa yakini ardhi imejaa dhuluma na ujeuri, na ufisadi umeuzingira kila mteremko na mwinuko na kweli zimeondoka mahali pake na nukta nyepesi za kielimu zimetengana na vituo vyao, dini imevulia mbali vazi la mapambo yake, na sheria imetia upanga wa shani yake ndani ya ala yake, na siri zake za batini na alama za uwepo wake zimepotea. Na damu za wanawe na wajukuu wake zilimwagwa mpaka mbingu ikawalilia wanawe kufa kwao na ugeni wake. Kila kiungo chake kimepata kuugua na kila mwanamke wake mwenye watoto wengi amekuwa tasa. Sasa hii ndio ajuza aliyepotewa na nguvu zake na ni bikizee ambaye sura yake na uangavu wake umegeuka, ulimi wake una kigugumizi kilichomshinda, meno yake yanao ukoga. Je dini hii ilikuwa ni dini aliyoileta Khatamun Nabiyyina[saw] Aliyoikamilisha Mola wa walimwengu? Sivyo kabisa! Bali imechafuliwa na mikono ya wenye bidaa walioifanya Kurani kuwa mkusanyiko wa uongo. Wakapotea na kuwapoteza wengine na hawakuwa wenye kufahamu. Hawa ndio watu wasiomiliki kitu isipokuwa ganda wala hawatambui lubu ya uhakika ni nini, juu ya haya wanajidhania kuwa miongoni mwa wenye elimu, bali masheikh wakubwa wa dini. Ndimi zao zaeleza visa tu vile walivyobuni mababu zao, na hawakubakiwa na kitu ila matarajio yao na matamanio yao. Misikiti yao imejaa wale watu wasiotambua siri za

ibada na wanajadiliana kuhusiana na maneno waliopata kusikia toka kwa kundi lenye hatia. Hawajakanyaga mitaa ya ruhania. Wanasali wasielewe hakika ya sala, wanasoma Kurani wasifahamu Neno la Mola wa ulimwengu. Haki imedhihiri wasitambue. Na Mwenyezi Mungu amemtuma Masihi wake wasimkubali, bali humhakirisha na hawamheshimu wala hawamjii wakiwa waaminio. Ukweli ulipowajia wakakataa ilhali hapo kabla walikuwa wanaungojea. Waambiwapo, Enyi watu, ikimbilieni heri, na msizifuate nyayo za shetani atiaye wasiwasi nyoyoni na kurudi nyuma, husema nyinyi m wapotevu. Walinikadhibisha pasipo kuchunguza ipasavyo kuchunguza. Na wananipita wakitakabari. Wamesahau yote iliyowasihi Kurani na hawajui Aliyoyateremsha Rahmani na wanapoteza umri wao katika hali ya kughafilika. Kama wangeifahamu Kurani wangenitambua, lakini wametupa Kitabu cha Mungu nyuma ya migongo yao wakijasiri. Husema, hukutumwa wewe ilihali Mwenyezi Mungu Anatosha na aya zake kuwa shahidi kama wangekuwa watafutaji wa haki. Wameweka wakfu ndimi zao kwa kutukana na kudhalilisha. Wakataka kupata msaada wa zile riwaya dhaifu zisizo za yakini hata chembe kwa kuipinga Kurani. Na Mwenyezi Mungu ameng'arisha haki, lakini hawasikii, na Akaondoa pazia kwenye siri, lakini hawajali. Wamesoma Kurani, lakini hawakupata habari ya siri za dafina zake. Wametiwa silisili za maneno ya Kurani na hawakupewa funguo za hazina zake zilizofungwa.

Hivyo, yawezekanaje warejee salama kutoka katika njia hii. Basi, wakapindamana na kuacha njia ya kuhakiki wala hawakuonja hata funda moja la kinywaji halisi wala hawanayo busara. Kisha Mwenyezi Mungu Aliponifanya kuwa Masihi Mau'udi na Akanituma kwa ukweli na haki wakati wa haja, wakaanza kunikadhibisha na kunikufurisha na kunitaja kwa kunikebehi na hawakujizuia. Jua la zama hizi limekurubia kuzama, na nyoka wa uhai amekusudia njia zake na haikubakia katika dunia ila nafasi ndogo tu. Je wanataka kuwa muhula wa shetani urefushwe? Na zama zetu hizi ni zama za mwisho na hizi zimewahilikisha watu wengi mpaka sasa. Na hapo kabla Adamu alianguka katika medani ya vita na shetani Akamshinda na hakuona ushindi hadi miaka elfu sita. Dhuria zake wakapondwa vipande vipande na wakasambaratishwa kila upande. Basi, mpaka lini shetani atapewa muhula? Je hajawapoteza watu wote isipokwa waja Masalih wa Mungu walio wachache? Yeye ameishatimiza jukumu lake na kukamilisha kazi yake, na sasa wakati umewadia kuwa Adamu asaidiwe na Mola wa walimwengu. Na hakuna shaka wala wasiwasi kwamba muhula wa shetani ulikuwa mpaka zama za mwisho kama inavyofahamika toka katika Kurani, yaani neno *Indhaar* — nafasi, muhula — lililomo ndani ya Kurani, kwani Mwenyezi Mungu akamwambia kwa kusema: 'Haya, hakika umekuwa

miongoni mwa waliopewa nafasi mpaka wakati wa siku maalum.’[41] Yaani siku ya kufufuliwa ambayo ndani yake watu watafufuliwa katika mauti ya upotevu kwa idhini ya Mungu Mwenye Uzima, Mhifadhi wa milele. Bila shaka siku hii ndiyo siku iliyofanana na siku ya kuumbwa Adamu, kwani Mwenyezi Mungu Alitaka ndani yake amuumbe aliye mithili ya Adamu, kisha atapakaze ardhini dhuria zake wa ruhania na kuwapa ushindi juu ya kila aliyekata uhusiano wake na Mungu, na akikatika akatengana Naye. Yasikika haja sana ya ujaji wa Adamu wa Pili ndani ya zama za mwisho ili alipie kilichoponyoka zama za awali na kwamba litimie onyo la Mungu kuhusiana na shetani. Kwani, Mwenyezi Mungu Akamfanya kuwa miongoni mwa waliopewa nafasi hadi mwisho wa dunia, na Akaashiria ndani yake kumhilikisha na kumfukuza katika mamlaka yake. Na kuna maana gani ya kumpa muhula pasipo kumwonya kwamba atauawa baada ya siku za nafasi na kukaa duniani? Na kuhilikishwa kwake ni adhabu yake kwa sababu yeye aliwaangamiza watu kwa fitina zake kubwa na elfu ya saba ilikuwa ni wakati uliowekwa kwa kumuua. Yeye akawaingiza watu ndani ya jahanamu katika milango yake saba na kutimiza haki ya upofu wake. Hivyo, elfu ya saba yaafikiana sana na milango saba. Na Mwenyezi Mungu Alikwisha andika kuwa yeye atauawa katika sehemu ya mwisho ya dunia na ndipo

[41] Sura Saad 38:81-82

watoto wa Adamu watajaaliwa uzima kwa rehema ya Mungu Mtukufu, na atapatwa na ushinde mkubwa sana kama alivyopatwa nao Adamu zama za mwanzo. Na hapo itakuwa ni kulipiza kisasi, mtu kwa mtu na heshima kwa heshima. Na ardhi itang'aa kwa nuru ya Mola wake, na adui wa Adam, mteule wa Mungu, ataangamia. Ndivyo inavyokuwa adhabu ya uadui wa wateule. Na ushindi huu ulikuwa haki na wajibu kwa Adamu, kwani shetani alimshinda katika sura ya chatu na kumtupa ndani ya shimo la dhila na akavunja mgongo wake baada ya Mwenyezi Mungu kumpa heshima. Na lengo la Iblisi lilikuwa ni kumuua na kumhilikisha na kumng'olea mbali na akataka kumtowesha yeye na dhuria zake na ali zake. Hivyo akahukumiwa kutoka kwenye mahakama ya kadiri ya Mungu kuuawa baada ya siku za muhula, na kwenye hii hii Akaashiria Mungu Subhana katika kauli yake '*Ilaa Yaumi Yub'athuun'* kama wajuvyo wanaotafakari. Hii haimaanishi kuwafufua wafu bali muradi wake ni wapotevu kujaaliwa uzima baada ya upotevu wao, na inaiunga mkono kauli hii ya Mwenyezi Mungu iliyomo ndani ya Kurani: 'Ili kuifanya ishinde dini zote',[42] kama isivyofichika juu ya wenye akili na maarifa. Kwani, kuishindisha dini juu ya dini zote inahakikika tu kwa ishara kubwa na hoja madhubuti na kukithiri watu wema na wacha Mungu. Na hakuna shaka kwamba ile

[42] Sura As-Saff 61:10

dini inayojaaliwa dalili zifikishazo kwenye yakini na kuzitakasa nafsi ipasavyo kutakasa na kuwaokoa katika kucha za shetani mlaaniwa ndiyo dini inayozishinda dini zote na ndiyo iwafufuayo wafu katika makaburi ya shaka na uasi na kuwahuisha kielimu na kimatendo kwa fadhili za Mungu Manani. Na Mwenyezi Mungu alikuwa Amekadiria kwamba dini yake haitapata ushindi kamili juu ya dini zote wala hazitajaaliwa nyoyo dalili za haki isipokuwa katika zama za Masihi Mau‘udi na Mahdi aliyeahidiwa. Ama zama zililzo kabla yake, takwa haitakuwa kwa wingi kwa ujumla wala ufahamu, bali ufasiki utakithiri na upotevu. Kwa ufupi, basi, ni kwamba mwongozo mpana kwa ujumla na hoja madhubuti timilifu zahusiana na zama za Masihi Mau‘udi kutoka kwa Mungu Mtukufu. Na katika zama zile kweli zilizofichika zitafichuka na uhakika utaondolewa pazia na mila za batili zitaangamizwa na dini za uongo pia. Na Islam itashinda mashariki na magharibi, na haki itaingia ndani ya kila nyumba kwa kuacha wakosefu wachache. Na kazi itatimia na Mwenyezi Mungu Ataondoa vita, na amani itapatikana juu ya uso wa ardhi na utulivu na suluhu itateremka ndani mwa nyoyo. Wanyama mbuai wataacha ukatili wao, na nyoka sumu zao. Mwongozo utabainika na upotevu utaangamia, wala haitabaki katika kufuru na ushirikina isipokuwa alama tu kidogo. Moyo unaougua tu utabaki kuambatana na ufasiki na ubaya. Wapotevu watapewa mwongozo na waliozikwa makaburini

watafufuliwa. Basi hii ndiyo maana ya kauli yake: '*Ilaa yaumi Yub'athuun*.' Ufufuo huu ndio ufufuo wasiouona watu wa awali wala mitume waliopita wala manabii wote. Na ingawaje dini ya Mungu ki-nguvu na kiuwazo ilizishindi dini zote, lakini hapo kabla haikutokea kwamba ikabiliane na dini zote kwa hoja na dalili za kutegemewa na kuzishinda kabisa na kuthibitisha kwamba hizo zimejaa uborongaji, na kwamba ijitokeze kama mashujaa kwa silaha za hoja mpaka ienee katika miji yote na nchi zote, lakini hii ilikuwa takdiri ya Mungu Wadudi na Alikwisha tangulia kusema ushindi kamili na suluhu kuu kwa ujumla yahusikana na zama za Masihi Mau'udi. Na ndiyo sababu shetani alipewa muhula hadi zama hizi zenye baraka, hivyo Mungu Akampa nafasi ili yatimie yote Aliyokusudia kwa walimwengu. Hivyo, shetani akawapoteza wote waliomfuata. Basi wakakata jambo lao baina yao sehemu sehemu, kila kundi likifurahia waliyo nayo, na hawakubaki juu ya njia iliyo sawa isipokuwa waja Masalih wa Mungu.

Na siri ndani mwake ni kwamba zama zimegawanywa katika namna sita toka kwa Mungu Aliyeumba ulimwengu katika nyakati sita, nazo ni hizi: Zama za Mwanzo, Zama za kuongezeka na kupata kukua, Zama za ukamilifu na upeo, Zama za kurudi nyuma na kupungukiwa uhusiano na Mungu na upungufu wa ufungamano, Zama za mauti kwa upotevu wa aina aina na Zama za ufufuo baada ya mauti. Kwa yakini mfano wa watu, mbele ya Mwenyezi Mungu, tangu wakati wa

Adamu mpaka zama za mwisho ni kama mfano wa mmea utoao chipuko lake, kisha hulitia nguvu na ukavimba ndipo ukasimama sawasawa juu ya bua lake, kisha ukawa kimanjano, tena kwa idhini ya Mungu unaanza kuanguka, kisha mazao yakavunwa na ardhi ikabaki tupu. Tena Mwenyezi Mungu Akaihuisha baada ya kufa kwake, na lo ikawa yenye rutuba na ikaotesha mimea ikistawi na kuwa chanikwiti, na macho ya wakulima yaburudika. Ndivyo Alivyopiga Mwenyezi Mungu mfano wa walimwengu. Hivyo, imethibitika katika sehemu hii kwamba zama za mauti ya ruhania zilikadiriwa toka kwa Mola wa walimwengu. Na ikakadiriwa kwamba watu wote katika elfu ya sita watapotea isipokuwa wachache walio Masalih. Ndiyo maana shetani alisema lazima nitawapoteza wote. Kama hii isingekuwa imekadiriwa, asingejasiri maluuni huyo kutamka maneno haya. Na kwa kuwa alielewa kwamba Mwenyezi Mungu Amekwisha weka nyuma ya zama hizo zama za ufufuo na mwongozo, ufahamu na uelewa, basi akasema: '*Ilaa Yaumi Yub'athuun*'. Kwa kifupi, miongoni mwa zama zote, zama za mwisho ni zama za ufufuo kama waelewavyo wenye elimu. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akagawanya elfu sita katika zama sita, na Akaweka Kiama katika sehemu fulani ya elfu ya saba. Na zilipofika elfu ya sita zilizo zama za kufufuliwa toka kwa Mwenyezi Mungu, ikatimia kazi ya kupoteza, na watu wakawa makundi mengi kwa sababu ya shetani dhalili. Uasi ukazidi na makundi mbalimbali yakawa

yasiyotawalika kama mfuro wa mawimbi mazito. Upotevu umekuwa mrefu kwenda juu kama milima, na watu wakafa kwa mauti ya ujahili na ufasiki na maovu na kutojali, na mauti yakaenea ndani ya mataifa yote na nchi zote na pande zote. Hapo ndipo Mwenyezi Mungu Alipoona kuwa wakati wa ufufuo umewadia na wakati wa mauti umefikia mwisho wake, basi, Akamtuma Mtume wake jinsi suna yake iivyoendelea katika karne za awali, ili kuhuisha wafu, na hii ilikuwa ni ahadi isiyokuwa na budi kutimia, kutoka kwa Mola wa mahuluku. Basi Masihi huyu huyu ndiye Khatamul Khulafaa na mrithi wa Manabii, na Imamu aliyetazamiwa kuja toka kwa Mungu Mtukufu, na Adamu ambaye kwa njia yake Mwenyezi Mungu Ameanzisha mara ya pili silsila ya kuhuisha. Na Mwenyezi Mungu Amemwita jina 'Ahmad' kwani kwa njia yake Mola Jalali Atahimidiwa ardhini kama Anavyohimidiwa mbinguni. Na pia amemwita 'Isa bin Mariamu' kwani Akaumba ruhania yake toka kwake Mwenyewe, na kulikuwa hakuna juu ya ardhi sheikh wake kama baba zake. Na akapewa lakabu ya Isa aliye Masihi kwa sababu juu yake ulimalizika Ukhalifa wa Nabii[saw] wa nyimati zote, Mbora wa Wateule, jinsi Ukhalifa wa silsila ya Musa[as] ulivyoishia kwa Isa[as] kutoka kwa Mungu Mtukufu, na pia kwa sababu hii kwamba jina lake litaenea kote ardhini na atakumbukwa katika kila kaumu kwa heshima na utukufu. Yeye atadhihiri upande mmoja kama umeme tena atang'ara katika pande zote na kuangaza anga lote

la mbingu, na pia kwa sababu ilikwisha andikwa tangu azali kwamba ataigusa mbingu kwa kuziondolea pazia kweli nyingi. Katika zama zake nukta yoyote haitabaki kufichika. Basi hizi ni sababu tatu za kumuita aliye Khatamul Khulafaa kuwa Masihi. Basi tafakari ndani yake ikiwa u miongoni mwa wenye busara. Kwa yakini yeye amepata baraka za Nabii[saw] wake anayemiliki sifa hizi tatu kikamilifu. Hivyo, acha kumtaja Isa[as] na mwamini kivuli cha Mbora[saw] wa Mitume wote na Khatamul Ambiyaa. Na mbele ya Mwenyezi Mungu, miongoni mwa mambo ya muhimu mojawapo lilikuwa ni kuzifanya zama za mwisho kuwa zama za ufufuo, yaani zama za kujadidisha silsila ya kuhuisha. Hii ndiyo kweli, basi usibishane kama majahili. Na kadhalika miongoni mwa makusudio makubwa ya Mungu kulikuwa ni kumhilikisha shetani kabisa na kumrudishia Adamu ushindi mara nyingine na kujaza ardhi uadilifu na unyoofu na baraka za namna namna na neema, na kuyaondolea pazia mambo yote ya hakika. Pia Atafikisha jambo lake na yule aliyetumwa Naye kwenye pande zote, na Atadhihirisha jalali Yake na *jamali* Yake ardhini na Atatumia kila njia kwa kutimiza jambo hili. Basi, Yeye Akamsimamisha mtumishi kutoka kwake kwa shabaha hii na kwa kujadidisha sheria njema, na Akamfanya miongoni mwa Bani Farisi toka kuumeni, na miongoni wa Bani Fatima kuukeni, ili kujumuisha ndani yake jalali na *jamali* na kumwekea sehemu moja bora sana ya sifa za wanaume na sehemu moja bora

sana ya sifa za kike, maana watakuwepo ndani ya Bani Farisi mashujaa watakaorudisha imani toka mbinguni. Na ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Akaniita Adamu na Masihi aliyeonyesha mfano wa Mariamu katika kuumbwa, pia Akamuita Ahmad aliyetangulia katika fadhila, ili Adhihirishe kwamba Amejumuisha ndani ya nafsi yangu kila shani ya Manabii kama hiba na kipaji. Na hii ndiyo haki wanayohitilafiana ndani yake. Hatarejea Adamu duniani wala Nabii wetu mtukufu[saw] wala Isa[as] mfile aliyetuhumiwa. Mwenyezi Mungu Ameepukana na upungufu na Yu juu sana kuliko mnayomtungia uongo. Je hizi si zama za mwisho? Mmekuwaje, mbona hamtafakari? Je Saa haijakaribia kwa kudhihiri Nabii wetu[saw], na alama zake hazijadhihirika? Basi mtakimbilia wapi? Mmekuwaje mnazisukuma habari toka kwenye nyakati zao na kuziahirisha ilhali mnajua? Je mmeisahau Hadithi بُعِثْتُ اَنَا وَالسَّاعَةُ كَهَاتَيْنِ — mimi nimetumwa na Kiama kama vidole hivi viwili. Imekuwaje, basi, kwani mnakufuru? Kiguseni kidole cha shahada na kidole cha kati na kumbukeni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Lakini hawakumbuki isipokuwa wale waelekeao kwa Mungu. Nami nimekuja ndani ya elfu ya saba ambayo ndiyo siku ya kuumbwa kwa Adamu. Kwa yakini ndani yake mna mwongozo kwa wazingatiao. Je hamsomi Sura Al-'Asr na ndani yake umebainishwa umri wa dunia katika idadi zake tangu Adamu mpaka Nabii wetu[saw] kwa watu wanaofahamu. Na huu ndio umri wanaoutambua watu

wa Kitabu, basi waulizeni ikiwa hamjui. Hamna hitilafu baina ya idadi za Sura Al-'Asr na hesabu yao isipokuwa tofauti ile iliyopo baina ya kalenda ya jua na kalenda ya mwezi. Kama mkishuku, basi hesabuni wenyewe. Na kama jambo hili limehakikika, basi jueni kuwa nilizaliwa mwisho wa elfu ya sita sawa na hesabu hii. Na hii ndiyo siku ya Adamu kuumbwa, na kwa Mola wetu siku moja ni kama miaka elfu sawa na mnavyohesabu. Na kama mnashuku katika yale tuliyoandika, yaani tangu silsila ya Adamu hadi siku yetu hii imebaki miaka elfu moja au na miaka michache zaidi kidogo, basi njooni tuithibitishe kutoka katika Kitabu cha Mungu na Hadithi na Vitabu vya Manabii wa zamani. Kwani thamani za herufi za Sura Al-'Asr, sawa na hesabu ya *Jummal*, kama iivyofichuliwa kwangu na Mungu Wahabu na jinsi zinavyofululiza riwaya za Watu wa Kitabu, zinaongoza kwenye jambo hili kwamba tangu Adamu, Nabii wa kwanza mpaka zama za Khatamul Ambiyaa[saw] ilikuwa imepita miaka elfu tano, isipokuwa miaka michache, na haikubaki katika elfu ya tano ila kidogo kuliko miaka mia mbili,[43] na kutoka katika Hadithi ya Mimbari yenye

[43] Zile kauli zinazohitilafiana na hesabu hii, na wataalamu wa zamani wamezitaja, ndizo kauli ambazo baadhi yao zabatilish baadhi nyingine. Hawakuafikiana juu ya neno moja, bali wanahangaika katika kila bonde. Hivyo haifai kuzishika kauli zao baada ya Kurani na Manabii wa zamani kuafikana juu ya hesabu hii. Mwandishi

vipago saba inafahamika ile ile maana tuliyoieleza katika mahali pake kwa wasomao. Na ilipothibitika kwamba kiasi hicho katika umri wa dunia kilikuwa kimeishapita mpaka zama za Mtume[saw] wa Mungu, Mbora wa mahuluku, basi na imethibitika pamoja nayo pia kwamba kiasi kilichobaki ni kidogo sana kulingana na kiasi kilichopita. Kurani imeieleza habari hii mara kwa mara kwamba Saa iko karibu, hamna shaka ndani yake, na ikasema: 'Imewakaribia watu hesabu yao'[44] na ikasema: 'Saa imekaribia'[45] na ikanena: 'Basi alama zake zimeisha kuja.'[46] Kadhalika zipo aya zingine pia kuhusiana na jambo hili. Hivyo, imejulikana kutokana na hizi kwa yakini kabisa, Enyi wenye akili, kuwa sehemu kidogo ya umri wa dunia inabaki kulingana na zama zilizoishapita hata kwamba alama za Saa zimedhihirika na siku ya ahadi imesogea karibu na wakati uliotazamiwa kuja umekwisha wadia, na wakati uliopita umekwenda mbali. Basi rudisha macho, je waona ndani yake uongo? Na amani iwe kwa yule aufuataye mwongozo. Na umeelewa kwamba muda uliopita tangu wakati wa Adamu hadi zama za Nabii wetu Mteule[saw] ulikuwa karibu miaka elfu tano na Kurani imeshuhudia juu yake, na watu wa Kitabu pia wameafikiana juu yake pasipo kuhitilafiana. Basi kadirio gani lililo dogo kuliko

---

[44] Sura Al-Ambiyaa 21:2

[45] Sura Al-Qamar 54:2

[46] Sura Muhammad 47:19

kadirio hili? Je huu sio wakati wa mwisho wa Alasiri? Tujibu kwa uadilifu. Lau kama uepe kukubali hii, hata hivyo huna budi kukiri kwamba muda uliobaki ni kidogo hata kuliko nusu bila hitilafu yoyote. Basi juu ya kwenda kombo umekubali madai yetu kwa kauli yako hii. Hivyo unalazimika kukiri kwamba katika muda wa zama za Adamu mpaka zama za Mtume[saw] wa Mungu muda uliobaki ulikuwa miaka elfu mbili na miaka mia chache, na haya haya ndiyo madai yetu. Basi sifa zote njema zamhusu Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu. Twasema kwamba tumetumwa mwanzoni mwa elfu ya mwisho miongoni mwa maelfu ya silsila ya ***Abul Bashar***[47] — Adam[as] — na hatima ya elfu ya sita kwa idhini ya Mungu, Mrehemevu kuliko warehemevu wote. Na hizi ni zama za Masihi aliye Adamu wa zama za mwisho. Na hii hii ndiyo hoja yangu uliyoikiri tayari, Ewe adui! Basi uangalie kuwa umebanwa barabara, na ndivyo abanwavyo kila anayetengana na wenye maarifa. Na Mwenyezi Mungu hakutuambia wakati wa Kiama, bali Ametuambia tu kwamba ndani ya elfu hii kitatokea,

---

[47] Katika baadhi ya ibara za kitabu chetu hiki badala ya kueleza neno 'hatima ya dunia' tumeandika neno 'mapinduzi makubwa' au 'kukatika silsila ya Adamu' au ibara nyingine. Sababu yake ni kuwa habari ya Saa imefichika na minghairi ya Mungu hakuna ajuaye maelezo yake. Hivyo, kinaya ni karibu zaidi na takwa. Twaamini mageuko makubwa kutokea baada ya muda huu na twamwachia maelezo yake Mola wetu Mtukufu. Mwandishi.

na Akatuarifu baadhi ya habari zake na Hakutuambia baadhi nyingine. Hivyo hatuna elimu ya wakati wa Kiama, wala malaika yeyote huko mbinguni hajui. Nasi hatuelewi uhakika wa Saa; twajua tu kwamba hii itakuwa ni mapinduzi makubwa na siku ya malipo, na maelezo yake twamwachia Yule Mjuzi Ajuaye uhakika wa mwanzo na wa mwisho. Twarudia tena kauli na twasema kwamba Mwenyezi Mungu Alifananisha zama za Mtume[saw] wa Mungu na wakati wa Alasiri. Ukitaka, usome ndani ya Kurani Sura Al-'Asr. Kadhalika habari za Alasiri zimekuja katika Hadithi Sahihi na *Akhbar* za kutegemewa zilizofululiza, mpaka zinapatikana ndani ya Bukhari na Muwatta' na vitabu vingine vya kutegemewa. Na siri ndani ya tashbihi hii ni kwamba Mwenyezi Mungu Alimtuma Musa[as] baada ya kuhilikisha vizazi vya kwanza na kumfanya kuwa Adamu kwa umati mpya na Akamfunulia wahyi Aliyoifunulia, na silsila ya dini yake ikakatika baada ya miaka elfu na mia tatu na kidogo zaidi. Ndivyo Alivyoamua Mwenyezi Mungu. Kisha Akamtuma Isa[as] ili awakumbushe wana wa Israeli waliyoyasahau katika mafundisho ya Torati na kuwatilia shauku ya huluka njema, na silsia ya dini yake iliishia katika muda uliokuwa takraiban nusu ya muda wa silsila ya Musa[as] kisha Akamtuma Nabii Wake Muhammad[saw], Mbora wa mahuluku na Mtume wake Mteule, juu yake rehema za Mungu na amani na baraka zake kubwa. Na Akaendeleza silsila ya wafuasi wake bora mpaka muda

uliokuwa nusu ya nusu aliopewa Isa[as], yaani karne tatu zilizokwisha katika miaka mia tatu baada ya Seyidna Mteule[saw]. Basi zama za Musa[as] zafanana na mchana mzima, na idadi ya mia zake yafanana na idadi ya masaa ya mchana. Na zama za umati wa Isa[as] zafanana na nusu ya mchana. Ama zama za watu bora wa umati wa Mbora[saw] wa Mitume wote, waliokuwa mpaka karne tatu, hizo zinafanana na nusu ya nusu ya mchana, yaani wakati wa Alasiri ulio masaa matatu katika siku za urefu wa wasitani. Kisha baadaye ukaja usiku wenye kiza kinene sawa na takdiri ya Mungu na hekima yake, nao ulikuwa umejaa dhuluma na ujeuri, nao uliendelea hadi miaka elfu. Kisha likachomoza jua la Masihi Mau'udi kwa fadhili za Rahmani. Basi, hii ndiyo maana ya Al-'Asr iliyotajwa ndani ya Kurani na huu ndio uhakika wa Al-'Asr uliotudhihirikia. Lakini pamoja na hii, ukaribu wa Kiama pia ni jambo la haki sahihi lithibitikalo toka ndani ya Kurani. Na Kurani inazo jiha mbalimbali za maelezo, na hii ndiyo jiha mojawapo, na jiha zote mbili ni sawa ukizingatia, na haikani ila jahili, kipofu, mwenye chuki na aliye asira ndani ya mapazia ya udhalimu, kwani ile maana tuliyokwishaeleza kabla katika maelezo inaondolea mbali baadhi ya mushkili unaowatatiza moyoni baadhi ya wenye kiu ya maarifa, kwa sababu ya kufululiza kwa wasiwasi wa shetani. Isitoshe, hii maana inaitetea Hadithi ya Bukhari na Muwatta' dhidi ya masuto ya asutaye na shutuma za mwenye kushutumu ambaye saa zote anakuwa na silaha za kuaibisha. Na

upinzani wenyewe ni kwamba inawezekanaje kuwa zama za Islam zishabihiane na wakati wa Alasiri ilhali zama za dini hii ni sawa na dini ya Musa[as] na ni zaidi ya dini ya Isa[as], bali mpaka wakati huu wa Alasiri zimezidi zaidi ya mara mbili kuliko zama zake. Basi kuna maana gani ya Alasiri kulinganishwa na zama ziilzotajwa? Bali maelezo hayo ni batili wazi wazi na ni miongoni mwa namna mbaya sana za uongo. Kwa hakika upinzani huu umezidi kuliko mipaka iliyokatazwa. Kwani, habari za ushukaji wa Isa[as] na kutoka kwa dajali na Yajuja na Majuja ambaye watu wengi wanamngojea, uongo wake umedhihiri dhahiri shahiri kwa maelezo haya. Maana wakati wa Alasiri umeishapita, bali bila shaka umepita mara nne kuliko huo kwa kuangalia zama za dini ya Musa[as]. Basi haukubaki wakati ili kudhihiri matabiri haya na wangojeao wamelazimika kusema kwamba haya ni batili kwa hakika. Na haikubaki njia ya kuyasadikisha isipokuwa isemwe kwamba matabiri haya yameishatimia tayari, na ameisha teremka Isa[as] aliyetazamiwa kuteremka na Dajali mwenye kutoka amekwisha toka na Yajuja na Majuja wamekwishadhihirika na imehakikia kuja kwao mbiombio toka kila mwinuko na wamefikia upeo wa maendeleo, na habari zote zimetimia tayari ziizokadiriwa na mitume wamekwishaletwa katika wakati uliowekwa. Na kwa kutazama kikomo cha karne tatu tusemapo kwamba zama za umati wa Musa[as], baina ya nyimati hizi tatu, ni ndefu zaidi, na zama za Isa[as] zilikuwa nusu yake, na nusu ya nusu zilikuwa kwa

Masalih wa umati huu, basi upinzani huu umebatilika, na anafunuliwa uhakika yule atafutaye haki kwa tabia salama na nia safi. Na yathibitika kwa yakini kwamba zama za umati uliorehemiwa wa Muhammad[saw] ni ndogo kwa hakika kuliko zama za umati wa Musa[as] na Isa[as].[48] Na hii ndiyo hisani yetu juu ya wapinzani watokanao na madhehebu ya Waislamu. Na hamna shaka iliyobaki ndani ya maelezo haya kwa mwenye akili, bali ni sababu ya kuburudisha na kutuliza. Na pamoja nayo unabatilika upinzani uhusianao na Hadithi ya umri wa Manabii. Kwani umri wa Isa kwa jiha ya

---

[48] Mtume[saw] wa Mungu amebainisha kuwa muradi wa nyimati zilizopita kabla ni Wayahudi na Manasara, basi mbishi hana njia iliyobaki. Je hukusika kauli ya Mtume[saw]: *'Faman'*! Basi fikiri na zingatia. Kisha twasema *kwa kujiteremsha chini* kwamba wakati wa kutumwa kwa Nabii wetu Mteule[saw] ulikuwa kama Alasiri kwa kulinganishwa na nyimati nyingine. Kwani, elfu ya tano kwa kulinganishwa na umri wa dunia — yaani elfu saba — hufanana na mnasaba upatikanao kwa wakati wa Alasiri ambao umeishapita bila hitilafu yoyote. Na hii ndiyo hivi kwamba mchana unapochukuliwa kuwa wa masaa saba kwa kuangalia katika baadhi ya sehemu wakati baina ya jua kucha na kuchwa ni kidogo, nawe wajua kuwa mchano ndio kiasi hiki katika baadhi ya nchi za mbali kama isivyofichika kwa wenye akili. Nasi tumechukua mchana katika sura ya kwanza kuwa wa masaa zaidi, na katika sura ya pili masaa machache, na tunayo hiari kama ujuavyo. Mwandishi.

kubaki dini yake ulikuwa nusu ya umri wa Musa[as] kama ilivyodhihiri bila kufichika, na umri wa Seyidna Mbora[saw] wa mitume kwa kutazama karne tatu ni nusu ya umri wa Isa bin Mariamu[as] waziwazi. Kisha baadaye ziko siku za mauti ya Islam hadi miaka elfu. Kisha baada ya kifo cha Mtume[saw] kwa hii maana kuna zama za Masihi Mau'udi anayefanana na Abu Bakr[ra] katika kumuua shetani mlaaniwa. Kwani Masihi Mau'udi amefanywa kuwa Khalifa bila mwingine kuwa katikati, bali kabla Nabii[saw] alikuwa hajazikwa. Na Mola wake Akamshirikisha katika habari za Ukhalifa wa Abu Bakr[ra], yaani zile habari zilizomo ndani ya Kurani, naye pia akajaaliwa uwezo kama Abu Bakr[ra] na azimio kama lake kwa kuzuia mafuriko ya upotevu uhilikishao. Na kwenye hii Akaashiria Mungu Mtukufu Subhana ndani ya kauli yake: 'Usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu;[49] yaani, miaka elfu; na istiara za aina hii zimekithiri ndani ya Vitabu vya zamani. Kisha baada ya elfu hii kuna zama za ufufuo baada ya mauti na zama za Masihi Mau'udi. Basi, leo imetimia elfu ya upotevu na mauti, na baada ya Islam kuzikwa hai ukawadia wakati wake wa kuinuka mara ya pili. Na Enyi mkanao, hoja ya Mungu imetimia juu yenu, hivyo msiwe miongoni mwa wanaomdhania Mungu vibaya; na Enyi wapigao hesabu, hesabuni. Na kwa yakini ahadi ya Mwenyezi Mungu ni haki; basi, maisha ya dunia yasiwadanganyeni wala

---

[49] Sura Al-Qadr 97:4

shetani maluuni asiwalaghaini. Enyi mujaahidi wakosefu, siku hizi ni siku za vita kuu, na ni siku za Masihi kuteremka, na za kutoka kwa shetani kwa ghadhabu wasiyoiona watu waliopita. Kwani, shetani ameishaona kuwa zama zake zimekwisha na wakati wa muhula wake umemalizika, na siku ya ufufuo imewadia. Na muhula wake ulikuwa mpaka siku watu watakapofufuliwa. Hii ndiyo Aliyokuwa Ameahidi Rahmani na Mitume walisema kweli. Na wale wanaojadiliana ndani yake baada ya ushahidi wa Kurani umewafikia, vifuani mwao mna kiburi. Hawa hawanyo haki ya kuikana dalili hii wazi iliyoshuka toka kwa Rahmani. Na hoja ya Mungu Dayani imetimia juu yao, lakini hawataki haki wala mwongozo na wanamaliza umri wao wakiifurahia dunia hii. Je hawakuziona ishara kubwa kubwa? Je haujafika mwanzo wa karne na ufisadi wa umati na fitina kubwa toka kwa maadui wa dini, na kupatwa kwa jua na mwezi na alama zingine? Kama m mashahihi, basi iko wapi takwa?

Enyi watu, mmeishaelewa tuliyoeleza hapo kabla kuwa hesabu za Sura Al-'Asr, kwa hesabu ya *Jummal* zinaongoza kwenye jambo hili kwamba zama zilizopita toka wakati wa Adamu mpaka kushuka kwa Sura hii ni miaka elfu nne na mia saba hivi. Hii ndiyo Aliyonifunulia Mola wangu, nami nikajua baada ya kufunuliwa, na historia pia ikashuhudia juu yake ambayo watu wa Kitabu kwa ujumla wameafikiana nayo pasipo hitilafu. Na mpaka siku yetu hii miaka elfu na

mia tatu imekwishapita baada ya muda huo. Na tunapojumuisha mida hii miwili, hii inakuwa ni miaka elfu sita kama waaminivyo wahakiki wa zamani. Toka hapa yathibitika kwamba kuzaliwa kwangu katika mwisho wa efu ya sita kwafanana na kuumbwa kwa Adamu katika siku ya sita. Na hakuna shaka kwamba mwenye kutumwa mwisho wa elfu ya mauti ameitwa na Rahmani jina Adamu. Hivyo, hii ndiyo miongoni mwa siri za hekima ya Mungu kwamba Akaniumba mwisho wa elfu ya sita ili kuumbwa kwangu kushabihiane na kuumbwa kwa Adamu. Na hii ilikuwa ahadi toka kwa Mungu Mwenye hekima na sifa za namna namna, na kwenye hii Ameashiria ndani ya kauli yake: 'Kwa hakika siku moja kwa Mola wako ni kama miaka elfu mnayoihesabu.'[50] Kwa yakini zama za kuumbwa kwangu ni elfu ya sita, hamna shaka ndani yake, basi waulize wale wanaojua. Na Torati pia imelinena jambo hili, ambalo Waislamu wanaliamini. Na yale yaliyo kinyume cha hesabu hii hayakuthibitika katika maandiko bayana na wajuzi wanaelewa habari hizi. Hivyo, haikuwapasa kukataa hesabu ya Torati na waliyonena Manabii. Na wanawezaje kukataa ambapo Kurani haikuyapinga, bali ikayasadikisha Sura Al-'Asr. Hivyo, pa wapi mahali pa kukimbilia kwao? Basi kwenye hii hii kauli ya Mungu Mtukufu inaashiria: 'Hutengeneza jambo toka mbinguni mpaka ardhini; kisha inapanda

[50] Sura Al-Hajj 22:48

Kwake siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu mnayotumia katika hesabu.'[51] Na someni pamoja nayo aya '*Ilaa yaumi Yub'athuun*' tuliyoiandika kutoka katika Sura As-Sajda. Na ni suna kwamba sura hii inasomwa katika sala ya Alfajiri siku ya Ijumaa. Na Mwenyezi Mungu Mwenye Mibaraka na Utukufu Ananena ndani ya Sura hii kwamba Yeye kwa kuteremsha Furkan Tukufu Akafanya tadbiri ya jambo la sheria na kuwakamilishia

[51] Sura As-Sajda 32:6

Mwenyezi Mungu Amebainisha katika aya hii na kuweka wazi ipasavyo kwamba siku za upotevu baada ya Tabligh ya Kurani ni miaka elfu na baada yake Masihi wa Rahmani atatumwa, basi baada ya kuainisha huku kwa uwazi mabishano yanakwisha, hususan inapounganishwa nayo miaka elfu iliyotajwa ndani ya vitabu vya Manabii wa zamani. Basi tafakari, tena tafakri mpaka upate yakini. Je huwaoni waliowafitini waaminio wanaume na waaminio wanawake★ na wakawaunganisha na jumuiya yao vijidudu wengi na wakauvuruga vuruvuru ulimwengu kwa bidaa zao na wakanuia kung'olea mbali haki kwa porojo zao na kwa kuangamiza sheria ing'aayo wakatumia milima ya dhahabu kama kutiririsha mto wa maji. Je unapatikana mfano wao ndani ya maadui wa awali? Au je Islam iliangukiwa na msiba mfano wa balaa hili hapo kabla? Hutakuta katu tangu Adamu mpaka mwisho wa wakati fitina kama fitina za hawa. Mwandishi

★ Sura Al-Buruuj 85:11

watu dini yao kwa njia ya Neno Lake. Kisha baada yake zitakuja zama ambazo zitarefuka mpaka miaka elfu ambapo Kitabu cha Mungu kitarufaishwa Kwake, na amri yake itapanda kwenye Mwenyezi Mungu kwa jiha mbili, yaani ndani yake haki ya Mungu na haki ya watu zitapotezwa na zitavuma dhoruba kali juu ya namna zake zote mbili na uongo na uzushi utatapakaa, yaani fitina za kidajali, na ufasiki na ukafiri na ushirikina utashinda. Na utawaona wakosefu wakitengana Naye na kusaidia dhidi Yake. Kisha baadaye itakuja elfu ya mwisho ambamo watu watasaidiwa na Mola wa walimwengu, na atatumwa Adamu wa zama za mwisho ili ajadidishe dini. Na kwenye hii hii imeashiriwa ndani ya aya iliyo baada ya aya hii, namaanisha kauli Yake: 'Na Akaanzisha umbo la binadamu kwa udongo.'[52] Binadamu huyu ndiye Masihi Mau'udi na kutumwa kwake kulikadiriwa baada ya kupita miaka elfu tangu karne zilizo karne bora miongoni mwa karne zote, na juu yake limeafikiana kundi la Manabii. Na imo ndani ya ***Sahihain*** — Bukhari na Muslim — iliyosimuliwa na 'Imran bin Husain akisema kuwa Mtume wa Mungu[saw] alisema: Sehemu bora ya umati wangu ni karne yangu kisha wale waliowakaribia, kisha wale waliowakaribia. Kisha baada yao watakuja watu watakaotoa ushahidi ilhali hawataambiwa kutoa, watahini na hawataaminiwa, na wataweka nadhiri lakini hawatatimiza, watanenepa

---

[52] Sura As-Sajda 32:8

sana. Katika riwaya nyingine imo kwamba wataapa ilhali hawataambiwa kuapa. Hivyo, yadhihirika kutokana na Hadithi hii iliyo ***muttafakun 'alaihi*** kwamba zama zilizolindwa na utawala wa uongo ambao ndio miongoni mwa sifa za kidajali, na ni zama za ukweli na wema na utakaso hazitapita zaidi ya miaka mia tatu toka karne ya Seyidna Mbora[saw] wa mahuluku. Kisha baada yake zitakuja zama zilizo kama usiku uliotanda wakati wa kufichika mwezi mpevu, na ndani yake uongo utazagaa, na mwenye kuangamia kwa sababu ya tamaa za nafsi ataangamia. Na kila siku utazidi uongo na maneno ya uzushi. Na uongo utakapofikia ukamilifu basi hii itasababisha kudhihiri kwa Dajali. Na hizi zitakuwa ni siku za mwisho za elfu hii kama itakavyo silsila ya kuzidi uongo na uzushi, na kama ifahamikavyo na Hadithi ya Mtume[saw] wa Mungu Jalali. Na hizo zitakuwa ni zile zama ambamo amri ya Mungu na mwongozo vitapanda juu, na Kurani itarufaishwa kwenye mbingu za juu. Na matukio yatukiayo yanashuhudia kwamba zama hizi chafu zimerefuka hadi miaka elfu, yaani mpaka zama hizi, mpaka nyoka mwenye sumu akawa kama nyoka mwenye sumu kali zaidi. Hivyo, tumefahamu kutokana na hii kwa yakini kamili na maarifa kwamba kauli ya Mungu Mtukufu: 'Kisha litapanda Kwake siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu mnayotumia katika hesabu,'[53] yahusiana na muda

[53] Sura As-Sajda 32:6

huu uliopita katika upotevu, ufasiki na uasi, na ndani yake washirikina wakakithiri isipokuwa wachache walioshika takwa. Na hii ndiyo miaka elfu pasipo kuzidi au kupungua. Basi dalili ipi i kubwa kuliko hii, laiti mngetafakari. Na kama hamkubali, basi tubainishieni nini maana ya aya hii kwa kuacha maana hii, ikiwa mnajua. Je mwadhani kuwa muda wa Kiama pia ni miaka elfu kama miaka ya muda wa dunia, au matendo yatapaa kwenye Mungu ndani ya siku ya Kiama katika muda mfano wake na Mungu Hatayajua hapo kabla? Enyi mpitao kiasi, Mwogopeni Mungu. Na ushahidi gani ni mkubwa kuliko uliokwisha dhihiri kwa hakika, yaani kiasi cha muda ambamo upotevu ulishinda. Kwani, mmeona kwa macho yenu kuwa muda wa zama za upotevu na nguvu yake na kuzidi kwake baada ya karne za wema ziliendelea mpaka miaka elfu kwa haki na ukweli. Je mnakataa hali mwashuhudia? Uongo ukaanzia kama mmea, kisha ukawa mti, mpaka jengo refu la Dajali likadhihiri nanyi mnaona. Ingawaje ulikuwepo hapo kabla pia, lakini pembe zake zikawa kali baada ya karne hizo tatu. Je hamsomi Hadithi kuhusiana na 'Karne'? Elfu hii ilijumuisha kila aina ya upotevu na namna mbalimbali za ushirikina na bidaa na namna tofauti za ufasiki na uasi. Na ndani yake haki za Mungu na haki za watu na haki za mahuluku zimepotezwa. Na mlango ya kuritadi ilifungulika. Basi, dalili ipi mtakubali baada yake. Na Yajuja na Majuja wamefunguliwa na mwaona wanakuja mbiombio toka kila mahali pa juu.

Na hawakutoka ila baada ya karne tatu, na heshima yao haikukamilika isipokuwa kwenye sehemu ya mwisho ya elfu hii. Na pamoja na elfu hii ukakamilika utawala wao. Na ndnai mwake mna ishara kwa watu wazingatiao. Na Kurani inaongoza kwenye siri hii iliyofichika, na yasema kuwa Yajuj na Majuja walizuiliwa na kutiwa pingu hadi siku ya wakati maalum na kisha watafunguliwa katika siku za jua la wema kuzama na katika zama za upotevu kama mnavyoona siku hizi na mnashuhudia. Na kwa wadhalimu yatosha maelezo kiasi hiki. Nami naona kuwa nimekamilisha niliyonuia kusema na kutimiza hoja juu ya wadhalimu. Na hii ndiyo hatima ya tuliyotaka. Basi sifa zote njema ni za Mungu kwa kutimiza jambo hili kwa watafutao haki wa zama hizi.

**Tamati**

Mwandishi: Mirza Ghulam Ahmad

17 Oktoba 1902